# Nipashe

Jumatatu Mei 13, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579916

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Majaliwa aonya migogoro kwenye nyumba za ibada

UKURASA 3







UKURASA 13

# Wastaafu wa PSSSF wasotea mafao miezi 3

**WAPEWA** ahadi kwenda ofisini Dar bila mafanikio......*Endelea Ukurasa. 2*



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisalimiana na Askofu wa Jimbo Kuu la Mwanza, Mhashamu Renatus Nkwande, baada ya kusimikwa katika viwanja vya Kawekamo jijini Mwanza jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Baba matatani tuhuma kuua mwanawe kwa dau la mil. 5/-

UKURASA 21

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MAPENDEKEZO 7 YA CHADEMA UCHAGUZI**

SIKU chache baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kutoa hukumu iliyobatilisha ...

UKURASA WA 2

**UVUVI WA SAMAKI WADOGO RUKSA**

SERIKALI imeondoa katazo la kutokuvua samaki wazazi wa kuanzia sentimita 85, hivyo kuanzia kesho wavuvi...

## Kuingiza mifuko plastiki faini ni mil. 20/-

UKURASA 3

**MICHEZO** BOCCO AISHUKURU SPORTPESA AKIPANIA KUITUNGUA SEVILLA UK. 31

**MAONI** UKURASA 5 II UK.6

# Wastaafu wa PSSSF wasotea mafao miezi 3

**Na Salome Kitomari**

WASTAAFU na warithi wa mfuko wa hifadhi ya jamii wa PSSSF wamekuwa wakikusanyika katika ofisi za mfuko huo Ilala, jijini Dar es Salaam kudai malipo yao ya miezi mitatu.

Wastaafu hao ambao wengine ni wagonjwa walisindikizwa na ndugu zao baada ya kuwenda benki kwa miezi mitatu bila kupata fedha za kila mwezi kwa mujibu wa sheria.

Wakizungumza na Nipashe katika ofisi za PSSSF Ilala, baadhi ya wastaafu walisema kila wanapoenda wanakutana na mtu mpya wa kuwapa majibu yale yale na kuwataka wajiorodheshe majina yao kwenye karatasi kwa ajili ya suala lao kushughulikiwa, lakini hadi sasa hakuna ufumbuzi.

Mmoja wa wastaafu hao, Peter Portas ambaye alistaafu mwaka 2012, alisema hawajalipwa tangu mwezi wa tatu na wa nne, na kwamba walipoenda kwenye ofisi hizo waliambiwa kuwa majina yao hayakuingizwa kwenye mfumo.

Naye Stellah Thomas, alisema alihakiki taarifa zake tangu mwezi wa pili mwaka huu na aliahidiwa kuanza kulipwa mwezi wa tatu, lakini hadi sasa hakuna alicholipwa.

"Leo wanatuambia uingizaji wa taarifa za wastaafu unafanyika Dodoma, sasa tusichoelewa wanataka twende Dodoma? Ni wangapi wataweza kwenda? Nimekuwa nikilipwa pensheni yangu kwa miaka mitatu sasa, lakini kwa sasa tunakumbana na usumbufu," alisema.

Regina Mgema aliyestaafu mwaka 2011, alisema alikuwa analipwa kila mwezi, lakini kwa sasa ana miezi miwili hajalipwa na hawajapewa taarifa rasmi ya kilichokwamisha malipo yao na lini wataanza kulipwa.

"Ilipofika mwezi wa nne niliienda benki, lakini sikukuta chochote nikaamua kuja hapa napo hawana majibu, wanasema masuala yote yanashughulikiwa Dodoma," alisema.

Ramadhani Chandewe aliyestaafu mwaka 2017, alisema alikuwa anapata fedha zake kama kawaida, lakini tangu kuunganishwa kwa mifuko hiyo wanasumbuliwa na maofisa wa Ilala ambao wanasema hawana majibu ya moja kwa moja kwa kuwa makao makuu kwa sasa ni Dodoma.

"Sasa sisi sijui twende Dodoma au twende wapi tupate fedha zetu, nimefanyakazi Mamlaka ya Bandari kwa miaka 60 na hakuna mwezi sikuchangia, imefika wakati wa kunilipa ni tatizo, hawajanilipa na hawana uhakika licha ya kuhakiki taarifa zangu tangu Januari, mwaka huu," alisema.

Deus Ngonyani aliyestaafu mwaka 2017, alisema ametokea Kilombero kwa treni usiku na asubuhi kwenda ofisi za PSSSF ambako alikuta wataafu wengine wenye tatizo kama la kwake.

"Nimefika hapa nimekuta wenzangu wana malalamiko ya mwezi

INAENDELEA UK. 8



Baadhi ya wauguzi wakiapa katika maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani jijini Dar es Salaam jana. Habari Uk. 26. **MPIGAPICHA WETU**

# Chadema yatoa mapendekezo saba muundo Tume ya Uchaguzi

**Na Enock Charles.**

SIKU chache baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kutoa hukumu iliyobatilisha uhalali wa wakurugenzi wa majiji, Manispaa na Halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi nchini, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimepongeza uamuzi huo wa mahakama na kutoa mapendekezo saba.

Uamuzi huo wa Mahakama ulitolewa Mei 10, mwaka huu kwa kubatilisha kifungu cha Sheria ya uchaguzi namba 7 (1) na 7(3) kinachoruhusu watendaji hao kusimamia uchaguzi.

Akizungumza na waandishi wa habari , jijini Dar es Salaam jana , Mkurugenzi wa wa Mambo ya Nje, Mawasiliano, Itikadi na Uenezi wa Chadema, John Mrema alisema wanapendekeza uwekwe utaratibu mpya wa kuteua wajumbe wa tume watakaosimamia uchaguzi nchini tofauti na huu uliopo sasa.

"Uwekwe utaratibu mpya wa kuteua wajumbe wa tume, tunaweza tukafanya utafiti hapo Kenya utaratibu wa kuwapata wajumbe wa tume yao watu wanaomba, wanaangaliwa kwa vigezo na wanafanyiwa usahili, ukiangalia Ghana ipo hivyo hivyo , Afrika kusini hivyo hivyo ,tume hii isiitwe tena Nec bali iitwe TIEC," Mrema alisema.

Akitaja mapendekezo mengine ni kuwapo kwa mfuko maalum wa tume hiyo, kuondolewa kwa zuio la kuishtaki tume mahakamani, matokeo ya urais kupingwa mahakamani, kura ya ndiyo na hapana pamoja na ushindi wa asilimia hamsini kwa wanaopita bila kupingwa na kuruhusiwa kwa mgombea binafsi.

Ijumaa iliyopita Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ilibatilisha kifungu cha Sheria ya uchaguzi namba 7 (1) na 7(3) kinachowaruhusu wakurugenzi wa majiji, Manispaa na Halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi nchini .

Katika kesi hiyo namba 8/2018 ambayo ilifunguliwa na mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Bob Wangwe, aliyewakilishwa na wakili wa kujitegemea Fatma Karume, walipinga kifungu cha Sheria ya Vyama vya Siasa, kinachotumiwa na NEC kuwateua wakurugenzi hao kuwa wasimamizi wa Uchaguzi.

# Uvuvi wa samaki sentimita 85 ruksa

**Na Rose Jacob,** GEITA

SERIKALI imeondoa katazo la kutokuvua samaki wazazi wa kuanzia sentimita 85, hivyo kuanzia kesho wavuvi watavua samaki hao bila kukamatwa.

Aliyetangaza kuondoa katazo hilo katika kijiji cha Kikumbaitale wilayani Chato mkoani Geita ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati akizindua ushirika wa chama cha wavuvi wa mwalo wa Kikumbaitale, na kuwakabidhi hundi ya Sh.milioni tano ikiwa ni kuwawezesha kukuza mtaji.

Hatua hiyo imefuatia matokeo ya utafiti uliofanyika na kubaini nchi za Kenya na Uganda hazikatazi samaki wazazi kuvuliwa, kwa kuwa wakipelekwa sokoni wanapata wateja, huku wafanyabiashara wa nchini wanapopeleka samaki zao katika nchi hizo hukosa soko.

"Wavuvi serikali imesikia kilio chenu cha muda mrefu, hivyo imeruhusu uvuaji wa samaki wa kuanzia sentimita 85 na kuendelea, lakini bado mchakato unaendelea wa kuangalia namna gani ya kuruhusu samaki aina ya ngele, gogogo na furu na kuwekwa kwenye utaratibu wa sheria na kanuni," alisema Ulega.

Ulega alisema suala la wavuvi kutumia nyavu za dabo na singo nalo halijaruhusiwa na linafanyiwa utafiti, hivyo kwa sasa hakuna anayeruhusiwa kuzitumia mpaka utafiti utakapokamilika na serikali itakapobaini kama kuna uwezekano.

Vile vile Ulega aliwataka wavuvi wote nchini kuunda ushirika ili waweze kukopesheka na kukuza mtaji, na kuahidi kuendelea kuwaunga mkono kama walivyofanya kwa wanaushirika wa Kikumbaitale ambao ndio wameufungua mlango wa wavuvi kuunda kikundi ambacho kinatambuliwa na serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Chato, Mtemi Msafiri akisoma taarifa ya wilaya hiyo, alisema idara ya mifugo na uvuvi ina jumla ya watumishi 24, ambapo 19 ni wa mifugo na watano wa uvuvi jambo ambalo linaleta changamoto katika utendaji kazi katika sekta ya uvuvi.

"Wilaya inaendesha shughuli za uvuvi katika eneo la kilomita za mraba zipatazo 896 ndani ya Ziwa Victoria, mkakati wa sasa ni kujielekeza katika uanzishaji wa mabwawa ya kufugia samaki kwenye maeneo ya kandokando ya ziwa, mito mikubwa na mabonde ya mpunga yenye uwezo wa kupata maji ya kutosha na ufugaji kwa njia ya vizimba," alisema Mtemi.

## HABARI KITAIFA

# Kusafirisha, kuingiza mifuko ya plastiki sasa faini mil. 20/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAINGIZAJI nchini na wasafirishaji nje mifuko ya plastiki iliyopingwa marufuku na serikali watapigwa faini ya Sh. milioni 20, kwa kukaidi marukufuku hiyo.

Hatua hiyo ilitangazwa jijini Dar es Salaam jana na Baraza la Taifa la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira (NEMC).

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema kwamba adhabu za wavunjaji wa amri ya serikali zimeainishwa katika 'kanuni za marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki za mwaka 2019, na kwamba adhabu hizo zitatumika kupambana na wakorofi. Kanuni hizo zimetungwa chini ya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

"Uingizaji nchini wa mifuko ya plastiki faini ni Sh. milioni 20 usafirishaji nje ya nchi wa mifuko ya plastiki ni milioni 20; uzalishaji, uhifadhi na usambazaji wa mifuko hii ni milioni 10; uuzaji wa mifuko ya plastiki ni Sh. 10,000; na utumiaji wa mifuko ya plastiki ni Sh. 30,000," alisema Dk. Gwamaka.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, shehena ya mifuko ya plastiki itasalimishwa kwa viongozi wa wilaya, kwamba kila wilaya itatenga eneo maalumu la kuhifadhi mifuko hiyo na umma utatangaziwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo.

Dk. Gwamaka aliitaja mifuko mbadala ni mifuko iliyotengenezwa kwa karatasi, nguo, gunia, vikapu na kadhalika na kufafanua kwamba mifuko ya aina hiyo ni ile ambayo ni rafiki kwa mazingira, ambayo haina madhara kwa afya ya binadamu na mazingira.

Aliwataka Watanzania kutambua kwamba marukufu ya serikali imeibua fursa kwa watu wabunifu kutengeneza mifuko mbadala na kueleza kwamba tayari vipo viwanda vya karatasi 25 nchini na baadhi yake vinatengeneza mifuko mbadala, na kueleza kuwa kuna viwanda vinavyotengeneza mifuko ya nguo. "Vile vile, kuna wawekezaji na wamiliki wa viwanda ambao walikuwa wanasubiri tamko la serikali ili wawekeze mara moja katika utengenezaji wa mifuko mbadala," alisema.

Aliwataka Watanzania wabunifu wenye kutaka kutumia fursa hii kuwekeza katika utengenezaji wa mifuko mbadala wasibabaike wala kusumbuka bali wawasiliane mara moja na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), NEMC, Shirika la Viwango Tanzania (TBS, Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo (SIDO) na Taasisi za Fedha.

Dk. Gwamaka alisema serikali imeunda kikosi kazi kuhusiana na suala hilo linaloratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais na NEMC na kuongeza kwamba serikali inaandaa mpango kazi wa utekelezaji wa katazo hili kwa manufaa ya wananchi.

"Serikali inatoa wito kwa wadau wote wakiwamo wawekezaji katika viwanda kuzingatia umuhimu wa uchumi wa mbadala wa mifuko ya plastiki kwa kuwa utaibua ajira nyingi zaidi na kukuza kipato cha wananchi wa kawaida hasa kinamama katika kutengeneza mifuko mbadala ambako kunahitaji teknolojia rahisi na nguvu kazi," alisema zaidi Dk. Gwamaka.



Mkazi wa kijiji cha Lutende wilayani Uyui, Issa Mtiliga, akitoa neno la shukrani jana kwa wakufunzi kutoka Mpango wa kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) kwa kuwajengea uwezo wakulima 100 waliopimiwa mashamba yao na kupata hati miliki za kimila ili waweze kutumia mtaji huo kuboresha ufugaji wa mifugo ikiwemo kuku wa kienyeji. **PICHA: VICENT TIGANYA**

# Majaliwa aonya migogoro kwenye nyumba za ibada

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka viongozi wa dini nchini kutokuwa chanzo cha migogoro katika nyumba za ibada na taifa.

Badala yake, amewataka viongozi wa dini kutumia nyumba za ibada katika kuliombea taifa pamoja na kujenga dhana ya amani na upendo miongoni mwa wananchi.

Aliyasema hayo jana jijini Mwanza wakati wa Misa ya kumsimika Askofu Mkuu wa Jimbo la Mwanza, Mhashamu Renatus Nkwande, na kueleza kuwa amani iliyopo nchini ndiyo chachu ya kufikia maendeleo.

"Tunawategemea viongozi wa dini katika maombi ya nchi, tuendelee kutumia nyumba za ibada kuliombea taifa, tuepuka migogoro, haipendezi kuona watu wa Mungu wanatumika kuleta migogoro," alisema Majaliwa.

Kadhalika, aliwataka viongozi wa dini kuwaelimisha waumini umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii ili kujikwamua na umaskini.

Alisema Serikali inathamini mchango unaofanywa na sekta binafsi na makanisa nchini katika sekta ya elimu na afya, kwamba serikali itaendeleza ushirikiano huo kwa kuwa umekuwa wa manufaa kwa Watanzania wote.

"Kwa sasa kuna shule za msingi 17,659 nchini na kati ya hizo 204 ni za Kanisa la Roman, shule za sekondari 4,883 na kati ya hizo 260 ni za Kanisa la Roman, kwenye ujenzi wa vyuo vikuu Kanisa la Roman linamiliki Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino Mwanza," alisema Majaliwa.

Aidha, Waziri Mkuu aliwataka maaskofu katika Jimbo Kuu la Mwanza kumpa ushirikiano Askofu Nkwande pamoja na kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali.

"Kuchaguliwa kwako ni ishara nzuri kwa waumini wa Jimbo Kuu la Mwanza, Ni Imani yetu utafuata nyayo za watangulizi wako. Kuwaongoza watu kiroho ni kazi ngumu, lakini jipe moyo utaweza," alisema Majaliwa.

Pia, Waziri Mkuu Majaliwa alichangia mifuko 400 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa Kanisa Kuu la Katoliki Jimbo la Mwanza na Sh. milioni mbili.

**ASKOFU NKWANDE AKEMEA UCHAWI, USHOGA**

Kwa upande wake Askofu Nkwande aliwahutubia waumini waliojitokeza katika misa hiyo aliwataka maaskofu kutokuacha kuelimisha jamii kutokana na uwapo wa imani potofu.

INAENDELEA UK. 8

# Kakobe aenda kanisani kwa Gwajima kumsafisha

**Na Mary Geofrey**

ASKOFU wa Kanisa la Full Gospel Bible Fellowship (FGBF), Zachary Kakobe, jana alikwenda katika Kanisa la Ufufuo na Uzima, linaloongozwa na Askofu Josephat Gwajima, kwa ajili ya kumsafisha kutokana na kashfa iliyompata ya kuonekana akiwa faragha na mwanamke.

Video iliyokuwa ikimuonyesha Askofu Gwajima akiwa faragha na mwanamke ambaye kwenye video hakuonekana sura yake, ilianza kusambaa kwenye mitandao ya kijamii ikiwamo magroup ya Whatsapp kuanzia Jumatatu ya wiki iliyopita.

Askofu Kakobe alifika kanisani hapo kwa ajili ya kuzungumza na waumini wa kanisa hilo huku akiwaeleza kuwa ni fitina iliyotengenezwa kwa ajili ya kumchafua kiongozi huyo wa kiroho na muungano wa makanisa mbalimbali ya kiroho.

Askofu Kakobe alihusisha tukio hilo na shughuli ya kutimiza miaka 30 ya kanisa lake iliyofanyika Mei 5, mwaka huu, ibada iliyohudhuriwa na maaskofu wa makanisa mbalimbali akiwamo Askofu Gwajima kuwa waliitengeneza kwa ajili ya kubomoa muunganiko huo.

Alisema kupitia ibada hiyo iliyohudhuriwa pia na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ilikuwa ya kipekee ambayo ilikuwa lazima aingilie kati kwa kumchafua Askofu Gwajima kwa sababu wengi hawajafurahia ushirikiano ule.

Alisema pia adui hakufurahia Askofu Gwajima kupatana na Makonda ndio sababu ya kuingilia kati ili kuonyesha kuwa ndiye aliyesambaza video ile.

"Wanataka tuamini Makonda ndiye muhusika wa kusamba za video hizi, tumewabaini na hatuwezi kamwe kurudi nyuma," alisikika akisema Askofu Kakobe.

Alimtaka Askofu huyo kutokubali mashtaka juu yake kuhusu uovu huo uliofanywa na watu wenye lengo la kutaka kuharibu na kuvuruga umoja huo.

Akifafanua, alisema kuwa hayupo kwa ajili ya kutetea dhambi ya uzinzi isipokuwa anaeleza uhalisia wa tukio lile ambalo halionyeshi sura ya mwanamke aliyeshiriki naye tendo lile.

"Mimi sina mchezo na dhambi na siko hapa kutetea uzinzi, katika kanisa letu tunapinga vikali dhambi ya uzinzi," alisema Askofu Kakobe.

Makonda alivyohusishwa

Katika sakata hilo, Askofu Kakobe alimtaja Makonda kama mtu ambaye aliwahi kutumiwa na adui kwa ajili ya kuwagombanisha na Askofu Gwajima, lakini baadaye alibaini ukweli na sasa tofauti zao zimemalizika.

Alisema hakuna kitu kinachoweza kuwatenganisha au kuwatofautisha na wataendelea kushirikiana bila kujali mambo yaliyopita. "Mwenye wivu ajinyonge au mnasema ajimalize? Lakini sisi tumempenda (Askofu Gwajima) sasa kuliko wakati wowote ule uliopita. Hawa mafitina walijaribu kupeleka fitina kwa Mkuu wa mkoa Makonda, naye akataka kukubaliana nao, lakini naye ameshtuka," alisema Askofu Kakobe huku akishangiliwa na waumini wa kanisa hilo.

Alisema walipatana na Makonda kwa sababu maaskofu ndio wazee wa taifa na kama Makonda ndiye alikuwa mwenye makosa walipaswa kumuonya na kuzunguza naye na si kutengeneza uadui.

"Kama Makonda ana upungufu, sisi siyo wanasiasa hivyo tunakuwa karibu naye ili tumsaidie vizuri na tutaendelea kuwa karibu naye na tutaendelea kuwa karibu naye tumsaidie,"

INAENDELEA UK. 26

# Wajasiriamali wasaka ujuzi mifuko ya karatasi

**Na Novatus Makunga,** ARUSHA

WAJASIRIAMALI wadogo wa mkoani Arusha, wameanza kujiandaa kutumia fursa ya kupigwa marufuku kwa matumizi ya mifuko ya plastiki kunakoanza mwanzoni mwa mwezi ujao kwa kusaka ujuzi wa kutengeneza mifuko mbadala ya karatasi.

Nipashe iliwakuta wajasiriamali zaidi ya 50 wakihudhuria mafunzo ya muda mfupi ya umahiri wa kutengeneza mifuko ya karatasi katika eneo la Njiro, mjini hapa.

Mmoja kati ya wajasiriamali hao ambaye ni mkulima kutoka kijiji cha Kikatiti wilayani Arumeru, Philip Nanyaro, alisema kupitia mafunzo hayo ya siku moja ameweza kupata ujuzi ambao utamwezesha kutengeneza mifuko 1,000 kwa siku.

"Hii ni fursa ambayo sisi Watanzania inabidi kuitumia ipasavyo badala ya kusubiri ichangamkiwe na wenzetu wa nchi ya jirani kwa kuleta mifuko mbadala, malighafi inapatikana hapa nchini," alisema Nanyaro.

Mwalimu mstaafu Eva Esther Mlamie, alisema hiyo ni nafasi nyingine inayopaswa kuchangamkiwa kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi na kwamba kupitia mafunzo hayo ya muda mfupi amepafa ujuzi wa kutengeneza mifuko ya aina mbalimbali.

"Ni ukweli usiopingika kwamba mifuko ya plastiki ilikuwa janga kubwa la mazingira yetu, lakini pamoja na hali hiyo hatua ya kusitisha matumizi yake inafungua fursa ya sisi wa kipato cha chini kujiongezea kipato," alisema Mlamie.

Mkufunzi wa mafunzo hayo yanayoendeshwa na Chuo cha Tanganyika Polytechnic, alisema wahitimu hao wataweza kutengeneza mifuko kwa kutumia aina tatu za karatasi alizozitaja kuwa ni pamoja na karatasi za manila, kahawia (brown paper) pamoja na za kawaida (plain laper).

"Kwa karatasi za kawaida zinatengeneza mifuko inayobeba bidhaa ama vitu vidogo vidogo, huku karatasi za kahawia kwa bidhaa kama vile sukari, mchele, unga na matunda wakati manila ni kwa mifuko mikubwa inayobeba vitu vingi," alifafanua.

Mollel alisema kwa bidhaa zenye maji maji au mafuta mfano vyakula mifuko itatengenezwa kwa kutumia karatasi zenye tabaka linaloteleza katika upande mmoja wa karatasi.

Mratibu na mbunifu wa mitaala katika chuo hicho Dk. Richard Masika, alisema mafunzo hayo yana hatua tisa, karatasi zinagawanywa katika madaraja matatu kutegemeana na uzito ikihusisha mifuko isiyokuwa rasmi ambayo haiwezi kusimama yenyewe, mifuko ulaya ambayo hutumika kwa ajili ya kubebea zawadi na mifuko inayosimama yenyewe.

Dk. Masika alisema kuwa uzalishaji wa mifuko hiyo ni rahisi kwa kuwa malighafi zinapatikana hapa nchini katika maduka yanayouza vifaa vya uchapaji na ofisini zikiwamo karatasi zenyewe, gundi, mikasi na rula kwa mtaji usiozidi Sh. 100,000.

"Tumewafundisha mpaka mbinu za masoko na tayari kuna soko katika maduka tunayonunua malighafi kwa kuhitaji mifuko itakayotengenezwa na wengine kutaka kuwaajiri hao wajasiriamali," alisema.

# Viwanda, hoja ya Zitto kutikisa Bunge

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BUNGE la Bajeti linaloendelea jijini Dodoma, leo linaingia katika juma la saba huku hoja zinazohusu masuala ya ujenzi, uchukuzi, kilimo, viwanda na biashara zikitarajiwa kuteka mijadala ya chombo hicho cha kutunga sheria.

Kwa mujibu wa ratiba ya iliyotolewa na Idara ya Habari na Elimu ya Bunge, leo wabunge watamalizia mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ulioanza Alhamisi.

Hoja kubwa inayotarajiwa kutolewa ufafanuzi na serikali ni iliyotolewa na wabunge wa upinzani, Zitto Kabwe (Kigoma Mjini) na David Silinde (Momba) kuhusu faida ya matumizi ya Sh. trilioni 18.7 walizosema zimetumiwa na serikali ya awamu ya tano kutekeleza miradi ya maendeleo iliyo chini ya wizara ya ujenzi.

Wakati wa mjadala, wabunge hao walihoji idadi ya viwanda na ajira zilizozalishwa kutokana na matumizi ya kiasi hicho kikubwa cha fedha na namna wizara hiyo ilivyochochea maendeleo ya sekta nyingine muhimu nchini.

Ratiba ya mkutano huo inaonyesha kesho na keshokutwa kutakuwa na mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, hoja za wabunge zikitarajiwa kujikita katika kuishauri na serikali jinsi ya kuimarisha sekta hizo mbili ili kutekeleza azma yake ya kujenga Tanzania ya Viwanda.

Katika mjadala huo wabunge wanatarajiwa kuibana serikali kuhusu kuyumba kwa sekta ya biashara kunakosababisha wawekezaji kufunga biashara na kuwakosesha ajira wananchi.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Alhamisi kutakuwa na mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka ujao wa fedha.

Ratiba hiyo pia inaonyesha Ijumaa utaanza mjadala wa siku mbili wa bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka ujao wa fedha.

Katika mjadala huo, hoja zinazotarajiwa kutolewa na wabunge ni pamoja na mchakato wa ununuzi wa korosho na upatikanaji wa mbolea na viuatilifu nchini.

Wabunge pia wanatarajiwa kuibana serikali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo ambao kwa miaka miwili iliyopita ulikuwa chini ya asilimia 30.



Naibu waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk Mary Mwanjelwa akicheza na kwaya ya Chuo Cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) tawi la Mtwara wakati wa mahafali ya 30 ya TPSC yaliyofanyika Mtwara mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaagiza watumishi wapya kunolewa TPSC

**Na Mwandishi wetu,** MTWARA

SERIKALI imezitaka taasisi zake kupeleka watumishi wapya katika Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) ili kujifunza maadili ya utumishi wa umma baada ya upungufu kadhaa kubainika miongoni mwa waajiriwa hao wapya.

Akizungumza wakati wa mahafali ya 30 ya chuo hicho mjini hapa mwishoni mwa wiki, wahitimu 2,686 wakitunukiwa vyeti katika fani mbalimbali, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, alisema kwa sasa mwongozo unaandaliwa ambao utawalazimisha waajiri wote katika sekta ya umma kupeleka watumishi wao wapya chuoni hapo kujifunza masuala mbalimbali yahusuyo utumishi wa umma.

Alitaja moja ya upungufu huo kuwa ni kuvuja kwa siri za serikali na kwamba tatizo hilo litakoma iwapo watumishi hao watapigwa msasa kuhusu utumishi wa umma na maadili yake.

"Nawaasa waajiri wote kuhakikisha watumishi wao wapya wanapita chuoni hapa, na hii ni lazima na siyo ombi," aliagiza.

Alikishauri chuo hicho kutoa mafunzo na ushauri ambao unaendana na azma ya serikali ya kujenga nchi ya uchumi wa viwanda.

"Hivyo ni matarajio ya serikali kuona chuo kinaendelea kufanya utafiti unaoenda sanjari na kasi ya serikali," alisema.

Aliwataka watumishi wa chuo hicho kufanya kazi kwa weledi, maarifa, ubunifu na kujituma ili kuiwezesha serikali kutoa huduma bora kwa wananchi.

Naibu Waziri huyo pia aliwataka wahitimu kuwa mabalozi wazuri kokote waendako na hivyo kuendelea kukipa chuo jina zuri.

Awali, Kaimu Mkuu wa Chuo, Dk. Emmanuel Shindika, alimweleza naibu waziri huyo kuwa kati ya wahitimu 2,686, wahitimu 787 walitunukiwa cheti cha awali (NTA 4), 711 cheti cha stashahada, 1,185 cheti cha astashahada na watatu shahada ya uzamili.

Alisema chuo kinaendelea kuboresha huduma zake mbalimbali, baadhi yake ni huduma za maktaba, maabara za kompyuta na mifumo ya usambazaji na upokeaji wa taarifa kwa kampasi zake.

Baadhi ya kozi zitolewazo na TPSC kwa ujumla mbali na zile za muda mfupi ni shahada ya kwanza katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, taarifa na nyaraka.

Majukumu mengine ya chuo hicho ni kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma katika nyanja za menejimenti, uongozi, utawala na uendeshaji wa ofisi ikiwa ni pamoja matumizi sahihi ya teknolojia za kisasa.

Mafunzo yanayotolewa na chuo hicho yamegawanyika katika sehemu kuu mbili mafunzo ya muda mfupi ambayo yanalenga katika kuboresha stadi za utendaji kazi za watumishi wa umma na pia mafunzo ya muda mrefu kuanzia mwaka moja hadi mitatu katika maeneo ya uongozi, utawala katika dhana mpya ya utendaji wa kimenejimenti ikiongozwa na usimikaji wa mifumo ya kimenejimenti kama uandaaji wa mipango mikakati, OPRAS, mikataba ya huduma kwa wateja, tathmini za kazi na namna za kuongeza tija katika uzalishaji.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (katika), akikagua ujenzi wa Kiwanda kipya cha kuchakataka nyama cha Eliya Foods Over Seas Limited  Longido mkoani Arusha jana. Kulia ni  Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe na Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Shabbir Virjee. Kushoto ni Msajili wa Bodi ya Nyama nchini, Imani Sichalwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanapa yazindua mfumo mpya wa utendaji

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKA la Hifadhi ya Taifa (Tanapa), limezindua mfumo mpya wa utendaji kazi ndani ya hifadhi, unaogawa madaraka katika ngazi ya kanda nne kuu zilizoundwa ili kuboresha utendaji kazi unaoendana na mfumo mpya wa Jeshi- usu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Tanapa, Jenerali mstaafu George Waitara, alizindua mfumo huo jana  na  kutoa vyeo vipya vilivyoidhinishwanа bodi hiyo kwa viongozi washirika ambao ni Naibu kamishna wa Uhifadhi wawili, Kamishna wa Uhifadhi wa Kanda wanne na Makamishna Wasaidizi waandamizi 14.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari jana na Kamishna Mwandamizi Msaidizi wa Uhifadhi, Pascal Shelutete, alitaja vyeo vingine vilivyotolewa ni makamishna wasaidizi 22 na maofisa wakuu waandamizi saba.

Jenerali Waitara, aliwataka viongozi wapya waliopata kiapo cha utii kutekeleza majukumu yao katika mfumo wa jeshi-usu kwa weledi, nidhamu, bidii, juhudi na maarifa ili kuongezatija katika usimamizi wa rasilimali za wanyamapori na mimea katika hifadhi za taifa pamoja na kuongeza pato la taifa.

Alisema muundo mpya unahusisha Kanda ya Kaskazini,yenye hifadhi za Arusha, Tarangire, Ziwa Manyara, Kilimanjaro na Mkomazi na Kanda ya Mashariki inayojumuisha hifadi za Saadani, Mikumi na Udzungwa Alisema Kanda ya Kusini itasimamia  hifadhi ya Ruaha, Kitulo na Katavi na Kanda ya Magharibi itasimamia hifadhi za Mahale, Gombe, Kisiwa cha Saanane, Kisiwa cha Rubondo, Serengeti pamoja na hifadhi mpya za Burigi, Kamisi Miharamuro, Ibanda a Rumanyika.

Aidha, kazi hiyo ilienda sambamba na kuwatunuku vyeti wahitimu 217 wa mafunzo yaliyochukua miezi sita kwa awamu mbili yaliyohusisha maofisa wa uhifadhi pamoja na waajiriwa wapya.

# Wanafunzi walia  ajali za bodaboda

**Na Mary Geofrey**

KATIKA kuadhimisha wiki ya Kimataifa ya Usalama Barabarani, wanafunzi wa Shule ya Msingi Bunge, wamewataka maderava wa pikipiki kuheshimu sheria za usalama barabarani.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Dunia (WHO) watoto kuanzia miaka mitano hadi 29 ndio wanaopoteza maisha kwa ajali za barabarani.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam, katika kuadhimisha siku hiyo iliyoandaliwa na Kampuni ya Mafuta ya Puma, walisema madereva wa pikipiki hawaheshimu alama za vivuko na hata wanapokuwa wamesimama eneo la kivuko hawasimami.

Zuwena Seleman, mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Bunge, alisema wanapokuwa eneo la kivuko madereva pikipiki hukatiza bila kuangalia usalama wa watembea kwa miguu.

“Tunawaomba madereva wa pikipiki wakifika eneo la kivuko wapunguze mwendo, watii sheria za usalama barabarani na waruhusu wanafunzi tuvuke pindi wanapotuona. Wakati mwingine wakitukuta tunavuka barabara wanatutukana matusi ya kudai tunawachelewesha,” alisema Nelian Edwin, mwanafunzi wa darasa la sita katika shule hiyo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mafuta ya Puma, Dominic Dhanah,

INAENDELEA UK.8

# Mradi wa maji wa bil. 1.8/- wasainiwa

**Na Mohamed Saif**

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (Mwauwasa), imesaini mkataba na Mkandarasi Kampuni ya Bennet Contractors Ltd ya mkoani Mwanza kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji wa Nyashimo, wilayani Busega mkoani Simiyu utakaonufaisha wananchi wapatao 12,000 wa vitongoji vya Bukabile, Bulima na Mwagulanja.

Hafla ya utiaji saini ilifanyikia Mei 10, 2019 wilayani Busega na kushuhudiwa na wananchi, watendaji wa serikali na viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka ambaye alisema zaidi ya asilimia 74 ya wananchi wa Busega watakua na uhakika wa maji safi na salama baada ya kukamilika kwa mradi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mwauwasa, Mhandisi Anthony Sanga, akielezea utekelezaji wa mradi huo alisema ni maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, baada ya ahadi aliyoitoa kwa wananchi wa Nyashimo ya kuwapelekea majisafi na salama.

“Mheshimiwa Rais Dk. John Magufuli alivyopita hapa Nyashimo wakati wa ziara zake aliwaahidi wananchi wa hapa kuwatatulia kero ya maji na aliiagiza Wizara ya Maji kuhakikisha inatekeleza mradi haraka iwezekanavyo,” alisema Mhandisi Sanga.

Alisema mradi utatekelezwa kwa miezi 15 na utagharimu Sh. bilioni 1.8 na unafadhiliwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Aliongeza kuwa utekelezwaji wa mradi ni neema kwa wananchi wa Busega na aliwasihi kuchangamkia fursa zitokanazo na ujenzi wake kuanzia hatua za awali za utekelezaji na alimuagiza Mkandarasi kuhakikisha anatekeleza mradi kwa ufanisi mkubwa na

INAENDELEA UK. 8




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kijiti hiki cha Dk. Mengi kienziwe Serengeti Boys

**HATIMAYE** kwa majonzi makubwa Alhamisi ya Mei 9, mwaka huu familia, wafanyakazi wa IPP na Watanzania kwa ujumla wakiongozwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, walipumzisha mwili wa mpendwa wao, aliyekuwa Mwenyekiti wa Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi katika nyumba yake ya milele.

Dk. Mengi ambaye alifariki dunia usiku wa kuamkia Alhamisi Mei 2, mwaka huu huko Dubai, Falme za Kiarabu, alizikwa kijini kwao, Nkuu Sinde, Kata ya Machame Mashariki wilayani Hai, Kilimanjaro.

Pamoja na mengi mema ya kukumbukwa ya Dk. Mengi, familia ya soka itabaki kumlilia na kumkumbuka daima kutokana na mchango wake mkubwa katika michezo.

Moja ya mambo ya kukumbukwa ambayo hata hayahitaji kuvuta kumbukumbu ya mbali ni jukumu kubwa alilokuwa amekubali kulibeba takriban miezi mitatu iliyopita la kuwa mlezi wa timu ya Taifa ya Vijana chini ya umri wa miaka 17, Serengeti Boys.

Dk. Mengi aliisaidia mengi Serengeti Boys ikiwa ni pamoja na maandalizi ya michuano ya Mataifa ya Afrika chini ya miaka 17 (Afcon U-17) iliyomalizika hapa nchini kwa Cameroon kutwaa ubingwa huo.

Hakika katika hilo, sote tunakubali kwamba Dk. Mengi ameacha alama muhimu katika medali ya soka nchini na Watanzania wataendelea kumkumbuka daima.

Hivyo, wakati huu tukiendelea kuomboleza msiba wa Dk. Mengi na kumuoba mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi, hatuna budi kutafakari na kujitoa kwa hali na mali kwa kuenzi yale yote mema aliyokuwa akiyatenda kwa maendeleo ya taifa letu.

Na kwa wadau wa soka, huu ni wakati sasa wa kujitokeza mapema kupokea kijiti chake cha mlezi wa Serengeti Boys ili kuenzi kazi yake ya kukuza soka nchini.

Nipashe tunatambua lengo la Dk. Mengi lilikuwa ni kuona siku moja Tanzania inatisha katika medali ya soka Afrika na duniani kwa ujumla. Na katika hilo, ndiyo maana bila kuombwa, kwa moyo wake aliamua kuwa mlezi kwenye mzizi wa soka, Serengeti Boys.

Alitambua Tanzania haiwezi kupiga hatua kisoka kama haitawekeza katika soka la vijana ambako ndiko chimbuko lilipo.

Kwa mantiki hiyo, huu ni wakati sasa kwa wadau wa soka kujitokeza kupokea kijiti hicho alichokiachia Dk. Mengi baada ya mauti kumkuta.

Tunatambua wapo Watanzania wengi wenye uwezo wa kubeba jukumu hilo, lakini pia pamoja na wingi huo inawezekana ni wachache wenye moyo wa kuguswa kama ilivyokuwa kwa Dk. Mengi.

Hivyo, Nipashe tukiwa kama wadau wakubwa wa soka nchini, tunawaomba Watanzania wenye mapenzi mema kwa maendeleo ya soka letu kuguswa kwa kukunjua mioyo yao kama Dk. Mengi na kujitokeza kuwa mlezi wa Serengeti Boys.

Ni matarajio yetu wadau wengi watajitokeza kugombania nafasi hiyo na haitasubiri hadi Shirikisho la Soka nchini (TFF) lipige mbiu.

Hilo likitendeka tutakuwa tumemuenzi Dk. Mengi kwa vitendo na hakika tutawafuta majonzi Serengeti Boys ambao ni miongoni mwa Watanzania wengi wanaoendelea kumlilia. Mungu ailaze roho ya Marehemu Dk. Mengi mahali pema peponi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hakuna 'mchawi' Simba, Yanga kufungwa Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

**SOKA** la Bongo kwa miaka ya sasa timu za Simba na Yanga zikifungwa ni kama 'msiba wa mswahili' ambao haukosi sababu.

Watoto wa mjini wanasema kuwa uswahilini mtu akifa, basi itatafutwa sababu ambayo si ya kitaalamu ambayo itaeleza sababu ya kifo cha marehemu.

'Aligombana na bibi kizee mmoja jirani.', mwingine atasema 'Alitembea na mume au mke wa mtu.', wapo watakaosema 'Alipandishwa cheo kazini wenzake wakamuonea kijicho.', vile vile kuna wengine watasema 'Alioa au kuolewa na mtu mwingine, kwa hiyo yule aliyeahidiwa na kuachwa ndiye aliyesababisha.'

Nikiandika hapa sababu naweza kufikisha hata 500 na zisiishe. Soka la Tanzania nalo linafanana na hayo, hasa kwa mashabiki wake ambao wengi wao wanazipenda sana Simba na Yanga.

Mashabiki wengi wa timu hizi hasa wa kizazi cha sasa, hawaamini kama timu zao zinaweza kufungwa na timu nyingine za Bongo kwa kawaida tu kuzidiwa kimbinu kwa siku hiyo na makocha wa timu zingine.

Ndiyo maana zinapofungwa hawakosi sababu. Inakuwa ni balaa moja kwa moja, lawama kwa wachezaji wao, lawama kwa kocha wao, lawama kwa waamuzi, ilimradi tu tafrani.

Ijumaa iliyopita Simba ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, huku watani zao wa jadi Yanga wakidungwa bao 1-0 dhidi ya Biashara ya Mara. Kwenye mitandao ya kijamii na mitaani imekuwa balaa.

Wenye kuwatupia lawama wachezaji wao wapo, makocha wapo, waamuzi wapo na hata ukitazama mechi ambazo Simba au Yanga zinapoteza zinakuwa na vurumai kubwa uwanjani na nje ya uwanja.

Ukisikiliza au kusoma maoni ya mashabiki wengi utagundua kuwa tuna safari ndefu sana kwenye soka.

Ni kama Simba na Yanga ndizo zina haki miliki ya kushinda na timu zingine hazina, badala yake zenyewe zipo kwa ajili ya kuzipa pointi tatu tu timu hizo.

Wakati mwingine sifa zinazotolewa kwa timu hizo haziakisi kile ambacho kinaonekana uwanjani, lakini mashabiki wanakuwa wameaminishwa kuwa timu hizo zina uwezo wa hali ya juu.

Inawezekana ni kweli, zina wachezaji wenye uwezo mkubwa kuliko zingine, lakini hilo halitoshi kufanya timu ishinde kila mechi, hasa kwenye mchezo wa mpira wa miguu. Hata Barcelona, pamoja na kuwa na wachezaji bora kabisa duniani, hufungwa na hakuna maneno, sembuse Simba na Yanga?

Na hii imekuja miaka ya hivi karibuni baada ya timu nyingi za Ligi Kuu kuwa dhaifu, huku Simba na Yanga zikijipigia.

Ni tofauti na mashabiki wa miaka ya '80 ambako pamoja na Simba na Yanga kuwa na wachezaji wenye vipaji na uwezo wa hali ya juu, lakini hazikuwa na uhakika kabisa zinapoenda kucheza na Pamba ya Mwanza, Tukuyu Stars, Sigara, Nyota Nyekundu, Pilsner, Mecco, Ushirika ya Moshi, Bandari Mtwara na nyingine.

Yanga kufungwa mabao 3-0 na Pamba wala haikuwa ajabu na wala hakukuwafanya mashabiki kuhamaki na kutafuta mchawi, bali kuzidiwa tu na wapinzani wao ndicho walichokiamini wakati huo.

Simba kuchapwa na Coastal Union au Mecco lilikuwa ni suala ya kawaida tu haikuwa ajabu kiasi watu waweke mijadala. Ni kwamba timu zinafungwa zinajindaa na mechi ijayo.

Mashabiki wa sasa wao wanachoona ni kwamba hizi timu kufungwa labda na timu za nje tu, lakini hapa nchini zikifungwa, basi kuna 'mkono wa mtu', kitu ambacho si kweli.

Hizi timu za Simba na Yanga pamoja na kuwa na mashabiki wengi kila kona nchini ni timu kama zote za Ligi Kuu, ambazo pia zina baadhi wachezaji kutoka timu hizo hizo zinazocheza nao, hivyo zinaweza kushinda, kufungwa au kutoka sare, na hazina maajabu sana kushinda zingine.

Mashabiki wa soka nchini sasa wanapaswa kuanza kujiandaa kisaikolojia, kwani huko tunakokwenda na Ligi Kuu ikipata udhamini mnono na timu zikijiandaa sawa sawa zikiwa na pesa, ushindani utazidi kuongezeka na Simba na Yanga zinaweza kuzidi kupoteza mechi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu zaidi ya sasa.

Mashabiki wasiwe wanafiki wa kulilia soka la Bongo likue wakati wao wanachotaka timu zao za Simba na Yanga ziwe zinashinda tu. Ili soka likue kwanza inabidi Ligi Kuu iwe na ushindani na moja wapo ni hili la timu yoyote hata kama ni kubwa, kutokuwa na uhakika wa kushinda, kama vile tunavyoona kwenye Ligi Kuu ya England.

BARUA/MJADALA

## Serikali itulipe mafao ya fidia zetu

**Mhariri,**

*POLE kwa majukumu ya kazi. Ninaleta kwako malalamiko ya wakazi zaidi ya 1,000 wa Kata za Mchikichini, Jangwani, Upanga Magharibi zote za jijini Dar es Salaam.*

*Sisi wakazi wa kata hizo tajwa tunaomba kulipwa mafao ya fidia zetu ili kupisha mradi wa Tanesco katika kata ya Mchikichini na Jangwani.*

*Tumekuwa tukifuatilia malipo yetu tangu mwaka 2017 hadi leo bado hatujalipwa. Tumefuatilia fidia zetu kwa Mkurugenzi Tanesco, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, pamoja na kwa Katibu Mkuu hazina, lakini hatujalipwa.*

*Tunaomba tulipwe kwani tumehangaika sana kudai haki yetu. Tumekwenda katika ofisi nyingi lakini hatujafanikiwa, tunakuja kwako utusaidie kutufikishia kilio chetu kwa Rais John Magufuli, kwani watendaji wake wameshindwa kutusaidia.*

*Mbali na hilo, sisi wakazi wa kata hizo tunasumbuliwa na kero ya utiririshaji wa maji machafu kutoka mradi wa Dawasco kata ya Upanga Magharibi.*

**Iddi Funndi Osama,**

*Katibu wa Kamati ya Mazingira na Maji ya mvua kata ya Mchikichini, Jangwani, Upanga Magharibi, Dar*

## Tuyalinde mazingira ya Tandale

*NINAJITOKEZA kwa mara ya kwanza katika gazeti letu hili lililo na kurasa iliyo mahsusi kwa lengo la kutuwezesha tueleze kero na dukuduku mbalimbali tulizo nazo ili ziwafikie wahusika kwa minajili ya kutatuliwa.*

*Mimi ni mkazi wa Tandale jijini Dar es Salaam. Ninakerwa kwa kweli na tabia iliyoenea katika eneo letu inayofanywa na baadhi ya wakazi wenzetu ya kujisaidia ovyo haja ndogo kwenye chupa za maji.*

*Mbaya zaidi wakishajisaidia kwenye chupa hizo za maji huzitupa ovyo kwenye barabara za mitaa mbalimbali na kuziacha bila hata ya kufikiria madhara yake katika suala zima la uchafuzi wa mazingira, lakini pia kwa kuhatarisha afya za wakazi wenzao.*

*Tatizo hili limekuwa ni la muda mrefu na inaonekana kama vile halijapatiwa ufumbuzi pengine kutokana na kufanyika kwa kificho na hasa nyakati za usiku na hivyo kusababisha ugumu kwa sisi wananchi kuwaona wahalifu hao.*


*Ninaomba kupitia kwako Mhariri watu hawa wasio wastaarabu waache tabia zao hizo. Vilevile naziomba mamlaka za kiserikali zilizo katika eneo letu zilishughulikie suala hili kwa ukamilifu kwani linatuathiri kiafya.*

**Raia Mwema-Tandale**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Lyon haijui inachokifuata Ligi Kuu




**Na Adam Fungamwango**

AFRICAN Lyon imekuwa timu ya kwanza msimu huu kushuka daraja, baada ya kuchapwa mabao 3-2 nyumbani kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es salaam dhidi ya Mbao FC.

Timu hiyo imebakiwa na pointi 22 tu ambazo hata ikishinda michezo yake minne iliyobaki itafikisha pointi 34 ambazo tayari zimeshavukwa na timu ambayo inafuatia juu yake, Mwadui FC yeye alama 37.

Lyon ni moja kati ya timu chache ambazo zina bahati ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara.

Imepanda na kushuka kama mara tatu hivi. Kuna timu nyingi huko nyuma zilizokuwa Ligi Kuu zikashuka daraja, mpaka sasa imebaki ni historia tu.

Timu kama Pan African, Tukuyu Stars, Pamba ya Mwanza, Toto Africa, African Sports, Mgambo Shooting, na nyingine nyingi ambazo hadi leo zipo, zimekuwa zikipambana kurejea Ligi Kuu, lakini zinakutana na changamoto za ushindani wa hali ya juu, kiasi cha kujikuta zinashindwa kufanya hivyo.

Kwa African Lyon siyo hivyo. Timu hiyo ikiwa Ligi Daraja la Kwanza kupanda Ligi Kuu kwake imekuwa si tatizo kabisa. Ni kama kumsukuma mlevi kwenye utelezi. Tatizo linakuja pale inapopanda Ligi Kuu.

Mpaka sasa haijulikani huwa inapanda Ligi Kuu kwa lengo gani. Kwa sababu hata ikipanda mikakati ya kuhakikisha inabaki Ligi Kuu haionekani. Hata kama ikibaki, inabaki kwa kudra za Mwenyezi Mungu kwa msimu mmoja ikiwa chupuchupu na unaofuata inashuka. Wakati mwingine inapanda msimu huo huo na kushuka msimu huo huo. Ni kama msimu huu. Ilipanda na kucheza Ligi Kuu mwanzoni mwa msimu wa 2018/19, lakini msimu huu huu imekuwa ni timu ya kwanza kushuka daraja. Ikumbukwe kuwa ilitumia msimu mmoja tu kupanda.

Angalau ilionekana ina nguvu ilipopanda na kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu wa 2008/09, ikiwa chini ya Mohamed Dewji ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Bodi ya Klabu ya Simba na mmoja anayemiliki asilimia 49 ya hisa.

Chini yake angalau ilileta ushindani na kuwa na wachezaji bora kabisa akiwamo Mbwana Samatta, Yusuph Soka, Rashid Gumbo na wengineo.

Ilicheza Ligi Kuu kwa misimu mitano hadi ilipoteremka daraja msimu wa 2012/13. Baada ya Dewji kuitema hadi leo haijarejea kuwa yenye ushindani, hasa inapokuwa kwenye Ligi Kuu.

Imekuwa ni timu yenye ushindani na nguvu kubwa inapokuwa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara. Ilikaa kwa misimu mitatu chini na ikafanikiwa kupanda msimu wa 2016/17, lakini msimu huo huo ilishuka daraja.

Msimu uliofuata ikapambana na kupanda Ligi Kuu iliyochezwa msimu huu, lakini imeshuka tena daraja.

Ni haki kwa timu hiyo kama inafanya vizuri kupanda, lakini pia inapaswa kupambana na kuonyesha ubora wake angalau kwa kudumu hata misimu mitatu na kuwa na malengo ya kufika mbali zaidi kuliko kupanda na kushuka kila msimu.

Tumeona timu kama Alliance, Biashara zilizopanda msimu huu ambazo pamoja na kwamba ziko kwenye hali mbaya, lakini zinaonekana zina viongozi thabiti wanaopambana na kuzifanya timu zao kuleta ushindani mkubwa kwenye ligi.

Timu zingine ambazo zimeleta mapinduzi makubwa ni KMC ya Kinondoni na Lipuli ya Iringa ambazo pamoja na ugeni wao kwenye Ligi, lakini mipango madhubuti ya viongozi wao ni kama zaidi ya timu za siku nyingi kwenye Ligi Kuu.

Mashabiki wa soka nchini wanahitaji timu za aina hiyo ili kuleta ushindani kwenye ligi na si timu za aina ya African Lyon tena ambazo zinaonekana zinacheza soka kwa mazoea.

Ni timu hii hii ambayo ilikuwa inatishia kujitoa kwenye ligi kwa kukosa pesa na kama ingefanya hivyo, basi ingevuruga msimamo wote na kuzipa hasara ya pointi na gharama baadhi ya timu.

Kwa jinsi ilivyo timu hiyo, viongozi wa Lyon inabidi wakae tena chini watafakari mustakabali wa klabu yao na kama imewashinda, basi waipige bei kwa watu ambao wanahitaji kuwekeza nguvu zao na pesa kwenye soka.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**



## Wanafunzi walia ajali za bodaboda

INATOKA UK. 5

alisema wameamua kuitumia siku hiyo kutoa elimu kwa madereva kuhusu kuzingatia sheria za usalama barabarani.

"Puma tumeungana na WHO kutoa elimu ya usalama barabarani kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Bunge ambao ni mabalozi wa elimu ya usalama barabarani hususani kwa Mkoa wa Dar es Salaam," alisema.

Alisema wameamua kuwatumia watoto kutoa elimu ya usalama barabarani kwa lengo la kuongeza uelewa kwa madereva hususani wa pikipiki kuhusu masuala ya usalama barabarani.

Dhanah alisema kampuni ya Puma Energy itaendelea kushirikiana na taasisi zitakazoendesha mipango mbalimbali ya usalama barabarani kwa lengo la kuhakikisha kuwa watu wanakuwa salama.

Awali Meneja Mpango wa Usalama Barabarani waWHO, Neema Swai, alisema kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Sema Usikike, Okoa Maisha' na kufafanua maadhimisho hayo huadhimishwa kila baada ya miaka miwili.

"Kila siku watoto ndio wanaotumia barabara kwenda shule na kurudi nyumbani, wasipokuwa na elimu ya kutosha tutawapoteza wengi. Mtambue, kwa mujibu wa takwimu WHO, watoto wenye umri kati ya miaka mitano hadi 29 wanapoteza maisha kwa wingi kutokana na ajali, si Malaria wala ugonjwa mwingine ni ajali," alisema Swai.

Kwa mujibu wa takwimu za WHO nchini, watu 32 wapoteza maisha katika ajali 100,000 zinazotokea, huku madereva wa pikipiki wakiongoza kwa asilimia 28 na watembea kwa miguu kwa asilimia 26.

## Mradi wa maji wa bil. 1.8/- wasainiwa

INATOKA UK. 5

kutoa kipaumbele kwa jamii inayozunguka kuwa ya kwanza kunufaika.

ayokabidhiwa kwa niaba ya Wizara ya Maji na alimsisitiza aendelee na moyo huo wa kizalendo na aliipongeza Bodi ya Wakurugenzi na wafanyakazi wa Mwauwasa.

Naye Mbunge wa Jimbo la Busega Mkoani Simiyu, Dk. Raphael Chegeni, aliyekuwa miongoni mwa viongozi walioshuhudia tukio hilo, alisema kero kubwa waliyokuwa nayo wananchi wa jimbo lake ni ukosefu wa majisafi na salama na tayari mwarobaini wake umepatikana.

Kwa upande wake, mwakilishi wa Mkandarasi, Sabato Boas aliahidi kutekeleza mradi kwa muda mfupi kadiri itavyowezekana na kwa utaalam unaotakiwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa kwenye mkataba.



Meneja wa PSSSF mkoa wa Ilala, James Mlowe, akitoa ufafanuzi kwa wastaafu waliokosa pensheni kwa miezi mitatu. **PICHA: SALOME KITOMARI**

## Wastaafu wa PSSSF wasotea mafao miezi 3

INATOKA UK. 2

Machi na Aprili, nilikwenda wilayani wakaniambia kuna makosa yamejitokeza ambayo yako nje ya uwezo wao labda niulizie makao makuu, baada ya kuona hakuna jibu na fedha haziingii nikaamua kuja hapa nako hakuna majibu," alisema na kuongeza:

"Suala hilo lilinikera sana na hapa nilipo ninadaiwa, nitaishije na sina mahali pa kukopa, Meneja wa mkoa naye anasema tatizo ni mifuko kunganishwa kumesababisha wengine wakose mafao, nilikuwa napata pensheni yangu hadi rais anatangaza mifuko iaunganishwa, ila sasa hatujui nini kimetokea hatupati fedha."

Mstaafu mwingine alisema awali walipokea ujumbe ukiwataka wajisajili na alichagua kwenda mwezi wa pili, na alipofika mapokezi aliambiwa hahusiki kwa kuwa wanaohakikiwa ni kutoka mifuko mipya.

Mstaafu huyo alisema aliamua kurudi nyumbani, lakini kwa miezi miwili hajapata na alipofuatilia walimwambia ni kwa sababu hajasajiliwa.

"Niliwauliza mbona hamkutujulisha kuwa lazima tusajiliwe, mwezi Aprili nilijisajili, lakini leo kama unavyoona wapo wengi nao hawajalipwa kama mimi," alisema.

Naye, Rukia Mavura, mjane ambaye anafuatilia fedha za warithi, alisema hajapata fedha ambazo anazitegemea zimsaidie kwenye matibabu na malezi ya watoto wake kwa miezi miwili sasa na hajui afanyeje ili aendelee kuishi.

"Hapa unaponiona nina upungufu wa damu na mikono na miguu yangu inakufa ganzi, macho hayaoni kwa sababu ya upungufu wa chakula, hapa nilipo sina fedha ya chakula wala kwenda hospitalini, Meneja anasema suala letu linashughulikuwa na hana uhakika lini hasa tutalipwa, naomba mnisaidie jamani nitakufa, nalala njaa na watoto," alisema huku akitokwa na machozi.

Mjane Naomi Magesa, alisema hajalipwa tangu mwezi wa tatu na kila wakifuatilia wanaambiwa wasubiri kwa kuwa mifumo ilikataa majina yao.

Abdalah Bombo aliyestaafu 2015, alisema PSSSF walishachukua fedha zao kwa miaka 60, lakini imefika wakati ambao wanatakiwa warudishe kwa sababu wastaafu wanawakwamisha.

"Nimeshadanganya watu walionikopesha hadi naonekana muongo, ukija PSSSF wanabadilisha watu, leo unamkutana Juma kesho Jonas, wanatufanya kama watu tusiostahili, hii ni mara ya nne sasa nakuja hapa na hakuna suluhisho," alisema.

Alisema wanachofanya ni kuwaweka sawa na siyo kutatua matatizo yao na kuhakikisha wanalipwa, wanawapiga danadana na familia zao zinaumia na kwamba ni vyema wawaeleze ukweli ni wakati gani fedha zitaanza kulipwa na siyo kusema data inatema majina yao wakati wamesoma.

Rebeca Mchau aliyestaafu 2010, alisema hadi sasa hakuna jibu lolote la kuonyesha lini watalipwa, na kwamba fedha hizo alitarajia kumlipia ada mjukuu kwake ambaye amefiwa na wazazi wake na sasa ana zaidi ya wiki mbili hajaenda shule.

**MAJIBU YA PSSSF**

Meneja wa PSSSF Mkoa wa Ilala, James Mlowe, alithibitisha kuwapo kwa tatizo hilo kutokana na mfumo mpya baada ya mifuko kuunganishwa na kwamba katika kuingiza majina ya wastaafu wapo waliosahaulika, licha ya kufanya uhakiki.

"Tunafanya tunaloweza kuwa kabla ya Mei 25, mwaka huu, wawe wamelipwa fedha zao zote za nyuma, hili ni tatizo la kimfumo lilijitokeza ila linashughulikiwa," alisema na kuongeza:

"Baada ya uhakiki wa wastaafu kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu, ambao hawajahakikiwa walitolewa kwenye daftari, wapo waliohakikiwa, lakini mfumo haukuwatambua kutokana na uchanga wa mfumo husika."

Mlowe alisema PSSSF ina wastafu 124,000, na kwamba kitakachofanyika kwa sasa ni kuandaa malipo kwa ajili ya wachache ambao majina yao yalirukwa wakati wa kuingiza taarifa kwenye mfumo.

## Majaliwa aonya migogoro kwenye nyumba za ibada

INATOKA UK. 3

"Tumekuwa tukisikia kinamama wanakatwa mapanga kutokana na imani za kishirikina, watu wanazungumzia uchawi, mtu anavimba tumbo au anashindwa kukojoa wanasema amerogwa, mimi huwa naita ni ushamba wa kukosa elimu. Sisi maaskofu tunapaswa kuwaelimisha na kuwaombea na kuwaambia kuwa kupitia Mungu wataokoka," alisema Askofu Nkwande.

Alisema maaskofu wanaweza kuwakomboa wananchi wenye imani potofu kupitia shule, na ndiyo maana Kanisa Katoliki limekuwa likijenga shule pamoja na vituo vya afya, lengo kuu likiwa jamii yote ya Watanzania wakombolewe.

Kadhalika, aliwataka Watanzania kuacha kuiga mambo kutoka Ulaya ikiwamo utoaji mimba na vitendo vya ushoga.

Alisema kitendo cha utoaji mimba ni mauaji na hakina tofauti na mtu aliyerusha bomu katikati ya watu.

Askofu Nkwande aliitaka Serikali kutokuwa wapole katika kukemea vitendo vya utoaji mimba na ushoga kwa kuwa vinakwenda kinyume cha Mungu.

"Na nyie serikali mkibanwa kidogo mnalegalega, kwa sababu hao watu wanawasaidia, lakini ukweli utoaji mimba ni mauaji," alisema Askofu Nkwande.

Alisema kwa sasa ni jambo la kawaida kuona taasisi kushangilia na kusaidia vitendo vya utoaji mimba na ushoga nchini, kwa sababu zimekuwa zikipata misaada kutoka kwa wakoloni.

Akitoa mahubiri Askofu Mkuu Mwandamizi wa Jimbo kuu la Dar es Salaam Mhasham Jude Thadei Rwai 'chi ambaye awali alikuwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Mwanza, aliwataka waumini kudumu katika kumjua Mungu na kumtumikia siku zote.

Akieleza Baraka zilizopo jimboni hapo Askofu Rwai'chi alisema wakristu wengi ni watoto na vijana na wanahitaji mafundisho, malezi, kuongozwa na kulindwa katika zama ambazo ni za dhoruba nyingi.

Misa hiyo ilihudhuriwa na mamia ya watu kutoka maeneo mbalimbali ndani ya mkoa wa Mwanza, na mikoa ya Shinyanga, Geita, Mara, Kagera na Simiyu.

**Imeandikwa na Rose Jacob, Elizabeth Faustine (Mwanza) na Gwamaka Alipipi (Dar).**

# Wanafunzi watoa suluhisho la mabomba kupasuka ovyo

**Na Salome Kitomari**

WANAFUNZI wa mwaka wa tatu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), wanaosoma TEHAMA, wametengeneza teknolojia rahisi ya kukabiliana na maji yanayovuja kwenye mabomba ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa).

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, wakati wa maonyesho ya wiki ya utafiti yaliyoandaliwa na chuo hicho, kiongozi wa wanafunzi watafiti, Lucas Alfayo, alisema kwa miezi mitatu wanafanya kazi na Dawasa kukamilisha mifumo na mitambo.

"Katika utafiti wetu tulibaini changamoto inayoikabili Dawasa kuwa ni presha kubwa ya maji ambayo hupelekea mabomba kupasuka na maji kumwagika, kuchafuka kabla ya kumfikia mtumiaji, jambo ambalo ni hasara kwao," alisema.

Alisema wako wanafunzi 37, lakini waliojikita kweye eneo la presha ya maji ni 11, na kwamba kinachotakiwa ni presha isizidi wala kupungua kwa kuwa ikizidi inasababisha mabomba kupasuka na hasara.

"Kwa kipindi cha miezi mitatu tumetengeneza mtambo mdogo kama njia ya kuwasaidia Dawasa kuhakikisha wanatoa maji yenye presha nzuri na yanamfikia mteja na kutowapunja, kwa kuwa wakati mwingine presha ya Bagamoyo inaweza kuwa kubwa kuliko ya Mbezi na kuwapo kwa wateja wanaokosa maji," alisema.

Aidha, alisema kwenye mtambo wao kutakuwa na vifaa maalumu ambavyo vitawekwa kwenye mabomba ya Dawasa ya maji kwenye maeneo mbalimbali.

Kwa mujibu wa Alfayo, katika utafiti wao walibaini kuwa Dawasa inakabiliwa na changamoto hiyo kwa kiasi kikubwa kwa kuwa wakitaka kujua presha ya maji ni lazima waende kwenye maeneo husika na kurekodi data kwenye karatasi na kuzipeleka ofisini.

"Mtambo wetu utatuma data moja kwa moja ofisini ambako kutakuwa na mtaalam wa mitambo ambaye atasimamia presha ya maji ya maeneo yote," alisema. "Kwa sasa ni hadi watu waripoti Dawasa, lakini kwa mtambo wetu maji yakianza kuvunja data zitakwenda moja kwa moja na kuwawezesha mafundi kujua eneo lenye tatizo kwa haraka," alifafanua.

Alisema kundi jingine la watafiti wanaangalia usafi wa maji na kama uchafu utapenya data zitapelekwa ofisini.

"Tunashirikiana na Dawasa kwa karibu sana na ikifika Julai, mwaka huu, tuwe tumemaliza na mfumo ujaribiwe. Tunawashukuru sana kwa kuliona wazo letu na tunatarajia watalitumia nasi tutanufaika kwa kupata ajira," alisema.

Alisema kununua tekonolojia nje ni gharama kubwa sana na itahitaji mtu kutoka nje kuiendesha ambaye ataajiri watu kutoka kwenye nchi yake, na kwamba Watanzania wana kazi za kibunifu zinazohitaji ushirikiano.

Akizungumza wakati wa kufungua wiki ya maonyesho ya UDSM, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William Anangisye, alisema kwa kutambua umuhimu wa ubunifu na utafiti wametenga Sh. bilioni moja kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya watafiti wanafunzi na wakufunzi.

Naye, Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Prof. Joyce Ndalichako, alivitaka vyuo vikuu nchini kuchapisha tafiti zao kwenye majarida ya kimataifa ili kuvifanya vishinde nafasi nzuri kwenye upangaji wa vyuo duniani na Afrika.




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Bunge, ambao ni Mabalozi wa Puma Energy, Said Mdachi na Swaum Abdallah, wakiwa na mabango yenye ujumbe, wakitoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva katika kituo cha mafuta cha Puma Ocean Road, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kampuni ya Puma Energy Tanzania ilipoadhimisha Wiki ya Usalama Barabarani ya Umoja ya Mataifa. **PICHA: JOHN BADI**

# Waazimia kuongeza uzalishaji alizeti, pamba

**Na Tiganya Vincent**

WAKULIMA wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui mkoani Tabora, wameazimia kuongeza uzalishaji wa zao la alizeti na pamba kwa ajili ya kujiongezea kipato na kuvutia wawekezaji katika sekta ya viwanda.

Azimio hilo lilifikiwa juzi na wakulima 200 na viongozi 20 wa vijiji vya Miyenze na Lutende wilayani Uyui baada ya kupata mafunzo ya kuwajengea uwezo kutoka Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (Mkurabita).

Akisoma maazimio ya wakulima, Meneja Urasimishaji ardhi Vijijini kutoka MKURABITA, Anthony Temu, alisema wakulima wamekubaliana kulima ekari sita za alizeti na ekari tatu za pamba na mazao ya chakula kwa ajili ya kuinua uchumia wao.

Alisema ongezeko hilo la kilimo linakwenda sambamba na mtumizi ya mbegu za kisasa za alizeti na kulima kulingana na ushauri wa wataalamu wa kilimo ili kuwa na malighafi nyingi zitakazovutia wawekezaji kwenda Uyui.

Aidha, wakulima hao walikubaliana kuanza kuwa na kilimo biashara kwa ajili ya kuongeza tija katika kilimo chao na kuondokana na umaskini unaotokana na uzalishaji wa mazoea wa uzalishaji wa kujikimu na kuelekea katika uzalishaji wa ziada.

Katika hatua nyingine, walikubaliana kuanzisha chama cha ushirika wa wafugaji ili kuunganisha nguvu katika kutafuta huduma mbalimbali ikiwamo ya kupata dawa za mifugo kwa urahisi na uuzaji wa bidhaa za mifugo kwa bei nzuri.

# Kairuki azigeukia halmashauri

**Na Magreth Magosso,** KIGOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, ameziagiza halmashauri zote zitenge Ardhi ya uwekezaji na kuweka miundombinu ya maji, nishati na barabara za lami ilikuwavutia wawekezaji na wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi.

Alitoa maelekezo hayo juzi mjini Kigoma katika ufungaji wa kongamano la biashara la nchi zinazozunguka Ziwa Tanganyika lililowakutanisha wajumbe zaidi ya 195 kutoka Zambia, Burundi, Rwanda, DRC na Tanzania, baada ya kuainisha vikwazo 24 kwa wawekezaji na wafanyabiashara na mchi hizo kuingia katika uchumi wa viwanda.

Vikwazo hivyo ni pamoja na vizi ya fedha Dola 50 inayotozwa nchini kwa wafanyabiashara wa nchi jirani, mrundikano wa tozo katika bidhaa hasa tozo zisizo na ulazima, urasimu wa vibali katika uwekezaji na utoaji wa bidhaa.

Waziri Kairuki alisema mabadiliko yanahitajika na kuutaka Mkoa wa Kigoma kupitia jiografia yake kutenga eneo maalum kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda na kuagiza mikoa isiyotenga ardhi ya uwekezaji ifanye hivyo kwa kuboresha miundombinu ya msingi kwa kushirikiana na mamlaka za maji na Shirika la Umeme (Tanesco) pamoja na za barabara.

"Namwakilisha Makamo wa Rais kufunga kongamano hili la siku tatu, lakini Serikali inafanya mabadiliko ya uchumi...ajenda kubwa mwaka 2019 ni mwaka wa uwekezaji, tunaboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, mmeorodhesha changamoto 24 kuwa ni kikwazo hasa suala la viza kuwakimbiza wafanyabiashara wa kikongomani kutumia bandari zetu, lakini kuna baadhi ya watumishi wanatoza tozo feki kinyume cha sheria, watawajibishwa," alisema Kairuki.

Alisema wajumbe wa kongamano hilo watoe mrejesho mbadala wa changamoto 24 mtambukwa ili atakapokuja na jopo lake la mawaziri siku za usoni wakamilishe matunda ya kongamano hilo kwa kuimarisha mazingira rafiki kwa wawekezaji na wafanyabiashara wa nchi zinazotumia Ziwa Tanganyika. "Nchi yetu inashika nafasi ya 141 duniani katika viashiria 11 vya sifa ya uwekezaji rafiki, mimi sijaipenda hii namba, kiukweli tunataka wepesi wa kuondoa usumbufu na vikwazo vinavyopelekea kuzorota kwa biashara mipakani, tunasikiliza na kuzitafutia fumbuzi vikwazo na tunaelimisha watumishi wa kila taasisi husika, iwajibike katika eneo lake isifanye kazi isiyomhusu," alibainisha.

# UDSM yabuni chakula cha samaki bei nafuu

**Na Salome Kitomari**

CHUO KIKUU cha Dar es Salaam, kimebuni chakula cha samaki cha bei nafuu, kinachoweza kutengenezwa na mkulima mwenyewe, huku kikiwa na protini nyingi kuliko vya viwandani.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, wakati wa kilele cha maonyesho ya utafiti chini ya kauli mbiu ya 'utafiti kwa maendeleo jumuishi na endelevu', Mkufunzi Dk. Shadrack Ulomi, alisema chakula hicho kinatengenezwa kwa funza, mende na majani ambayo yanapatikana kirahisi.

Alisema utafiti wao umekuja na matokeo ya kuweza kutengeneza chakula cha samaki ambacho hakitumii dagaa ambavyo kina protini kwa wingi.

"Kuna mimea ina protini nyingi sana, mfano Azola na Lusina zina protini ya asilimia 25 hadi 30, wadudu wanaofugika kama funza wenye protini hadi asilimia 60 na madini mengi, na mende wana 45 hadi 60," alisema. Kwa mujibu wa Dk. Ulomi, protini hiyo ndiyo inayotumika kutengeneza chakula cha samaki, na huchukua mimea hiyo wanaikausha na kuchanganya na vitu vingine kama pumba na vitamini B.

Alisema funza na mende wanaweza kukaushwa na kusagwa pamoja na kisha kuchanganywa na pumba, na kuongezwa virutubisho vingine vya vitamini na kuwa na chakula bora cha samaki.

"Tumeshaona chakula tunachotengeneza kwa kutumia hivi vitu ni kizuri sawa sawa na kinachotoka viwandani kinatumia dagaa. Tunataka kuokoa dagaa ambao wanapotea ziwani na mfugaji wa chini apate vitu rahisi vya kutengenezea chakula," alibainisha.

Dk. Ulomi alisema chakula cha samaki kinatumia zaidi ya asilimia 65 ya gharama za uzalishaji, na kwa kwamba ili kumuwezesha mkulima kupata faida si lazima protini ipatikane kwa bei na njia rahisi.

"Ukipata protini kwa bei rahisi ndiyo namna pekee ya kupata faida kwenye ufugaji wowote uwe wa samaki au mwingine," alisisitiza.

Alisema utafiti huo wanausambaza kwa wakulima kwa njia mbalimbali na kwamba wapo tayari kutoa ushirikiano kwa watu mbalimbali ambao watahitaji elimu hiyo.

Aidha, waliiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kueneza teknolojia hiyo iwafikia wakulima wengi wa samaki, na kwamba UDSM iko tayari kushirikiana nao kutoa elimu hiyo.

Kuhusu mkulima wa kawaida kuzalisha funza, alisema ni jambo rahisi kwa kuwa takataka zikikusanywa inzi akitua atataga mayai ambayo yataanguliwa na kuwa funza.

Alisema funza watadumu kwa siku sita na inapofika siku ya saba hubadilika na kuwa inzi na wanaondoka, na kwamba inatakiwa kuwachukua kabla ya siku ya saba.

Kuhusu kuzalisha mende, alisema ni rahisi zaidi kwa kuwa ukishampata mmoja na kuweka kwenye chombo na kuwa mwanzo wa kufuga na kwamba chakula chake ni wanga kama unga wa viazi na mahindi, pakiwa na unyevunyevu wanazaliwa kwa wingi.




Ofisa anayehusika na usajili wa laini za simu kutoka kampuni ya Tigo Tanzania, Atupiani Makweta, akimsajili Mbunge wa Tunduma, Frank Mwakajoka, kwa kutumia mfumo mpya wa usajili kwa kutumia alama za vidole mwishoni katika viwanja vya Bunge mjini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lukuvi ateua wenyeviti wa mabaraza ya ardhi, nyumba

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameteua wenyeviti wapya wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba 20 na wengine 42 kupangiwa vituo mbalimbali kwa lengo la kuboresha na kuleta ufanisi katika Mabaraza.

Waziri alifanya uteuzi na mabadiliko hayo kutokana na mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (1) cha Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura 216.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara, Wenyeviti wapya 20 walioteuliwa ni Rajabu S. Mnyukwa Mwenyekiti wa Baraza Kilosa, Edward Mhina (Nzega), Nadhiru Ngukulike (Tarime), Rebeca Mjanja (Lindi), Hussein Lukeha (Mtwara), Augustine Lugome (Kyela), Baraka Shuma (Iramba) na Tendai Chinolo (Lushoto).

Wengine ni Mtengeti Sangiwa (Njombe), Jackson Kanyerinyeri Maswa, Jacob (Rungwe), Ntumengwa Ntumengwa (Mbulu), Justina Lwezaura (Rukwa), Jesca Mugalu (Mbinga), Reginard Mtei (Bukoba), Jimson Mwankenja (Morogoro), Bahati Ndambo (Chato), Richard Mmbando (Ulanga), Felix Frederick (Mpanda) pamoja na Ngassa Maduhu (Ukerewe).

Uteuzi wa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba wa Wilaya ni wa miaka mitatu kuanzia April 1 , 2019 .

# Neema zaidi ya watalii

**Novatus Makunga,** ARUSHA

KUNDI la watalii 336 lilitarajiwa kuwasili nchini jana na leo watashiriki katika kongangamo la kimataifa la uwekezaji mjini hapa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Utalii (TTB), Devota Mdachi, alisema kuwa watalii hao wanakuja kutangaza vivutio vilivyopo nchini kupitia mkakati unaofahamika kama 'Tour Africa- New Horizon visit to Tanzania'.

Alisema watalii hao watakuwapo nchini kwa siku nne na kutembelea hifadhi za taifa za Manyara na Serengeti, Bonde la Ngorongoro, Olduvai Gorge na katika maeneo ya utalii wa utamaduni.

Alisema katika msafara huo wamo wawekezaji 54 kutoka makampuni na wafanyabiashara 27, waandishi wa habari 40 pamoja na wadau wa utalii. Wamo pia wasanii na watu maarufu pamoja na maofisa wa Serikali ya China.

Alisema ujio huo umefanikiwa kutokana na ubia walioanzisha bodi yake na kampuni ya kimataifa ya Touchroad International Holding Group ya nchini ambayo inaendesha shughuli zake katika nchi zaidi ya 30 duniani pamoja na balozi wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki.

"Baada ya ziara hiyo tunategemea kuwa watalii kutoka China watamiminika, lakini pia tutashirikiana kuratibu safari za moja kwa moja za ndege za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)," alisema.

Alisema kongamano la Jumatatu la uwekezaji kati ya China na Tanzania, litafunguliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki.

Alisema kongamano hilo linatarajia kuwakutanisha wafanyabiashara na wawekeza wa kampuni zilizojikita katika nyanja mbalimbali zikiwamo za uimarishaji wa biashara ndogo na kati, utafiti na maendeleo, viwanda, utalii, utamaduni, ujenzi, nishati, mafuta na gesi.

"Kongamano limelenga kuvuta uwekezaji, mitaji na teknolojia na kutangaza fursa mbalimbali zilizopo nchini zikiwamo za Kilimo, ufugaji, madini, uchakataji ngozi, pamoja na viwanda na usindikaji wa mbogamboga," alifafanua.

Alisema Kongamano hilo kwa upande wa Tanzania litawashirikisha wafanyabiashara na kampuni zaidi ya 90.

Kadhalika, alisema Balozi Kairuki na mwenzake wa China nchini, Wang Ke pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Geofrey Mwambe, ni miongoni mwa watakaohudhuria kongamano hilo.

Akizungumzia kongamano hilo Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha wafanyabiashara, wasindikaji na wasafirishaji wa mbogamboga, viungo, matunda na maua (TAHA), Jaqueline Mkindia, alisema wanatarajia kulitumia kufungua soko jipya nchini China hususan la parachichi.

Mkurugenzi Mkuu wa Uhifadhi kwa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Dk Allan Kijazi na Mkurugenzi wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Dk. Fred Manongi, walieleza kuwa wamejiandaa kikamilifu kuhakikisha wanaongeza idadi ya watalii katika maeneo yao kutoka China inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watu duniani.

# M/kiti wa CCM aiagiza serikali kuchunguza mauaji Mto wa Mbu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, Loata Sanare, ameigiza serikali Wilaya ya Monduli kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo cha matukio ya ubakaji na mauaji ya wanawake katika eneo la Mto wa Mbu yanayotokea mara kwa mara.

Tangu kuanza kwa vitendo vya wanawake kubakwa na kuuawa katika eneo la Mto wa Mbu, wanawake 10 wameshapoteza maisha licha ya polisi kuunda vikundi vya polisi jamii katika eneo hilo. Sanare alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya hiyo, kilichoshirikisha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Monduli, Steven Ulaya, wakuu wa idara na maofisa watendaji wa kata, wenyeviti wa CCM kata, ambapo alisema ni lazima uchunguzi wa kina wa mauaji hayo ufanyike, ili kuondoa taharuki hiyo na wanawake kuishi kwa hofu kubwa.

"Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Iddy Kimanta, nikuombe licha ya uchunguzi ambao unafanyika kila mwanamke anapouawa, sasa ufanyike uchunguzi wa kina kwa ajili ya kujua kiini cha mauaji haya, ambayo sasa yamekuwa tishio kwa wanawake wa Mto wa Mbu na wananchi kwa ujumla," alisema.

Awali Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa CCM (UWT) Mkoa wa Arusha, Yasmin Bachu, alisema akiwa kwenye ziara yake ya kikazi Kata ya Mto wa Mbu, siku chache zilizopita, wanawake waliomba CCM iwasaidie ili kuondoa changamoto ya wanawake kuuawa, hali inayowasababisha kushindwa hata kwenda shambani kwa ajili ya shughuli za uzalishaji.

"Mheshimiwa mwenyekiti wa CCM mkoa wa Arusha, kwa niaba ya wanawake wa Mto wa Mbu, nakuomba utusaidie kuiomba serikali ihakikishe ubakaji na mauaji ya wanawake wanatokomeza," alisema.

Baada ya maelezo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Kimanta alikiri vitendo vya wanawake kubakwa kisha kuuawa katika Kata ya Mto wa Mbu.

"Ni kweli mpaka sasa wanawake 10 wameshapoteza maisha kwa kubakwa kisha kuuawa na watu wasiojulikana na hivi karibuni mwanamke mmoja amebakwa na kuuawa na kwamba watu saba wanashikiliwa na polisi kwa ajili ya mahojiano," alisema.

Kimanta alimuahidi Mwenyekiti Sanare kuwa ofisi yake kwa kushirikiana na vyombo vya dola itaendelea kufanya uchunguzi juu ya matukio na watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alisema changamoto kubwa inayowakabili ni wananchi kutokuwa tayari kutoa ushirikiano wa kutoa taarifa sahihi za watuhumiwa wa uhalifu huo.

Aidha aliwataka wenyeviti wa vitongoji kuwa na orodha ya majina sahihi ya wananchi wanaoshi katika maeneo yao, kwa sababu kwa sasa kuna wimbi kubwa la wananchi wageni wanaoishi eneo hilo bila uwapo wa taarifa zao sahihi.

"Wenyeviti wa vitongoji kuanzia sasa naomba muwe na orodha sahihi ya majina ya wananchi katika maeneo yenu, kwa sababu kuna idadi kubwa ya watu ambao hawatambuliwi na ninyi viongozi na wanaishi kwenye chumba kimoja zaidi ya watu kumi wake kwa waume," alisisitiza.



Mvua zinazoendelea kunyesha maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Arusha, zimevunja daraja katika korongo la Oljoro Kata ya Oljoro, Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru. Kuvunjika kwa daraja hilo kumekata mawasiliano kati ya Kijiji cha Mbuyuni na kijiji cha Mirongoine. **PICHA:ALLAN ISACK**

# Mwanamke aliyeibuka kidedea apewa 5

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI Mtendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Devotha Mdachi, amempongeza Elizabeth Mwakijila kuwa Mtanzania wa kwanza aliyeshinda na kukabidhiwa Tuzo ya Kimataifa ya utalii nchini Uswisi hivi karibuni.

Akitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki wakati akimkabidhi cheti maalum kilichotolewa na Chama cha Utalii cha Wanawake (AWOTTA), Mdachi alisema amekuwa jasiri kusimama na kuitangaza Tanzania na vivutio vyake.

Alisema tuzo hiyo itasaidia kuongeza idadi ya watalii kuja nchini na kuongeza pato la taifa na kuinua uchumi wa nchi.

"Sisi tunakupongeza sana, umekuwa mwanamke jasiri na umepeperusha vema bendera uliokabidhiwa wiki mbili zilizopita na ukarudi na tuzo yako," alisema.

Aidha, alisema pia TTB inampongeza mwanamke huyo kwa ujasiri aliouonyesha na uzalendo wa kutangaza vivutio vilivyopo nchini na kushinda tuzo.

Naye Elizabeth Mwakijila, alisema alitumia vema nafasi hiyo kuitangaza Tanzania kwa kuonyesha vivutio vilivyopo na kuwabadilisha wazungu wengi ambao walikuwa wakiamini baadhi ya vivutio vipo Kenya kama Mlima Kilimanjaro.

"Mimi kupitia filamu yangu niliyotengenza niliweza kuwabadilisha na kuwaaminisha Mlima huu upo Tanzania na wengi wamefurahi na wameahidi kuja nchini kutembelea," alisema.

Aliwataka vijana na kila Mtanzania kwa nafasi yake kutangaza vivutio vilivyopo na kuacha kutegemea serikali pekee kufanya hivyo.

# Veta yaanza kuwanoa vijana masuala ya utalii

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHUO cha Hotel na Utalii cha Veta Njiro, mkoani Arusha, kimeanza kujiandaa na ushindani katika soko la ajira duniani na kusaidia nchi kufikia uchumi wa viwanda kwenye sekta ya utalii, kwa kuanzisha kozi ya utalii.

Kozi hiyo unahusu waongoza utalii, wasimamizi na waendesha utalii katika ngazi za Stashahada na Cheti.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa kozi hizo, Mkuu wa Chuo cha Veta Njiro, Christopher Ayo, alisema chuo hicho kilianza mwaka 2010 na walikuwa wakiendeleza taaluma za hoteli tu, ila baada ya kuona uhitaji mkubwa wa vijana kwenye shughuli za utalii walianza mchakato wa kuandaa mitaala.

"Kwa miaka mitatu tulikuwa tunaandaa mitaala sasa umeshaiva na tumezindua kozi hii ili vijana wetu wapikwe vizuri kwenye nyanja hii ya utalii na waweze kushindana na vijana wa Kenya na nchi zingine duniani ambao wanasifiwa," alisema.

Alisema kozi hiyo ni moja ya matunda ya ufadhili wa Canada ambao licha ya kuwafadhili vifaa vya kufundishia na kuwapika walimu, pia wanasaidia katika kozi hizo mpya.

Aidha, alisema mikoa ya utalii kama Arusha na mingine itanufaika zaidi kwa kupata vijana walioiva katika kuhudumia wageni na kuitangaza Tanzania ipasavyo.

"Kozi hizi zitatuletea mapato zaidi kwenye nyanja ya utalii na tutanufaika sana kufundishia vijana wetu... kozi hizi ambazo zitawaongezea ujuzi na kuvutia watalii kuja nchini tofauti na sasa wanafanya kwa mazoea," alisema.

Aidha, alisema vijana waliopo sokoni wengi wanashindwa kuhudumia wageni vizuri na kusababisha Kenya kuzoa sifa hizo ambazo hata Tanzania wanaweza kuzipata pindi watakapowapika vema.

"Hii inatokana na vijana wetu kukosa elimu ya darasani, lakini sasa watakapopata naamini wageni watahudumiwa ipasavyo na kuitanganza nchi yetu kila kona ya dunia," alisema

Aliongeza kuwa kwa kuanzisha kozi hizo, kunaifanya Tanzania kuwa na vyuo viwili vinavyotoa kozi ya Astashahda na cheti katika masuala ya utalii ambavyo ni Veta Njiro na Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kutoka Wizara ya Sayansi na Teknolojia, Dk. Noel Mbonde, alisema lengo la kazi yake ni kuhakikisha wanapata kozi mpya za umahiri nchini ili kuleta mapinduzi kwenye sekta ya utalii.





# Kambi maalum kuchunguza wenye magonjwa

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

MAOFISA uuguzi wa Mkoa wa Kilimanjaro wameweka kambi maalum ya uchunguzi wa shinikizo la damu, kifua kikuu na saratani ya matiti katika Wilaya ya Mwanga ili kuwasaidia wananchi wa vijiji vya pembezoni ambao hawawezi kufikiwa na huduma hiyo.

Muuguzi Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Gaudensia Olomi, alisema uchunguzi huo unafanyika bure katika uwanja wa Waziri Mkuu mstaafu wa serikali ya awamu ya kwanza, Cleopa Msuya.

Alisema wananchi wengi wanaotoka katika maeneo ya pembezoni wamekuwa wakishindwa kufikia huduma hizo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo gharama za uchunguzi na matibabu.

"Tunafanya haya kumuenzi muasisi wa huduma za uuguzi duniani, Florence Nightngale, ambaye alizaliwa mwaka 1820 huko Italia na kufariki mwaka 1910. Muasisi huyo alifanya kazi ya kutoa huduma kwa jamii, hususani waathirika wa vita vya kwanza vya Dunia.

"Na Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga imepata fursa ya kuwa mwenyeji kimkoa katika kuadhimisha siku ya wauguzi duniani kutoa huduma ya afya bure katika shule za msingi na sekondari."

Olomi alisema huduma ambazo zinatolewa katika uwanja wa mpira wa C.D Msuya ni uchangiaji damu salama, kupima na kutoa elimu kuhusu maambukizi ya VVU na kutoa elimu na chanjo ya kuzuia maambukizi ya saratani ya mlango wa kizazi (HPV).

Magonjwa mengine ni uchunguzi wa kifua kikuu, kupima sukari, kupima shinikizo la damu, kupima uzito na urefu, kuchunguza saratani ya matiti pamoja na kutoa elimu ya uzazi.



Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Juma Tukosa, akipiga makofi baada ya kuzindua rasmi bweni la wanafunzi wa kike 80 wanaotoka katika mazingira magumu wanaosoma Kiwoce Open School. **PICHA: GODFREY MUSH**

# Vikwazo wazalishaji sekta ya maziwa vyaondolewa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

OFISA Mwandamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Maendeleo ya Sekta Binafsi na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi anayeshughulikia mazingira ya biashara, Christopher Mramba, amesema serikali imeondoa vikwazo na urasimu usio wa lazima kwa wasindikaji na wazalishaji wa sekta ya maziwa.

Akizungumza na wasindikaji wa maziwa mkoani Kilimanjaro, wakati wa warsha ya siku mbili ya uhamasishaji unywaji wa maziwa yaliyosindikwa, ofisa huyo aliwaeleza kuwa serikali ina nia njema ya kusimamia sekta hiyo kutokana na udhibiti usioridhisha wa biashara.

Mramba alisema: "Serikali inataka mzalishe vizuri na mfanye biashara vizuri bila vikwazo, bila urasimu usio wa lazima. Kwa wale ambao mmezoea kusikia neno urasimu pengine ni neno ambalo sio baya, isipokuwa wanataka kukulazimisha ufuate taratibu hizi na hizi," alisema na kuongeza: "RC Mghwira (Mkuu wa mkoa) kawaambia watu wa TBS (Shirika la Viwango Tanzania) acheni urasimu, acheni watu wazalishe na kazi yenu ni kuwahudumia wazalishaji na wafanyabiashara kwa ufanisi. Ni udhibiti wa biashara ambao unamuwezesha yule anayefanya biashara kufanya biashara vizuri zaidi na hilo ndio lengo la serikali."

Katika warsha hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alizindua rasmi Jukwaa la Maziwa la mkoa huo.

Aidha, serikali imeeleza kuwa nia yake ya kusimamia na kutengeneza mazingira mazuri ya kufanya biashara na usindikaji wa maziwa ni pamoja na kutatua kero ambazo wazalishaji wanakutana nazo hasa wasindikaji na wazalishaji wa maziwa.

Mramba ameeleza zaidi kuwa mpango huo unatokana na udhibiti usioridhisha wa biashara.

"Udhibiti hauna maana ya kuzuia biashara isifanyike, udhibiti hauna maana ya kuzuia uzalishaji usifanyike, una lengo la kuhakikisha uzalishaji, biashara zinafanyika kwa kufuata kanuni ambazo ni rahisi kuzifuata, hazina muingiliano wa majukumu," alisisitiza.

Pamoja na mambo mengine, wasindikaji na wazalishaji wa maziwa walipata elimu kuhusu jitihada wezeshi kwa wafugaji, fursa za upatikanaji wa mitaji kwa wafugaji na vikundi vya vijana na wanawake, viwango vya ubora wa bidhaa za maziwa na usimamizi wa afya na usalama wa mlaji wa bidhaa za maziwa.

# TEWW yawaondoa hofu mfumo wa elimu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUFUNZI Mkazi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), Amina Mbughi, amewaondoa fikra hasi wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kuhusu tofauti ya mfumo rasmi wa elimu ya sekondari na mfumo usio rasmi, akisema mfumo usio rasmi unatolewa nchini ili kuondoa vipingamizi vinavyopatikana katika mfumo rasmi wa elimu.

Alitoa ufafanuzi huo jana wakati akizungumza katika halfa ya ufunguzi wa jengo jipya la hosteli ya wasichana ya Kiwoce Open School, iliyopo katika Kijiji cha Msasani, Moshi Vijijini, yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80.

"Kazi yangu mimi na Ofisa Elimu Sekondari haiwezi kutenganishwa. Nieleze tofauti iliyopo ni kwamba elimu ya mfumo usio rasmi inatolewa kwa kuondoa vipingamizi vinavyopatikana katika mfumo rasmi," alisema Mbughi.

Alisema elimu katika mfumo usio rasmi ni sawa na elimu iliyo katika mfumo rasmi ambayo Mkoa wa Kilimanjaro una vituo zaidi ya 30.

Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Juma Tukosa, akizungumza na wanafunzi, wadau wa elimu na wazazi wa wanafunzi wanaosoma katika kituo hicho alisema serikali inatambua vituo vyote vinatoa mfumo usio rasmi ni sawa mfumo rasmi. Mkurugenzi wa Kiwoce Open School, Graceanna Lyimo, alisema licha ya kupata mafanikio katika sekta ya elimu, ndoto yake kubwa ni kuhakikisha kituo hicho kinakua kwa ajili ya vijana wanaotoka katika mazingira magumu.

"Ndoto yangu nyingine niliyonayo sasa hivi ni kwa wale ambao hawawezi kusoma na kuandika, lakini kwa vitendo wanaweza wakafanya. Mfano tuna wasichana wa kazi za ndani wanaochukuliwa kwenda kufanya kazi anaweza kupika na kufanya kila kitu, lakini hawezi kupata ajira. Hivyo ndoto yangu ni kuwainua vijana ambao hawawezi kusoma kitaaluma na wanaweza kufanya kwa vitendo," alisema.

Kwa mujibu wa Graceanna, awali ndoto yake ilianza mwaka 2007 alipoamua kubadili eneo kilipojengwa kituo hicho ambacho ilikuwa ni sehemu ya wanawake kukutana na kujifunza mambo mbalimbali ya kujiinua kiuchumi kama vile kilimo na biashara ndogo ndogo.

Awali, akisoma risala ya wanafunzi wa kituo hicho cha Kiwoce Open School, Angel Emmanuel, alisema katika kumjengea msichana mazingira rafiki ya kujifunzia ili aweze kufanikisha malengo yake.

Pia, ameeleza kuwa hali hiyo inatokana na changamoto zinazowakabili wasichana, shule yao inatilia mkazo uwezeshaji wanafunzi wenye mazingira magumu kwa vile bado jamii haijajielekeza kwa dhati kutatua changamoto hiyo.

Nipashe
Spotika
JUMATATU MEI 13, 2019



**KWA NINI BALLON D'OR NI MESSI SIO VAN DIJK** UK. 20



# PATASHIKA...

Beki wa kati wa at RB Leipzig, Ibrahima Konate (kulia), akimdhibiti mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski katika mechi ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga ambayo ilimalizika kwa sare tasa juzi. Kwa matokeo hayo sasa Bayern itasubiri mechi yao ya mwisho ya funga msimu, na kama ikishinda itakuwa imetwaa ubingwa huo kwa mara ya saba mfululizo. **PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE

HII ni mara ya kwanza katika historia ya michuano ya Ulaya, timu za Ligi Kuu England (EPL), zote nne kukutana zenyewe kwa zenyewe kwenye mechi ya fainali za michuano hiyo wakati huu Liverpool na Tottenham zikikutana Juni Mosi, mwaka huu jijini Madrid kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya huku Arsenal na Chelsea zikikutana fainali ya Europa League Mei 29, mwaka huu jijini Baku Azerbaijan.



# SABABU 3 KWA NINI BARCELONA IMTIMUE VALVERDE

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA hawapo kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kufungwa mabao 4-0 na Liverpool kwenye mchezo wa pili wa nusu fainali ya michuano hiyo.

Barcelona iliwafunga vijana hao wa kocha, Jurgen Klopp mabao 3-0 kwenye mchezo wa kwanza pale Camp Nou, kabla ya Liverpool kupindua matokeo kwa ushindi wa 4-0 kwenye dimba la Anfield.

Baada ya mchezo huo, Kocha wa Barcelona, Ernesto Valverde alisema kwamba Liverpool ilikuwa timu bora.

“Walikuwa bora na tunatakiwa kulikubali hilo. Matokeo yalikuwa ni 4-0 na ndio maana hatukuwa na cha kujitetea.”

Hata hivyo, mashabiki wa Barcelona hawakuwa na furaha na sasa ni wazi kwamba kocha huyo anapaswa kuondoka. Kwani Barcelona imemaliza msimu kama ilivyokuwa msimu uliopita walipotupwa nje na AS Roma.

Ingawa wametawala Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na wameshinda, bado wana wakati mgumu kwenye michuano ya Ulaya. Hapa tunaangalia sababu tatu kwa nini Ernesto Valverde anatakiwa kutimuliwa...

**1. Valverde hachukui maamuzi, anamtegemea Messi tu**

Akiwa anachukuliwa kama kocha mwenye msimamo, Valverde amekuwa akitabirika katika kila mchezo kwa uteuzi wake wa kikosi. Malcom mara chache mno amekuwa akipewa nafasi msimu huu na licha ya kuwapo kwa Arthur kwenye kikosi, alichagua kumtumia Arturo Vidal kwenye mchezo wa pili dhidi ya Liverpool.

Ingawa alikuwa akiwabadilisha wachezaji wa kikosi chake msimu huu, hakuwa tayari kujaribu wachezaji wengine.

Pia amekuwa akimtumia Messi kama ndiye kila kitu kwa timu, hata wakati ambao raia huyo wa Argentina anaposhindwa kuwa kwenye kiwango chake. Uwezo wa Malcom na Ousmane Dembele umekuwa mzuri, lakini aliamua zaidi kumchezesha Coutinho. Barcelona inahitaji kocha ambaye anaelewa falsafa na kuichezesha timu kwa uwiano.

**2. Kujiamini kupita kiasi**

Licha ya kumpoteza Neymar aliyejiunga na Paris Saint-Germain, miamba hao wa Catalunya bado ni moja ya timu yenye kikosi chenye uwiano mzuri zaidi barani Ulaya. Hata hivyo, kuridhika kwao kunawagharimu kwa miaka mingi sasa.

Waliichukulia Roma ‘kishikaji’ baada ya ushindi wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na kwenye mchezo wa pili ikawagharimu. Hii inatokea kwa mara ya pili chini ya Valverde na kwa hakika sasa anatakiwa kubadilika.

Barcelona ya Pep Guardiola au ile ya Luis Enrique ilikuwa imara na haikuwa ikifanya mzaha kwenye mchezo wowote. Walifunga mabao na kutawala mchezo wote, lakini kwa sasa hali iko tofauti kabisa.

Yalikuwa makosa makubwa kwenye mchezo wa marudiano dhidi ya Liverpool kocha hakuwa na njia mbadala kwa timu yake.

**3. Kushindwa kwa mbinu zake**

Alikuwa na nafasi ya kuonyesha mbinu zake katika nafasi nyingi, lakini alishindwa kufanya hivyo.

Ingawa amekuwa kwenye Ligi Kuu ya Hispania kwa muda mrefu, amekuwa na wakati mgumu kwenye Ligi ya Ulaya. Anakosa mbinu mbadala kwa timu yake kama ilivyotokea kweye mchezo wa pili dhidi ya Liverpool.

Alichagua kikosi kile kile, ingawa walishinda kwenye mchezo wa kwanza, Sergi Roberto alikuwa amezidiwa uwezo na Sadio Mane. Philippe Coutinho hakuwa kwenye kiwango kizuri kwenye mchezo wa kwanza, lakini akamuacha tena kwenye kikosi cha kwanza. Hana uwezo wa kufikiria mbadala wa timu hasa inapokuwa haipo kwenye kiwango kizuri.

Mara nyingi amekuwa akimtegemea zaidi Messi na anaposhikwa kama ilivyokuwa kwenye mchezo dhidi ya Liverpool, mambo yakawa tofauti kabisa kwamba na Valverde hapa mpango B. mbinu za Klopp zilionekana wazi kabisa na yeye Valverde alishindwa kabisa kuusoma mchezo huo.

## JE, WAJUA?

KIPIGO cha mabao 4-0 ilichokipata Barcelona dhidi ya Liverpool, ndicho kikubwa zaidi kuwahi kukipata dhidi ya timu za Ligi Kuu England katika michuano yote ya Ulaya iliyowahi kushiriki.

# MICHEZO



# KAGERA SUGAR INAVYOIDUWAZA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya tatu mfululizo sasa, Simba imeshindwa kupata tiba ya kuifunga Kagera Sugar ya mkoani Kagera. Hii ni baada ya Ijumaa Mei 9, mwaka huu, Simba kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Uhuru na kuweka rekodi ya kupoteza mara tatu mfululizo dhidi ya timu hiyo.

Mara ya mwisho Simba kuifunga Kagera Sugar ilikuwa ni Ligi Kuu ya msimu uliopita 2017/18, mechi iliyochezwa Januari 22 kwenye Uwanja wa Kaitaba na kushinda mabao 2-0.

Hata hivyo, kwa mujibu wa rekodi zetu ni kwamba, kwa misimu mitano sasa, timu hizo zimekuwa zikionyeshana ubabe kwa kugawana dozi. Ina maana zote zimekuwa na nguvu sawa.

Tangu Ligi Kuu wa msimu wa 2014/15 hadi sasa timu hizo zimecheza mechi 10, na kila moja imeshinda mechi tano na kupoteza tano. Pia timu zote zimeshinda nyumbani mara mbili, na kushinda ugenini mara tatu.

Zifuatazo ni rekodi za matokeo ya timu hizo kwa misimu mitano iliyopita hadi sasa...

**1. Kagera Sugar 1-0 Simba-2014/15 (U/Taifa)**

Ni mechi iliyochezwa Desemba 26, 2014, kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, ilishuhudiwa Mnyama akiangukia pua kwa kuchapwa bao 1-0, lililowekwa wavuni na straika wao tegemeo wakati huo, Atupele Green dakika ya 21 ya mchezo na kudumu kwa dakika zote 90.

**2. Simba 2-1 Kagera Sugar-1014/15 (Kaitaba)**

Simba ililipiza kisasi kwenye mechi ya marudiano Uwanja wa Kaitaba kwa kuifumua Kagera Sugar mabao 2-1. Mechi hiyo ilichezwa Aprili 6, 2015, ikiwa ni mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2014/15.

Yalikuwa ni mabao ya Ramadhani Singano ambaye kwa sasa yupo Azam na Ibrahim Ajibu anayekipiga Yanga kwa sasa, akifunga kwa mkwaju wa penalti, huku lile la wenyeji likifungwa na Rashid Mandawa anayecheza soka la kulipwa nchini Botswana kwa sasa.

**3. Simba 3-1 Kagera Sugar-2015/16 (U/Taifa)**

Msimu wa 2015/16 ulikuwa mzuri kwa Simba kwani ilishinda mechi zote za nyumbani na ugenini, ikianza kushinda mechi ya mzunguko wa kwanza Septemba 20, 2015 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kwa kuichapa Kagera Sugar mabao 3-1.

Shukrani kwa 'hat-trick' ya straika Mganda Hamsi Kiiza aliyekuwa amejiunga na timu hiyo akitokea Yanga, mabao ya dakika ya 31, 47 na 90, huku Mbaraka Yusuph akiifungia timu yake bao la kufutia machozi.

**4. Kagera Sugar 0-1 Simba-2015/16 (Kaitaba)**

Kagera Sugar ilishindwa kujibu kipigo kwenye mechi ya mzunguko wa pili, ilipokubali kulala kwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Kaitaba, Februari 7, 2016. Bao pekee kwa Simba na kwenye mechi hiyo, lilifungwa na kiungo mshambuliaji ambaye anaichezea Yanga kwa sasa, Ajibu dakika ya 45.

**5. Simba 2-0 Kagera Sugar-2016/17 (U/Uhuru)**

Ilikuwa ni Ligi Kuu msimu wa 2016/17, mechi ya kwanza ikichezwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam Oktoba 15, 2016 Simba ikishinda kwa mabao 2-0 kupitia kwa Mzamiru Yassin, huku Shiza Kichuya akifunga bao la pili kwa mkwaju ya penalti.

**6. Kagera Sugar 2-1 Simba-2016/17 (Kaitaba)**

Ilikuwa ni mzunguko wa pili wa Ligi Kuu msimu wa 2016/17, mechi ikichezwa Uwanja wa Kaitaba na Kagera Sugar kuinyuka Simba mabao 2-1, wafungaji wakiwa ni Mbaraka Yusuph na Edward Christopha, wote wakitokea kikosi cha pili cha Simba, bao la kufutia machozi la Simba likifungwa na Mzamiru Yassin.

**7. Kagera Sugar 0-2 Simba-2017/18 (Kaitaba)**

Kagera Sugar ilikumbana na kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Kaitaba mechi ya mzunguko wa kwanza Januari 22, 2018. Ilikuwa ni Ligi Kuu msimu wa 2017/18. Mabao ya Simba yalifungwa na Said Ndemla na John Bocco.

8. Simba 0-1 Kagera Sugar-2017/18 (U/Taifa)

Simba iliaibishwa mbele ya Rais Dk. John Magufuli, Mei 19, mwaka jana ikiwa ni mechi ya mzunguko wa pili. Ilikuwa ni mechi ya kukabidhiwa Kombe la ubingwa wa Ligi Kuu. Iliambulia kipigo cha bao 1-0 kwenye Uwanja wa Taifa, likiwekwa wavuni na Edward Christopha dakika ya 84.

**9. Kagera Sugar 2-1 Simba-2018/19 (Kaitaba)**

Kagera Sugar iliendelea kuisulubu Simba kwa mara ya pili mfululizo msimu huu wa 2018/19, ikianza kwa kuisasambua 2-1 Uwanja wa Kaitaba Aprili 20, mwaka huu, Kassim Hamisi na Ramadhani Kapera wakiifungia mabao hayo, huku la wageni wao, likifungwa na Emmanuel Okwi.

**10. Simba 0-1 Kagera Sugar-2018/19 (U/Uhuru)**

Hii ndiyo mechi ya mwisho iliyochezwa Ijumaa iliyopita Mei 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Kagera Sugar ikiipa Simba kipigo cha tatu mfululizo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, mechi ya mzunguko wa pili.

Beki wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala' alijifunga mwenyewe bao hilo katika harakati za kuokoa mpira, akichanganyana na kipa wake, Aishi Manula dakika ya 41.

## NJE YA UWANJA

# HAT-TRICK AJAX BADO YAMTOA CHOZI MOURA

Lucas Moura ameendela kumwaga machozi kila wakati anaporejea kuitazama mechi ya Tottenham dhidi ya Ajax wakati walipotokea nyuma na kupindua matokeo kwa kushinda 3-2.

Kikosi hicho cha Mauricio Pochettino Jumatano iliyopita kilikata tiketi ya kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kikiwa ugenini jijini Amsterdam – shukrani kwa Moura aliyefunga mabao matatu 'hat-trick' katika kipindi cha pili na kufanya matokeo ya jumla kuwa mabao 3-3 kufuatia mechi ya kwanza Spurs ikiwa nyumbani kulala 1-0, hivyo miamba hiyo ya London kunufaika na bao la ugenini.

Bao la ushindi lilikuwa la 'usiku' kufuatia kupatikana dakika za majeruhi ya 96, na Moura bado anapata hisia wakati anapotazama kipindi hicho kigumu.

"Nadhani kuwa ninaota," Lucas aliiambia tovuti ya Tottenham.

"Ilikuwa siku isiyotarajiwa. Ni mwenye furaha, mwenye fahari sana. Mara zote ninasema kwamba wakati unapoamini na unapofanya kwa bidii, unapokea mambo mazuri na kundi hili na timu hii inastahili hili.

"Niliamini kuwa ilikuwa inawezekana kushinda mechi na kwenda fainali, lakini sikuamini kwamba ningefunga mabao matatu na la tatu lilikuwa la dakika za mwisho. Ilikuwa kamili.

"Nilitazama tena mechi. Kila wakati ninapotazama video hiyo ninalia kwa sababu ina hisia sana. Kila mchezaji anataka kuwa na nyakati kama hii, kuishi katika nyakati kama hii, ni mwenye furaha sana na tunahitaji kufurahi."



NIPASHE JUMATATU MEI 13, 2019





# NYOTA WA5 WENYE 'HATI PUNGUZO' SOKONI

**LONDON, England**

GARETH Bale, David de Gea na Neymar wanaweza kuondoka wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Wakati dirisha la usajili likikaribia kufunguliwa, klabu za soka zimeanza kuingia kwenye shoo ya usajili.

Klabu kadhaa kubwa kama vile Real Madrid, Manchester United na Arsenal zimekuwa na wakati mgumu kwenye viwango vyao msimu huu na zitakuwa zikitaka kuimarisha vikosi vyao kwa ajili ya msimu ujao.

Tunatarajia kuona rekodi kadhaa zikivunjwa wakati huu wa usajili, hata hivyo kuna nyota wakubwa ambao bado hawapo vizuri na klabu zao za sasa na watakuwa na uwezekano wa kupunguzwa bei wakati wa dirisha la usajili.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao watalazimika kujadiliana kupunguzwa bei [wenye 'hati punguzo'] ili kuuzwa msimu ujao...

**5. Gareth Bale (Real Madrid)**

Real Madrid waliweka rekodi ya dunia ya pauni milioni 85 kumsajili Gareth Bale kutoka Tottenham Hotspur mwaka 2013. Hata hivyo, raia huyo wa Wales amekumbwa na majeraha na kuwa na kiwango kibovu hapo Bernabeu na hakuweza kufanya kile kisichotarajiwa kutoka kwake.

Amewachezea miamba hao wa La Liga mechi 29 msimu huu, na alichangia mabao nane na pasi za mwisho tatu. Alitarajiwa kuwa katikati ya majukumu ya kuongoza safu ya ushambuliaji pale Santiago Barnabeu baada ya kuondoka kwa Cristinao Ronaldo kwenda Juventus kipindi cha majira ya joto, lakini alishindwa kufikia malengo.

Kwa mujibu wa ripoti za hivi karibuni, kocha wa Los Blancos hao, Zinedine Zidane amemuambia mchezaji huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur kwamba hayupo kwenye mipango yake na anaweza kuondoka kipindi cha majira ya joto.

**4. Alexis Sanchez (Manchester United)**

Vitu vikubwa vilitarajiwa kutoka kwa Alexis Sanchez wakati alipojiunga nao akitokea Manchester United kutoka Arsenal wakati wa dirisha dogo la usajili mwaka 2018. Hata hivyo, mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile, amekuwa kwenye kiwango kibovu hapo Old Trafford na sasa anaonekana wazi kuwa hahitajiki na klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amecheza mechi 20 za Ligi Kuu msimu huu na amefunga bao moja na pasi za mwisho tatu kwa timu hiyo. Kwa sasa ndiye mchezaji anayelipwa zaidi katika klabu hiyo na mara kwa mara amekuwa akiachwa kwenye kikosi cha kwanza na kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Kikosi hicho cha 'Mashetani Wekundu' hao kinatarajiwa kuimarishwa zaidi kwa kuwauza baadhi ya wachezaji na Sanzhez anaweza akawa na 'hati punguzo' sokoni ili aondoke.

**3. Thibaut Courtois (Real Madrid)**

Thibaut Courtois ni nyota wa Kombe la Dunia mwaka jana nchini Urusi na alijiunga na Real Madrid akitokea Chelsea kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 35 wakati wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2018.

Hata hivyo, mambo hayakwenda kama yalivyopangwa pale kwenye dimba la Bernabeu na amekuwa kwenye wakati mgumu wa kuimarika kwa kiwango chake katika klabu hiyo. Amefungwa mabao 33 kwenye mechi 26 za Ligi Kuu alizowachezea Los Blancos hao msimu huu na hakuruhusu bao katika mechi nane tu.

Kuteuliwa kwa Zinedine Zidane kama kocha wa klabu hiyo ni wazi kwamba nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza ni ngumu. Zidane amebainisha wazi kabisa kwamba atamtumia zaidi Keylor Navas kama golikipa chaguo lake la kwanza.

Kocha huyo wa Real Madrid hivi karibuni alibainisha kwamba anaweza kumuuza golikipa mmoja wakati wa kipindi cha majira ya joto na ni wazi kwamba uwezekano wa Courtois kuuzwa hapo ni mkubwa.

**2. David de Gea (Manchester United)**

Mmoja wa magolikipa bora duniani kwa sasa, David de Gea, ameonyesha kiwango kizuri kwa Manchester United katika miaka ya hivi karibuni na ameshinda tuzo ya Sir Matt Busby kama mchezaji bora wa mwaka mara nne katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Golikipa huyo wa kimataifa wa Hispania amecheza mechi 274 za Ligi kwa Mashetani Wekundu hao na ameisaidia klabu hiyo kushinda taji la Ligi Kuu na moja la Ligi ya Europa pamoja na mataji ya FA na EFL.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ameonyesha wazi kwamba anataka kuondoka katika klabu hiyo.

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu ujao na Manchester watakuwa tayari kumwekea hati punguzo sokoni ili kumuuza badala ya kumuacha aondoke huru mwakani.

**1. Neymar (Paris Saint-Germain)**

Paris Saint-Germain walitumia kiasi cha pauni milioni 200 kwa ajili ya kumsajili Neymar kutoka Barcelona wakati wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2017, na kumfanya kuwa mchezaji ghali zaidi duniani wa wakati wote.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil amecheza mechi 36 za Ligi na kufunga mabao 33. Alitoa mchango mkubwa wakati PSG wakishinda mataji matatu msimu uliopita na alipewa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Ligue 1 msimu wa 2017-18 kwa kiwango bora.

Hata hivyo, mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara msimu huu na amecheza mechi 16 tu za ligi. Kwa sasa anachukua mshahara mkubwa ikilinganishwa na wachezaji wanzake na PSG, wanaweza kumuuza ili kupata fedha wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa ripoti za hivi karibuni, Real Madrid imeonyesha nia ya kutaka kumsajili na kuna uwezekano akaondoka katika klabu hiyo.



David de Gea

## NUKUU



"Natumai [nitakuwa fiti kwa wakati]. Matibabu yanakwenda vizuri hadi sasa. Nimeanza kukimbia moja kwa moja wiki hii [iliyopita]," **Harry Kane aliiambia BT Sport wakati akizungumzia uwezekano wa yeye kucheza mechi ya fainali Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool Juni Mosi, mwaka huu baada ya Tottenham kuitoa Ajax kwa faida ya bao la ugenini kufuatia matokeo ya jumla kuwa 3-3.**



"Kiwango kwa ujumla kilikuwa kikubwa mno. Katika maisha yangu nimetazama mechi nyingi za soka, lakini sikumbuki nyingi kama hii. Kushinda tayari ni vigumu, lakini kushinda bila kuruhusu bao ['clean sheet'] - Sijui ni kwa namna gani wavulana wamelifanya hili. Nilimuona James Milner akilia baada ya mechi uwanjani, inamaana sana kwa sisi sote," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp aliiambia BT Sport baada ya kikosi chake kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kuitoa Barcelona kwa tofauti ya mabao 4-3**



"Kulikuwa na kuchanganyikiwa kidogo [kwangu] leo kwa sababu kila mmoja alisema usipige. Ilinitia hasira- sikuwa mbali kwa wachezaji wengine kuniambia usipige. Kwa hiyo nilichukua hatua ya kupiga. Nilishafunga mabao kama hayo wakati wa mazoezi. Ni hadithi ya kushangaza kwa sababu ni miaka 15 katika kiwango cha juu cha kuwa na viungo kuniambia usipige. Kwa miaka 15 nilisema usihofu, siku moja nitapiga na kufunga bao kali," **Vincent Kompany akizungumzia bao la mkwaju wa mbali alilofunga na kuipa Manchester City ushindi wa 1-0 dhidi Leicester City kabla ya mchezo wao wa funga msimu dhidi ya Brighton and Hove Albion jana.**

## Michezo




Kutoka kulia ni mastraika wa Simba, Meddie Kagere na Emmanuel Okwi, kila mmoja akiwa na mpira wake baada ya kufunga hat-trick kwenye mechi dhidi ya Coastal Union Jumatano iliyopita: Kulia ni kocha wa timu hiyo, Patrick Aussems. **PICHA: MAKTABA**

# MAPRO WANAVYOTESA LIGI KUU KWA HAT-TRICK

**Na Mwandishi Wetu**

MASTRAIKA wa Simba, Emmanuel Okwi na Meddie Kagere, Jumatano iliyopita walifunga mabao matatu 'hat-trick', kila mmoja kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union kutoka Tanga.

Katika mchezo huo uliofanyika kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, mastraika hao tegemeo wa klabu hiyo kubwa nchini walifunga mabao hayo wakiisaidia timu yao kushinda 8-1.

Hiyo inakuwa ni hat-trick ya tano sasa kwenye Ligi Kuu msimu huu, huku Okwi akiongoza kwa kufunga hat-trick mbili, lakini pia wachezaji watatu wakiwa ni wa kigeni.

Na katika hat-trick hizo ni mchezaji Mtanzania mmoja tu ndiye ameonekana kujitutumua mpaka sasa. Wafuatao ni mastraika waliofunga hat-trick kwenye Ligi Kuu mpaka sasa msimu huu.

**1. Emmanuel Okwi-Simba**

Huyu ni straika mwandamizi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, msimu huu amepiga hat-trick mbili mpaka sasa. Okwi ni raia wa Uganda ambaye kwa muda mrefu amekuwa akicheza Ligi ya Tanzania.

Ya kwanza ilikuwa ni Oktoba 28, mwaka jana katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu dhidi ya Ruvu Shooting. kwenye mechi hiyo Simba ilishinda mabao 5-0.

Okwi alifunga mabao yake dakika ya nane, 53 na 77, huku mengine yakifungwa na Kagere na Adam Salamba.

Jumatano iliyopita alifunga ya pili msimu huu kwenye mechi dhidi ya Coastal ikifa mabao 8-1.

Alifanya hivyo dakika ya 10, 19 na 46, huku mabao mengine matatu yakifungwa na Kagere, Hassan Dilunga na Clatous Chama.

"Nawapongeza wachezaji wenzangu kwa sababu tumecheza mechi nyingi sana kwa muda mfupi na tumekuwa na muda mfupi wa kupumzika, lakini tunamshukuru Mungu tumekuwa tukipata matokeo mazuri. Lakini pia nashukuru kwa kuweza kuisaidia timu yangu kupata ushindi," alisema mara baada ya mechi dhidi ya Coastal kumalizika.

Kuhusu kurejea tena kwenye kiwango chake kwa siku za karibuni, huku akifunga mabao karibuni kila mechi, Okwi alisema kuwa alisaidiwa zaidi na wachezaji wenzake.

"Siri ni kutokata tamaa na pia kuwa na ushirikiano mzuri na wachezaji wenzangu kwa sababu unapokuwa haupo sawa, halafu wachezaji wenzako wanakupa ushauri, wanakuhamasisha, wanakusaidia uwanjani, tunasaidiana, tunapambana na hakuna kukata tamaa," alisema.

**2. Meddie Kagere-Simba**

Ni msimu wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu ya Tanzania akitokea nchini Kenya kwenye Klabu ya Gor Mahia.

Kagere alifunga hat-trick yake ya kwanza akiwa kwenye ardhi ya Tanzania Jumatano iliyopita Simba ilipoichakaza Coastal Union mabao 8-1.

Alifanya hivyo dakika ya 69, 74 na 82 na kuweka rekodi yake kwenye Ligi Kuu ya Tanzania, mabao mengine yakifungwa na Okwi aliyefunga matatu, Dilunga na Chama.

Mara baada ya mechi hiyo alisema wamekuwa wakishinda kutokana na kucheza kwa ushirikiano, kwani bila hivyo ingekuwa kazi bure.

"Wachezaji tumekuwa tukipendana na hii hata mimi imenisaidia kufikisha mabao haya, kupata hat-trick na timu kupata ushindi," alisema.

Kuhusu ufungaji bora alisema kuwa atajitahidi kufunga kuangalia mwisho wa Ligi Kuu hali itakuwaje.

**3. Alex Kitenge-Stand United**

Alex Kitenge ni raia wa Burundi, akikamilisha idadi ya wachezaji watatu wa kigeni waliofunga mabao matatu kwenye mechi moja Ligi Kuu ya Tanzania Bara.

Straika huyo wa Stand United, alifanya hivyo Septemba 16, mwaka jana kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu wakati timu yake ikicheza dhidi ya Yanga katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Hat-trick yake ilikuwa dakika ya 14, 58 na 90 timu yake ilipocheza dhidi ya Yanga, lakini kwa bahati mbaya sana pamoja na kufunga mabao matatu, timu yake ilifungwa 4-3.

Mabao ya Yanga yalifungwa na Mrisho Ngassa, Ibrahim Ajibu, Andrew Vicent na Deus Kaseke.

**4. Salum Aiyee-Mwadui**

Salum Aiyee ndiye Mtanzania pekee kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kufunga mabao matatu kwenye mechi moja 'hat-trick'.

Ilikuwa ni Januari 6, mwaka huu wakati alianza kutupia katika dakika ya 48, 68 na kisha kukamilisha hat-trick yake dakika ya 83 kwenye mechi ambayo timu yake ya Mwadui ilicheza dhidi ya Kagera Sugar.


Mechi hiyo ilichezwa kwenye Uwanja wa Mwadui Complex mjini Shinyanga.

## NAJUA WAJUA

**Liverpool imecheza mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tisa, ni Real Madrid pekee (mara 16), Milan (mara 11) na Bayern Munich (mara 10) zilizocheza fainali mara nyingi kuishinda katika historia ya michuano hiyo.**



## AFRIKA



# WAKALI
## WA3 UNITED ITAKAOWAPOTEZA

Paul Pogba

**MANCHESTER, England**

NI miezi minne tangu Ole Gunnar Solskjaer amechukua mikoba ya ukocha Klabu ya Manchester United. Hata hivyo, Ole amekua na rekodi bora.

Hivyo kwa sasa, Ole ni kocha mkubwa. Akiwa na rekodi nzuri kwenye mwanzo wake hapo United akapewa rasmi mikoba ya kuinoa timu hiyo kama kocha wa kudumu. Ana historia na klabu hiyo, alicheza chini ya zama za Ferguson, na alikuwa katika himaya nzuri kwenye kikosi hicho.

Licha ya Scott McTominay kufunga bao la ufunguzi dakika ya 8 kwenye mchezo uliopita dhidi ya Huddersfield, mchezo huo ulimalizika kwa sare. Man United ilipata pointi tano tu katika mechi tano zilizopita za Ligi Kuu na matokeo yake dhidi ya Huddersfield yakaifanya ishindwe kufuzu kwa michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Huku Manchester United ikiwa ni moja ya klabu yenye mafanikio makubwa zaidi kwenye historia ya Ligi Kuu ya England, imekosa nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. Hiyo ina maana kwamba kwa mara ya pili mfululizo United imeshindwa kufuzu kwenye michuano hiyo mikubwa Ulaya.

Bahati mbaya kwa mashabiki ni kwamba, mambo yanaonekana kuwa magumu kwa upande wao. Kama ni kweli kwa yale yanayoandikwa na magazeti basi ni wazi kwamba, United itakuwa kwenye wakati mgumu.

Kuijenga timu ni kitu kigumu, na imewachukua Liverpool na Tottenham kuwa kwenye wakati mgumu wakati wakilitimiza hilo. Kwani sasa ni wazi kwamba kuna wachezaji muhimu kwa kikosi hicho wanaweza kuondoka mwishoni mwa msimu.

Makala haya yanakuchambulia wachezaji watatu muhimu wa kikosi hicho ambao wanaweza kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu...

**3. Ander Herrera**

Amekuwa na mchango mkubwa kwa kikosi hicho msimu huu na ni wazi kwamba, Ander Herrera atakosekana katika kikosi cha United kwenye nafasi ya kiungo.

Bahati mbaya kwa mashabiki wa United, hii inaonekana kama vile tayari usajili wake umekamilika. Akiwa mwishoni mwa msimu wake wa sasa, ni wazi kwamba Herrera anakwenda kujiunga na PSG kipindi cha majira ya joto. Kwa mujibu wa ripoti za hivi karibuni, kama ambavyo Gazeti la AS lilivyoripoti, Herrera amekubali kusaini mkataba wa miaka mitatu na mabingwa hao wa Ufaransa.

Inaonekana kama Herrera anakwenda kuziba pengo la Rabiot ambaye anaondoka akiwa mchezaji huru wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Mchezaji imara na mwenye kipaji Rabiot anaonekana anahitajika zaidi na Man United kwa ajili ya kuziba pengo la Herrera, lakini United itakumbana na ushindani mkubwa kutoka kwa klabu kama Tottenham, Arsenal na Liverpool. Juventus pia ni klabu nyingine inayomuwania Mfaransa huyo.

**2. David De Gea**

Pengine huu unaweza kuwa si msimu mzuri zaidi kwa David De Gea, ikumbukwe kwamba yeye ndiye mchezaji pekee wa Manchester United aliyeshinda tuzo ya Sir Matt Busby kama mchezaji bora wa mwaka mara nne (mwaka 2014, 2015, 2016 na 2018).

Kwa mujibu wa vyanzo vingi, De Gea hayupo tayari kusaini mkataba mpya na anaona kwamba anastahili kulipwa mshahara mkubwa zaidi kama anaopewa Alexis Sanchez wa pauni 500,000 kwa wiki.

Kiuhalisia De Gea hakuwa tayari kusaini mkataba mpya na hivyo kwa vyovyote United watalazimika kumuuza ili wasimkose mwakani. PSG na Real Madrid ni klabu mbili ambazo zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili golikipa huyo wa kimataifa wa Hispania.

Kiukweli, kumpoteza mtu kama De Gea itakuwa ni sawa na kupoteza uti wa mgongo wa timu.

**1. Paul Pogba**

Mchezaji pekee ambaye timu yake haipo kwenye nne bora kuwapo kwenye kikosi bora cha mwaka cha Ligi Kuu ya England na hivyo ni wazi kwamba, Paul Pogba ni nguzo muhimu kwa kikosi hicho. Amefunga mabao 13 na kutoa pasi za mwisho tisa msimu huu.

Hakuna shaka kwamba ni mmoja wa viungo wenye vipaji vya ukweli duniani. Hata hivyo, kiwango chake kimekuwa cha kupanda na kushuka msimu huu.

Baadhi ya mashabiki wa United wasingependa kusikia kuhusu kuondoka kwa mchezaji huyo. Kwa mujibu wa Gazeti la The Daily Star, kocha Zinedine Zidane amebainisha kwamba anataka kumsajili mchezaji huyo ili kuimarisha kikosi chake.

Kwa sasa amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake, lakini mshahara wa Pogba ni kikwazo kikubwa.

United wanaweza kupata kiasi cha euro milioni 90 kama wakimuuza Mfaransa huyo.

**NDANI YA 18**

Georginio Wijnaldum ni mchezaji wa kwanza Liverpool kucheka na nyavu mara mbili kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akitokea benchi tangu Ryan Babel alipotupia kwa idadi hiyo dhidi ya Besiktas mwaka 2007. Kadhalika, ni mchezaji wa kwanza kufunga mabao mawili dhidi ya Barcelona akitokea benchi kwenye michuano hiyo.



GARETH Bale, David de Gea na Neymar wanaweza kuondoka wakati wa kipindi cha majira ya joto. Wakati dirisha la usajili likikaribia kufunguliwa, klabu za soka zimeanza kuingia kwenye shoo ya usajili.
**Uk.16-17**




# KWA NINI BALLON D'OR NI MESSI SIO VAN DIJK

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imetolewa na Liverpool kwenye nusu fainali ya pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Katika mchezo wa kwanza ilishinda 3-0 na mambo yakabadilika kwenye mchezo wa pili na wakafungwa 4-0 kwenye dimba la Anfield. Divock Origi na Georgino Wijnaldum kila mmoja alifunga mabao mawili wakati kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kikipindua matokeo pale Anfield na kuwatupa nje mabingwa hao wa Hispania.

Kwenye mchezo wa kwanza Lionel Messi alikuwa ndiye shujaa, ambapo alifunga mabao mawili, na raia huyo wa Argentina akajikuta akizuiwa na Virgil van Dijk kwenye mchezo wa pili.

Kikosi hicho cha kocha Ernesto Valverde kilionekana kuwa kwenye wakati mgumu zaidi katika mchezo huo wa pili na hivyo kujikuta wakitolewa kwa aibu kubwa. Msimu huu ulionekana kama Barcelona wangeshinda mataji matatu na hivyo kuwa na nafasi ya wazi kabisa kwa Messi kubeba Ballon d'Or ya sita.

Ingawa Barcelona wametolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, tayari imeshashinda taji la Ligi Kuu na ipo kwenye fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'] ambapo watacheza dhidi ya Valencia.

Pamoja na yote bado Messi anaweza kushinda Ballon d'Or ya sita kwa sababu ya kuwa kwenye kiwango bora zaidi msimu huu. Hapa tunakuchambulia sababu tatu kwa nini Messi bado anaweza kushinda tuzo ya Ballon d'Or msimu huu...

**3. Rekodi binafsi ya ufungaji**

Kusema kwamba Messi ameachwa na washambuliaji wa England kwenye ufungaji wa mabao Ulaya msimu huu, hii ni kutomtendea haki. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina amefunga jumla ya mabao 48 katika mechi 46 za mashindano yote kwa Barcelona msimu huu. Kwa sasa anaongoza kwenye orodha ya ufungaji wa mabao kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, lakini pia anaongoza kwa kufunga mabao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kufungiwa kwa Kylian Mbappe kwa mechi tatu za Ligi Kuu inamaana kwamba ni wazi kabisa Messi atashinda tuzo yake ya sita ya Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora kwa Ligi tano kubwa za Ulaya.

Messi si tu kwamba anaongoza kwa uwezo binafsi, lakini pia kiwango chake cha kucheka na nyavu msimu huu kimekuwa cha kuvutia zaidi. Mabao yake mawili dhidi ya Manchester United kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya yaliwafanya 'Mashetani Wekundu' hao kutupwa nje.

**2. Kiwango cha Ronaldo**

Tuzo ya Ballon d'Or kwa kipindi cha miaka 10 ilikuwa ikishindaniwa kati ya Cristiano Ronaldo na Messi hadi Luka Modric alipoinyakua msimu uliopita. Ronaldo hajawa na msimu mzuri zaidi wa kupachika mabao kwenye msimu wake wa kwanza na miamba wa Italia, Juventus, ambao walitolewa kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya vijana Ajax.

Hii ilikuwa ni mara ya kwanza tangu msimu wa 2009-10 kwamba Ronaldo kutocheza kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mfungaji huyo mwenye rekodi ya aina yake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya alifunga mabao sita tu kwenye mashindano hayo, ikiwa ni nusu ya yale ya Messi akiwa amefunga mabao 12.

Ronaldo kwa sasa anashika nafasi ya tatu kwa ufungaji bora kwenye Ligi Kuu ya Italia, Seria A, nyuma ya nyota wa Sampdoria, Fabio Quagliarella na Duvan Zapata wa Atalanta. Licha ya kwamba Juventus walishinda taji lao la nane mfululizo la Serie A, walitolewa kwenye Coppa Italia na Atalanta. Licha ya kufunga kwenye mechi zote mbili za robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Ajax, Ronaldo hakuweza kuwazuia vijana hao wa Uholanzi kusonga mbele.

Huku Ronaldo akiwa ameshinda mara tano Ballon d'Or, hivyo Messi ana nafasi kubwa ya kuibeba kwa mara ya sita.

**1. Kutokuwa na mashindano makubwa**

Tukubaliane hili. Linapokuja suala la viwango binafsi, Messi amekuwa hana mpinzani msimu huu. Akiwa amechaguliwa kuwa nyota bora wa mchezo mara 22, amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi hapo kwa miamba Barcelona na kuiwezesha kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Licha ya kwamba, Virgil van Dijk ameshinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka kwenye Ligi Kuu ya England, lakini linapokuja suala la kiwango binafsi, Messi yupo juu zaidi.

Licha ya kwamba, raia huyo wa Uholanzi amekuwa kwenye kiwango kizuri cha kuwabeba vijana hao wa kocha, Jurgen Klopp bado nafasi yake ni ndogo kuweza kumpiku Messi.

Huku Manchester City kabla ya mechi za funga msimu jana ikionekana wazi kwamba ilikuwa na nafasi kubwa ya kushinda taji la Ligi Kuu, na nafasi ya mabeki kushinda tuzo hiyo kuwa ni nadra tangu Fabio Cannovara aliyeisaidia Italia kutwaa Kombe la Dunia mwaka 2006, ni wazi kwamba Messi ana nafasi kubwa ya kumshinda Van Dijk na kutwaa tuzo hiyo.

## USILO LIJUA



WAKATI Arsenal na Chelsea zikitarajiwa kukutana fainali ya Europa League Mei 29, mwaka huu jijini Baku, Azerbaijan, itakuwa ni mara ya kwanza katika historia ya michuano hiyo timu za England kukutana fainali tangu mwaka 1972 Wolverhampton Wanderers ilipokutana na Tottenham. Katika fainali hiyo Spurs ilishinda 3-2



# DC awapongeza wanawake kuanzisha gulio

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, amewapongeza wanawake wa Jiji la Mbeya kwa ushirikiano wanaouonyesha kwa kuungana katika vikundi na kunufaika na mikopo inayotolewa na halmashauri.

Ntinika alitoa pongezi hizo wakati wa uzinduzi wa Gulio la Biashara lililopo ndani ya Soko la Kimataifa la Mwanjelwa jijini hapa na wanawake wa jiji hilo kuonyesha ushirikiano kwenye uanzishaji wa gulio hilo.

Aliwataka waendelee na ushirikiano huo ikiwa ni pamoja na kuendelea kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali ili wanufaike na asilimia nne ya mapato ya halmashauri ambayo yanatengwa kwa ajili ya vikundi vya vijana.

"Mmeonyesha ushirikiano mkubwa sana kwenye shughuli hii hivyo nawaomba muendelee na ushirikiano huo ili muweze kukuza vipato vyenu hasa mkiwa katika vikundi, halmashauri inatenga zaidi ya milioni 900 kwa ajili yenu, vijana na walemavu," alisema Ntinika.

Alisisitiza kuwa wanawake hao watafanikiwa zaidi wakiwa kwenye vikundi na kwamba kwa sasa serikali ya awamu ya tano inalenga kuhakikisha inafikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Sara Ndambo ambaye ni mwanzilishi wa gulio hilo la Mwanamke Shujaa, alisema lengo la kuanzisha gulio hilo ni kuwainua wanawake kiuchumi ili waweze kukuza vipato vyao na kujitegemea.

Aliwaomba wanawake kuendelea kujitokeza kwenye gulio hilo ili wafikie malengo yao kwa kujifunza fursa mbalimbali za maendeleo zilizopo katika mkoa huo.



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Mbeya, Vincent Msolla (kulia), akikata utepe kuashiria kuzinduliwa rasmi kwa mafunzo ya vitendo kwa vijana wa Mradi wa Youth Building unaoendeshwa na Taasisi ya Catholic Releaf Service (CRS) jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Baba adaiwa kumuua mwanawe kwa dau la mil. 5/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu wawili akiwamo mmiliki wa Shule ya Sekondari ya Ushindi iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani humo kwa tuhuma za mauaji ya mtoto, Rose Japhet (6), tukio linalohusishwa na imani za kishirikina.

Wanaoshikiliwa ni Andrew Mwambuluma, mkazi wa Mbalizi ambaye pia ni mmiliki wa Shule ya Sekondari Ushindi na baba mzazi wa marehemu, Japhet Nguku (37) mkazi wa Kijiji cha Msewe wilayani Mbarali.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamshna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema watuhumiwa wanadaiwa kumuua mtoto huyo Mei 3, mwaka huu kwa kumnyonga kisha kumnyofoa baadhi ya viungo. Kamanda Matei alisema mwili wa mtoto huyo ulikutwa umetelekezwa kwenye Msitu wa Hifadhi wa Chimala, wilayani Mbarali ukiwa umekatwa kanyagio la mguu wa kulia na baadaye ilibainika kuwa kanyagio hilo lilikuwa limefukiwa Mbalizi.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni tamaa ya fedha na Japhet alikubali kumuuza mtoto wake kwa mmiliki wa shule ya Ushindi kwa Sh. 5,000,000 ili achukuliwe viungo na kwenda kutengeneza ndagu (dawa ya utajiri) za biashara.

"Japheti alikubali kumtoa mtoto wake kwa Andrew ambaye ni mfanyabiashara wa shule ya sekondari ili akatwe kanyagio la mguu wa kulia kwa ajili ya kupeleka kwa mganga wa kienyeji ili atengenezewe ndagu kwa ajili ya kuendeshea biashara," alisema Kamanda Matei.

Alisema baada ya Japhet kukamatwa na kubanwa alieleza ukweli wa tukio hilo na ilibainika kuwa kanyagio la mtoto huyo lilikuwa limewekwa kwenye karatasi ya plastiki kisha kufukiwa Mbalizi umbali wa zaidi ya kilomita 70 kutoka eneo alipouawa. Alisema baada ya mmiliki wa shule kutajwa kuhusika na tukio hilo, alikamatwa na alipohojiwa alikiri kuhusika kisha wawili hao wakapelekwa selo wakati uchunguzi unaendelea kufanyika ili kubaini ukweli zaidi.

Kamanda Matei alisema kwa sasa Jeshi hilo linaendelea na ufuatiliaji wa tukio hilo ikiwa ni pamoja na msako wa kumtafuta mganga ambaye alikuwa anashirikiana na wauaji hao.

Hata hivyo, inadaiwa kuwa Japhet alikamatwa na wananchi wa Kata ya Nsalala katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi baada ya kumshtukia na aliendа akawaonyesha lilipofukiwa kanyagio la mtoto akidai kuwa ni la mtoto wake. Wananchi hao walimshtukia baada ya kutafuta mtoto kwa muda mrefu huku yeye akiendelea na biashara ya mafuta na walipombana alienda kufukua sehemu alipokuwa amefukia kanyagio la mtoto.

Mama mzazi wa mtoto aliyeuawa, Scola Chafungwe, alisema aliachana na mume wake baada ya kuchoshwa na mateso aliyokuwa anayapata ya kipigo.

Alisema wakati akiwa nyumbani kwao mkoani Njombe alipata taarifa kuwa mtoto wake aitwaye Rose amepotea akiwa na baba yake katika Mji wa Mbalizi na ndipo akafunga safari kwenda kumtafuta.

"Nimeishi na mwanaume huyu Igurusi kwa muda wa miaka 12 na tuna watoto wanne, lakini maisha yangu yalikuwa ya kutatanisha ndio maana niliondoka, Ijumaa nilipigiwa simu na kaka yangu kuwa eti mtoto amepotea, nilipowasiliana na mume wangu aliniambia yuko Mbalizi na ndiko mtoto amepotelea," alisimulia Scola.

Aliiomba serikali kumchukulia hatua kali za kisheria mwanamume huyo kwa madai kuwa hata wazazi wa mwanamume huyo wanashangaa sababu za kumchukua mtoto kinyemela na kuwaacha wengine kwa babu yao.

# Wazazi wanaokwamisha maendeleo waonywa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imewatahadharisha wazazi wanaokwamisha miradi ya maendeleo inayopelekwa na taasisi mbalimbali kwa ajili ya vijana kuwa watachukuliwa hatua za kisheria.

Tahadhari hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa jiji hilo, Vincent Msolla, kwa niaba ya Mkurugenzi wa Jiji hilo, James Kasusura, wakati wa kufunga mafunzo ya miezi minne kwa vijana yanayotolewa na Mradi wa Youth Building unaotekelezwa na Taasisi ya Catholic Relief Service (CRS) kwa kushirikiana na Shirika la Caritas Mbeya.

Mradi huo unatekelezwa na taasisi hizo katika kata mbili za Jiji la Mbeya ambazo ni Mabatini na Sinde na kushirikisha zaidi ya vijana 70 ambao wanafundishwa masuala ya ujasiriamali na uongozi.

Meneja wa mradi huo, Marilyn Chottah, alisema mradi huo unatekelezwa katika mitaa 10 ya kata hizo mbili, lakini changamoto wanayokabiliana nayo ni pamoja na baadhi ya wazazi kutotoa ushirikiano.

Alisema baadhi ya wazazi wanakwamisha mradi kwa kutumia fedha mabazo vijana wao wanatumiwa kwa ajili ya nauli za kuwawezesha kufika kwenye mafunzo na hivyo kushindwa kuhudhuria.

"Mradi unawahusisha vijana wenye umri wa miaka 18 na 26, tunashirikiana na serikali za mitaa husika, Caritas Mbeya na kampuni za ufundi, lakini changamoto inayotukabili ni baadhi ya wazazi kukosa ushirikiano na mradi," alisema Chottah.

Alisema kwa sasa mafunzo ya nadharia ambayo yamefanyika kwa miezi minne yamefikia ukomo na sasa vijana hao wanaenda kwenye kampuni mbalimbali kwa ajili ya kupata mafunzo kwa vitendo yatakayodumu kwa miezi mitatu.

Msimamizi wa mradi huo kutoka CRS, Nyanyonyi Neke, alisema baadhi ya vijana hawajitambui na hivyo kushindwa kushiriki kwenye mradi.

Alisema vijana hao wanaoshiriki kwenye mradi huo wanatoka katika familia zenye mazingira duni na huchujwa mpaka wapatikane ambao wanaweza wakafundishika na matokeo ya mradi yakaonekana.

Alisema baadhi huwa wanakuwa na sifa za kutoka kwenye familia duni, lakini wakifanyiwa usaili wanabainika kuwa hawajui hata kuandika majina yao na hivyo kuondolewa kwenye mradi na baadhi hukataliwa na wazazi wao.

Baada ya maelezo hayo, Ofisa Maendeleo wa Jiji la Mbeya, Msolla alisema kwa sasa serikali inataka ushirikiano na wadau mbalimbali, lakini wazazi wanaokwamisha miradi yao watashughulikiwa.





# Askofu akemea ufanyajikazi kimazoea

Na Peter Mkwavila, DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Dodoma, Amoni Kinyunyu amewataka Watanzania kuachana na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa Ibada maalum ya uzinduzi wa usharika wa Betheli pamoja na kutimiza miaka 10 ya Kanisa hilo.

Askofu Kinyunyu alisema kuwa yapo mambo ambayo yanashindikana kufikia malengo kutokana na baadhi ya watu kufanya kazi kimazoea jambo ambalo limekuwa likikwamisha shughuli za maendeleo.

Alisema kila kiongozi kwa sekta yake iwe serikalini, taasisi za umma, mashirika binafsi na taasisi za kiroho ni lazima kufanya kazi kwa kujituma na kuacha mazoea.

Akizungumzia watumishi mbalimbali wa serikali, alisema kuwa ili kujenga nchi yenye uchumi imara ni lazima kuwa na watu ambao hawana mizaha katika kazi wanazozifanya.

Kwa upande wa viongozi wa dini Askofu Kinyunyu alikemea viongozi ambao hawataki kufanya kazi ya Mungu kwa misingi ya kuongozwa na vitabu vitakatifu na badala yake wanafanya kwa mapenzi yao wenyewe.

Kwa upande wake mchungaji kiongozi wa Usharika wa Betheli, Mchungaji Elineema Mcharo, alisema kuwa pamoja na kanisa kutoa huduma ya kiroho imekuwa ikijishughulisha na utoaji wa misaada mbalimbali kwa jamii.

"Kanisa limekuwa likisaidia jamii kiroho, kimwili, kielimu na kiafya ikiwa ni sehemu ya kutimiza majukumu yake kwa misingi ya maandiko matakatifu ya biblia.

"Kwa kutambua kuwa kanisa linatakiwa kuwajali na kuwasaidia wahitaji kumeanzishwa miradi mbalimbali ikiwamo ufugaji wa samaki kwa lengo la kuinua pato la dayosisi na usharika kwa ujumla," alisema.

# Kutengeneza mifuko ya plastiki kosa la jinai

Na Renatha Msungu, DODOMA

KUFUATIA katazo la utumiaji mifuko ya plastiki ifikapo Juni, mwaka huu, jumla ya Watanzania milioni 26.5 tayari wamefikiwa na taarifa hiyo kupitia jumbe za simu zinazotumwa kwa kila mmoja.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, imeandaa kanuni kuhusu katazo hilo ambalo atakayebainika kuzalisha mifuko hiyo atakuwa ametenda kosa la jinai. Kutokana na kosa hilo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ili iwe fundisho kwa wengine.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Balozi Joseph Sokoine, alisema tayari wametoa maelekezo mahususi kwa sekretarieti za mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa katazo hilo ambalo baadhi wameanza kutenga maeneo ya kuhifadhi mifuko itakayo rasimishwa.

Balozi Sokoine alisema kwa mujibu wa kanuni hizo itakuwa marufuku kuzalisha au kuingiza na kusambaza mifuko ya plastiki. Alisema kwa kushirikiana na mitandao ya simu tayari wananchi wamepata taarifa kuhusu katazo hilo. Alifafanua zaidi kuwa wameandaa taarifa za kupeleka taasisi za kidini ili wasaidie kusambaza kwa waumini kuhusu katazo hilo.

Aliongeza kuwa wamekutana na wazalishaji wa mifuko mbadala na wamepanga kuongeza kasi ya uzalishaji wa mifuko hiyo.

Alisema serikali inaendelea kutoa taarifa kwa wananchi ili kuhakikisha wanafanikisha zoezi hilo la wananchi kuacha kutumia mifuko ya plastiki.

Alisema lengo ni kuhakikisha wanalinda afya za wananchi kutokana na kuepuka kutumia mifuko hiyo. Alifafanua kuwa kwa wale ambao watahitaji kusalimisha shehena za mifuko hiyo utaratibu utatolewa na mahali maalumu watakapotakiwa kupeleka.

Alisema Juni mosi, mwaka huu serikali itaendesha oparesheni kabambe nchi nzima ya kusaka mifuko ya plastiki ambayo itahusisha vyombo vya ulinzi na usalama vya mikoa na wilaya zake.

Oparesheni hiyo pia itahusisha mamlaka mbalimbali zikiwamo TFDA, Bandari, Viwanja vya Ndege, Uhamiaji na Usafiri wa nchi Kavu.



Mwenyekiti Chama cha Wabunge walio katika Mapambano dhidi ya Rushwa (APNAC) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, akifungua warsha kuhusu hali ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Mapambano dhidi ya Rushwa iliyofanyika jana, jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mavunde atekeleza ahadi ya mifuko 100

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

MBUNGE wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, ametekeleza ahadi yake ya kuwapatia mifuko 100 ya saruji wananchi wa kata ya Chigongwe kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati ya Msembeta.

Wananchi hao walikuwa wakikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa huduma za afya na kulazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 10 kufuata kijiji jirani.

Akishiriki jana hatua za awali za ujenzi wa zahanati hiyo, Mavunde alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa ahadi yake kwa wananchi hao aliyoitoa Aprili 6, mwaka huu.

"Wakati wa mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero za wananchi iliibuka hoja hapa ya ukosefu zahanati na mimi Mbunge wenu niliahidi kuanzisha ujenzi wake," alisema.

Mavunde aliahidi kusimamia kukamilika kwa zahanati hiyo na kuondoa adha ya wakazi 2300 ambao wanatembea kilomita 10 kufuata huduma za afya.

Esther Masimami kwa niaba ya wananchi wenzake, alimshukuru Mbunge Mavunde kwa kuanzisha mchakato huo wa ujenzi ambao utawapunguzia adha kubwa ya ukosefu huduma ya afya.

Alisema wananchi watahakikisha wanajitolea nguvukazi kama sehemu ya mchango wao kwenye ujenzi.





Naibu Waziri wa Elimu Zanzibar, Simai Muhammed Said (kushoto), akimkabidhi cheti Said Hassan Ali baada ya kuhitimu mafunzo ya maadili ya ndoa yanayotolewa na ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yashtushwa ndoa nyingi kuvunjika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhammed Said, amesema ndoa zinazoyumba na zenye mizozo hupelekea watoto kuathirika kisaikolojia.

Akizungumza na wahitimu wa mafunzo ya maadili ya ndoa kwa wanandoa na wanaotarajiwa kufunga ndoa katika Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar, alisema ndoa nyingi ambazo huzigharimu familia gharama kubwa hazidumu na kupelekea ongezeko la talaka.

Alisema ndoa hizo zimekua zikivunjika katika kipindi kifupi na hupelekea familia za mume na mke kubaki katika simanzi na huzuni kubwa. Alisema subra, uvumilivu na mapenzi ya kweli yanakosekana katika ndoa za siku hizi na kupelekea ndoa nyingi kuvunjika.

Aliwataka wahitimu wa mafunzo hayo kuimarisha ndoa zao kwa maslahi ya vizazi vyao na kuwa walimu kwa jamii katika kutoa elimu waliyoipata.

Naye Katibu wa Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar, Shekhe Fadhil Suleiman Soraga, alisema serikali kupitia ofisi ya Mufti imeamua kutoa mafunzo hayo kutokana na ongezeko kubwa la talaka na kuwataka wahitimu hao vyeti walivyopatiwa isiwe ni pambo bali kuyafanyia kazi kwa vitendo mafunzo hayo. Wahitumu hao walisema mafunzo waliyoyapata yatawaongezea namna ya kuwa na mapenzi ya kweli, kudumisha ndoa zao na kutatua migogoro itakayowakabili kwa kutumia misingi ya sheria ya dini ya kiislamu.

Khadija Mussa, aliiomba serikali kupitia ofisi ya Mufti iweke cheti cha mafunzo ya ndoa iwe ni kipengele cha kuzingatia kama ilivyo cheti cha kupima Ukimwi ambacho ni muhimu kwa wanaotaka kufunga ndoa.

"Pia tunaiomba ofisi ya Mufti kuweka matawi ambayo yataweza kutoa elimu hii maeneo ya vijijini ili kurahisisha upatikanaji wa mafunzo haya kwa jamii kwa kuwa baadhi yetu tunatoka vijijini tumekuja mjini kutafuta elimu hii," alisema.

Muhoro Haji Ali kutoka Ksiwani cha Tumbatu Kaskazini Unguja, alisema amejifunza mambo mengi katika mafunzo hayo, ikiwamo haki za mke, mirathi, talaka,malezi ya mtoto na jinsi ya kutatua migogoro katika ndoa.

Jumla ya wahitimu 43 walitunukiwa vyeti baada ya kumaliza mafunzo hayo wakiwamo wanawake 26 na wanaume 17.

# RC ataka maoni ya wananchi udhibiti mafuriko kuzingatiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema kuna haja ya kuzingatiwa ushauri wa wananchi wakati wa kutafuta ufumbuzi wa changamoto za mafuriko katika mitaa ili kupunguza ukubwa wa madhara yanayojitokeza.

Akitoa tathmini ya ziara aliyoifanya katika maeneo mbalimbali yaliyofurika maji ya mvua mkoani humo, Mkuu huyo wa mkoa alieleza kuwa hadi Mei tisa mwaka huu, wastani wa nyumba 2,160 zimeathirika kutokana na mvua kwa kuingiliwa na maji na nyingine kuanguka viwambaza kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha.

Alisema maeneo mengi yaliyoathiriwa na mvua hizo ni shehia ya Chumbuni, yametokana na kushindwa kutiririka vyema kwa maji yanayotoka katika mito sambamba na kuziba kwa maji kutoka katika njia zake za asili kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya ujenzi holela.

Alisema ili kutatua changamoto hiyo, kuna haja ya wataalamu wanaosimamia miradi ya ujenzi wa michirizi ya maji ya mvua, kukaa pamoja na kuzingatia ushauri unaotolewa na wakazi wa maeneo hayo badala ya kuzingatia utaalamu pekee kwa lengo la kuleta ufanisi.

Alieleza kuwa ziara aliyoifanya katika maeneo hayo imelenga kubaini ukubwa wa tatizo na kutafuta njia za dharura na za muda mrefu kupunguza makali ya madhara ambapo alimuagiza Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kutafuta njia itakayosaidia kuondoa maji katika maeneo hayo wakati maandalizi ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa kadhia hiyo yakiendelea.

Alisema ili kukabiliana na madhara ya mvua hizo, serikali kupitia kamati za maafa za taifa, mikoa, wilaya na shehia inaendelea kufanya tathmini ya athari hizo na kuanza kutoa misaada ya kibinadamu wakati ikitafuta suluhisho la kudumu kwa kuendelea na ujenzi wa mitaro ya kupitishia maji ya mvua ambayo imeanza kuwa na matokeo mazuri katika baadhi ya maeneo.

Aidha Ayoub aliwapa pole wananchi wote walioathiriwa na mvua hizo na kuwataka kuendelea kuwa na subira, na pia kuwaelekeza masheha kuendelea kufanya uhakiki wa kaya na maeneo yaliyoathirika katika maeneo yao ili kurahisisha upatikanaji wa huduma muhimu kwa kaya zilizoathiriwa.

Sheha wa shehia ya Chumbuni Juma Juma, alisema kunatokana na kupuuzwa kwa ushauri wa kamati yake kwa wataalamu wa ujenzi wa mtaro wa kupitishia maji ya mvua ulioanzia katika uwanja wa Mzizima kwa Mzushi, jambo lililopelekea mtaro huo kushindwa kufanya kazi ipasavyo.

Alisema awali maeneo ya Chumbuni yalikuwa hayaingii maji kutokana na maji kupitia katika mto, lakini baada ya ujenzi huo na maji kuelekezwa katika mtaro huo kumepelekea kuongezeka kwa wingi wa maji.

Sheha huyo alisema wastani wa nyumba 60 huathiriwa na maji ya mvua kila mwaka ambapo katika mwaka huu nyumba 18 zimeathirika katika shehia hiyo na kusababisha zaidi ya kaya 20 kuhama au kuishi kwa shida katika makaazi yao.

Mkuu wa michirizi wa Manispaa ya Mjini, Mzee Khamis Juma, alieleza katika kutatua changamoto hiyo, serikali imeingiza eneo hilo katika awamu ya tatu ya mpango wa ujenzi wa mradi wa huduma za jamii mijini (ZUSP) unaotarajiwa kuanza utekelezaji wake mwakani.

## Waaswa uhujumu wa miundombinu

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

WANANCHI wa Jimbo la Pangawe, wametakiwa kuacha kuifanyia hujuma miundombinu ili iweze kuwasaidia.

Hayo yameelezwa na Mwakilishi wa jimbo hilo, Khamis Juma Maalim, wakati alipofanya ziara ya kuangalia familia zilizoathirika kutokana na mvua za masika zinazoendelea kunyesha katika eneo la Pangawe bondeni Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

Alisema kitendo cha baadhi ya wananchi kutia taka katika mitaro husababisha kutuama maji na kurudisha nyuma juhudi zilizochukuliwa na viongozi wao kuijenga.

Aidha, aliwataka wakaazi hao kuizibua mara moja mitaro hiyo ili kuepuka maafa.

Khamis ambae pia ni Waziri wa Katiba na Sheria, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitomfumbia macho mtu yeyote atakayebainika kuharibu miondombinu kwa makusudi ili kuepukana na athari zinazoweza kujitokeza.

Aliwataka wananchi hao kushirikiana na viongozi wao ili kuhakikisha wanalinda na kuitunza miondombinu kama vile ya maji, umeme na barabara ili iwe endelevu na kufikia malengo yaliokusudiwa.

Kwa upande wake Diwani wa kuteuliwa Wilaya ya Magharibi 'B', Thuwaiba Jeni Pandu, alilishukuru Baraza la Manispaa Wilaya ya Magharibi 'B' kwa kukubali kumalizia ujenzi wa mtaro huo ulioachwa na viongozi wa Jimbo jambo ambalo litaweza kuwasaidia wakati utakapokamilika.

Kwa upande wao wakazi wanaokaa karibu na mtaro huo waliiomba Serikali kuwachukulia hatua kali wanaofanya uharibifu wa mazingira ili kulikomesha kabisa tatizo hilo lililodumu kwa muda mrefu na kuiathiri jamii.

## Wagoma kufanya usafi stendi kwa kutolipwa

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

SAKATA la madai ya wahudumu 11 wa usafi katika soko na kituo cha magari Buseresere, wilayani Chato, mkoani Geita limechukua sura mpya baada ya kugoma kufanya usafi kushinikiza kulipwa madai yao ya kati ya miezi miwili hadi minne.

Wakizungumzia hatua hiyo jana, baadhi ya wahudumu hao Auleria Laulian na

Majadala Msumbwa, walidai ni kutokana na kutotekelezwa kwa agizo la Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, baada ya kutoa saa 48 kulipwa, lakini hadi jana ikiwa ni siku ya tano hawajalipwa hali iliyosababisha kusitisha kufanya usafi.

Akithibitisha kugoma kwa wahudumu hao, Mwenyekiti wa Kijiji cha Buseresere, Deus Musiba, alisema hatua hiyo imesababisha hofu ya kuwapo kwa uwezekano wa kutokea magonjwa ya milipuko hasa katika kipindi hiki cha mvua.

"Ni kweli wamegoma toka juzi hawafanyi kazi...hata mimi nakiri kuwa madai yao yana msingi kwa sababu baadhi yao wanadai kati ya miezi miwili hadi minne na anayepaswa kuwalipa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, baada ya kukichukua chanzo hicho cha Mapato," alisema.

Baadhi ya wafanyabiashara wanaoendesha biashara katika soko na kituo cha mabasi Buseresere, walielezea athari zilizoanza kujitokeza kutokana na mgomo huo kuwa ni pamoja na Uchafu na harufu mbaya.

Wiki iliyopita Mei 4, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, alitoa saa 48 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Eliud Mwaiteleke, katika mkutano wa hadhara wahudumu hao kulipwa madai yao huku akionekana kukurewa na hatua hiyo ikiwamo wa hudumu hao kufanya kazi bila vitendea kazi.

Alikiri katika mkutano huo kuwa angeweza kutekeleza agizo hilo na kumuahidi Mkuu wa Mkoa kuwa wangelipwa kama alivyoagiza huku akijitetea kuwa makusanyo katika soko na kituo hicho cha mabasi yameshuka.

Hata hivyo utetezi huo ulipingwa na Diwani wa Kata ya Buseresere, Godfrey Miti, mbele ya Mkuu wa Mkoa akisema makusanyo yanayopatikana yanatosha kuwalipa wahudumu hao na kubaki na kama halmashauri ya

wilaya imeshindwa kukisimamia chanzo hicho basi kirejeshwe kwa wananchi kwa serikali ya kijiji au kata ili ikisimamie kama ilivyokuwa awali.



Waziri Mkuu mstaafu , Mizengo Pinda , (kulia) akiongea na Mjumbe wa Bodi ya Kampuni ya Moutai Group ya China, Wang Yan (Kushoto), wakati wa Kongamano la Biashara na Utamaduni lililoandaliwa na Kampuni ya China Moutai Group katika ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ambalo pia liliambatana na uzinduzi wa kinywaji cha Kweichow Moutai nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aomba wachungaji wa makanisa kuhakikiwa

**Na George Tarimo,** MUFINDI

SERIKALI imeombwa kuweka utaratibu maalumu utakaotumika kuwatambua wachungaji na makanisa yao badala ya utaratibu wa sasa unaotaka kanisa kusajiliwa Wizara ya Mambo ya Ndani bila kuweka mwongozo wa nani anaruhusiwa kuchunga kanisa.

Ombi hilo limetolewa na askofu wa kanisa la Havest Gospel Pentekoste, Emmanuel Mhina, kwenye ibada ya kusimikwa kwa Askofu Mkuu wa kanisa la True Gospel Embassy nchini, Cretus Mpwepwa, katika kijiji cha Kinegembeasi wilayani Mufindi, mkoani Iringa.

Askofu Mhina alisema utaratibu wa sasa umeweka wazi kwa watu wote wenye tamaa ya kujivika utumishi wa Mungu kwa lengo la kujipatia fedha kinyume na taratibu. Kadhalika alisema viongozi wengi hasa wanaojiita wachungaji hawajasoma kwenye vyuo vya biblia na hivyo kuwa rahisi kupata upenyo wa ukengeufu wa imani, lakini hao watumishi wanapojiunga kwenye vyuo hivyo wanajifunza mambo mengi ambayo yanatakiwa kuwasilishwa kwa jamii.

"Ninakemea vikali viongozi kama hawa wanaotoa mafundisho ya kupotosha badala ya kufundisha jamii, lakini pia nimeona baadhi ya nchi kama Rwanda wameweka sheria ya kutaka wachungaji wawe na elimu ya kiasi fulani na sisi kama Tanzania inatakiwa tuweke msisizitizo kama huo ili tuweze kupata viongozi bora na wenye maadili kwa taifa," alisema Mhina.

Alimtaka askofu aliyesimikwa uaskofu kuzingatia mambo kadhaa wakati wa kuhudumia waumini wake ikiwa ni pamoja na kulihubiri neno, kuandaa moyo wake katika hali ya kupokea mambo makubwa na kuyatatua, awe mtu mwenye karipio au kuonya, kuwa mkaribishaji, kutokuwa mtu wa kupenda fedha, kutokuwa na ubinafsi, kutokuwa mwepesi wa hasira, kutenda mema, kudumu katika utakatifu pamoja na kuwa mtu mwenye kudhibiti nafsi.

Naye Katibu wa kamanisa ya Pentekoste Wilaya ya Mufindi, askofu Benson Nyalus, alimshauri askofu Mpwepwa kuilinda nia yao iwe ile ile ya Kristo Yesu ambayo ilikuwa watu waache dhambi wafuate yaliyo mema pamoja na wachungaji kuacha kutafuta fedha kwa waumini wao kwa kuwa nia ya Kristo Yesu ilikuwa siyo hiyo bali ilikuwa ni kuhubiri neno.

Kwa upande wake Askofu Mpwepwa alizungumza baada ya kusimikwa alisema atahakikisha kanisa hilo linajenga vituo vingi vya kulea watoto wenye mazingira hatarishi ikiwa ni moja ya nia yao kama kanisa kuendelea kutoa elimu kwa jamii.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Mufindi ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye ibada hiyo, Hezron Myinga, aliwaomba viongozi wa dini kuhubiri amani na kuombea viongozi wote wa serikali kuanzia ngazi ya chini hadi ya kitaifa.

# Wauguzi waomba kuboreshewa mazingira ya kazi

**Na Steven William,** MUHEZA

WAUGUZI kutoka katika hospitali mbalimbali wilaya tisa katika Mkoa wa Tanga, wameiomba serikali kuwaboreshea mazingira ya utoaji huduma katika maeneo ya kazi kwa kupatiwa vitendea kazi vya kutosha.

Maombi hayo yamo katika risala ya Siku ya Wauguzi Duniani iliyosomwa na Katibu Mkoa wa Tanga, Hadija Mbasha, katika maadhimisho yaliyofanyika kimkoa halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

Mgeni rasmi katika sherehe hizo alikuwa Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Abdi Makange.

Katika risala yao, waliiomba serikali kuwaboreshea mazingira ya utoaji huduma kwenye maeneo yao ya kazi kwa kupatiwa vitendea kazi bora na vya kutosha.

Walisema wanahitaji kupandishwa vyeo kwa wakati pamoja na kulipwa stahili zao za pesa za saa za ziada, pesa za sare ambazo kwa sasa ni Sh. 120,000 lakini waajiri wao hawalipi.

Pamoja na utoaji huduma bora kwa jamii, walisema wauguzi wanachangamoto kubwa ikiwamo upungufu wa hali ya juu wa wauguzi, vitendea kazi, ucheleweshwaji wa kupandishwa vyeo na ukosefu wa nyumba za kuishi kwa wauguzi wanaofanyakazi vituo vilivyopo vijijini.

Changamoto nyingine ni pamoja na wauguzi wa ngazi zote kukosa haki ya msingi kama vile malipo ya kujikimu wakati wa kusafirisha wagonjwa kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine, kikizo, malimbikizo ya mishahara na ukosefu wa bajeti katika halmashauri za kushughulikia masuala ya wauguzi.

Muuguzi Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Hawa Kayuzi, alisema Mei 12, kila mwaka wanaadhimisha sherehe hiyo ambayo ndiyo tarehe aliyozaliwa mwanzilishi wa wauguzi duniani Florence Nightngale, mwaka 1820 huko nchini Italia katika mji wa Florence. Naye Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Flora Kessy, alisema siku ya wauguzi dunia ni muhimu, inatoa fursa ya wauguzi kutoa kero zao ambazo zinawakabili katika maeneo yao ya kazi huku akiwataka kufanya kazi kwa bidii, upendo na uvumilivu.

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Makame, alisema uuguzi ni kada muhimu katika ufanikishaji utoaji huduma bora za afya katika jamii na kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Wauguzi sauti iongozayo kwa wote'.

Alisema kuwa wauguzi wanaendelea kuchangia kwa kasi kubwa kupunguza vifo vya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano katika Tanzania na Mkoa wa Tanga.

HABARI KIMATAIFA

## Askari wa Ufaransa wauawa Burkina Faso

**OUAGADOUGOU, Burkina Faso**

MATEKA wawili wa Ufaransa, raia mmoja wa Marekani na raia mmoja wa Korea Kusini wameachiliwa baada ya vikosi vya Ufaransa kuendesha operesheni kabambe kaskazini mwa Burkina Faso.

Mateka hao wawili wa Ufaransa walitekwa Mei 1, mwaka huu katika Hifadhi ya Taifa ya Pendjari kaskazini mwa Benin ambako walikuwa wakisafari.

Hata hivyo, kwenye operesheni ya kuwaokoa mateka hao, askari wawili wa Ufaransa waliuawa.

Katika taarifa iliyotolewa na Ikulu ya Burkina Faso ilitangaza kwamba watalii hao wawili wa Ufaransa walitekwa nyara Jumatano wiki iliyopita kaskazini mwa Benin, katika Hifadhi ya Taifa ya Pendjari, kwenye mpaka na Burkina Faso ambapo kunaripotiwa kuna makundi kadhaa ya wanamgambo wa kjihadi.

Mwanamke mmoja kutoka Marekani na mwengine kutoka Korea Kaskazini pia wameokolewa katika operesheni hiyo ya vikosi vya jeshi la Ufaransa, Elysee imebaini

*RFI*

## UN yasema msaada wa dharura wahitajika DRC

**KINSHASA, Congo**

TAARIFA kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) zinasema kumekuwapo na matukio makubwa ya uvunjifu wa amani ambayo yameyumbisha juhudi za kukabiliana na ugonjwa wa Ebola eneo la Butembo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na baadhi ya maeneo nchini humo.

Kwa mujibu wa msemaji wa Umoja wa Mataifa (UN), Farhan Haq alisema wakati operesheni zikiwa zimezinduliwa upya Ijumaa, WHO inamatumaini kwamba harakati za kuchukuwa vipimo katika maabara ambazo bado zinakabiliwa na vizuizi, itasababisha kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa wenye virusi vya Ebola katika siku zijazo.

Alisema mlipuko wa ugonjwa huo uko katika hatua hatarishi, ambako kwa sasa kunaongezeko la maambukizi katika wiki za hivi karibuni jambo ambalo linahatarisha kuenea kwa maambukizi hayo katika majimbo mengine nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na nchi jirani. WHO imesema kunahitajika msukumo mkubwa wa msaada wa kisiasa na kifedha kutoka kwa wahusika nchini DRC na Kimataifa kukabiliana na hali hiyo tata.

*VOA*

# China, Marekani zatoa kauli zinazokinzana

**ASHINGTON, Marekani**

MVUTANO wa kibiashara kati ya Marekani na China umeendelea huku nchi hizo zikitoa kauli zinazokinzana.

Mvutano huo umetokea wakati ambapo Rais wa Marekani Donald Trump akiongeza ushuru maradufu kwa bidhaa za China zinazoingia Marekani.

China na Marekani zinatoa taarifa zinazokinzana juu ya mazungumzo yao ya biashara yanayoendelea kwa sasa.

China imesema bado ina matumaini kuhusu kuutatua mvutano wa kibiashara, wakati Marekani imesema imeongeza ushuru mara mbili kwa bidhaa kutoka China.

Hata hivyo, mjumbe wa China katika mazungumzo na Marekani Liu He ameonya kwamba kuna viwango vimeongezwa na Marekani ambavyo nchi yake haitakuwa tayari kuvivuka.

Makamu wa Waziri Mkuu wa China, Liu He alisema mazungumzo kati yake na Marekani hayajavunjika licha ya kuwapo vikwazo vidogo ambavyo ni vya kawaida, kwamba China itaendelea kuwa na mtazamo chanya juu ya mazungumzo ya biashara na Marekani, licha ya Rais Trump kuamua kuziongezea ushuru bidhaa za China.

Maoni ya Liu yanakinzana na ya Waziri wa Fedha wa Marekani, Steve Mnuchin, ambaye aliwaambia waandishi wa habari kwamba hakuna mazungumzo yoyote ya biashara yaliyopangwa kufanyika kati ya nchi hizo mbili kwa sasa.

Rais Trump amejisifu kwa kuandika kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter kwamba ameikomoa China kwa kiasi ambacho labda nchi hiyo haitotaka kurudi kwenye meza ya majadiliano kabla ya uchaguzi wa mwaka 2020.

Marekani imechochea vita vya biashara kwa kuongeza ushuru kwa thamani ya Dola za Marekani bilioni 200 kwa bidhaa za China zinazoingia nchini humo.

Gazeti la kizalendo la Global Times liliandika kwenye tahariri yake kwamba Marekani haijatambua maslahi ya pande zote mbili, na wala haizingatii kwa kiasi kikubwa uvumilivu wa China.

Siku ya Ijumaa, Rais Trump aliweka vikwazo vipya dhidi ya bidhaa zinazoingia Marekani kutoka China. Hatua hiyo iliongeza ushuru kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwenye bidhaa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na simu za mkononi, kompyuta na vitu vya kuchezea watoto.

Wizara ya Biashara ya China ilieleza kuwa imehuzunishwa sana na uamuzi huo wa Marekani. *DW*



Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, akiwa na mkewe wakiangalia matokeo ya uchaguzi ubaoni. **PICHA: REUTERS**

# Guaido ataka uhusiano na jeshi la Marekani

**CARACAS**

KIONGOZI wa upinzani Venezuela, Juan Guaido amesema amemuagiza mjumbe wake wa kisiasa mjini Washington, Carlos Vecchio kuanzisha mara moja uhusiano na jeshi la Marekani.

Lengo kuu likiwa ni kumpa wakati mgumu Rais wa Venezuela, Nicolas Maduro ajiuzulu.

Guado alisema amemuagiza Vecchio, ambaye Marekani inamtambua kama balozi wa Venezuela, kuanzisha mawasiliano ya moja kwa moja kuelekea ushirikiano wa kijeshi.

Kauli hizo, alizotoa wakati wa maandamano likiwa ndilo ombi kubwa zaidi kuwahi kutolewa kwa Marekani kuingilia kati mzozo wa nchi hiyo unaoongezeka kwa kasi.

Juzi, Waziri wa Ulinzi wa Venezuela, Vladmir Pradino, alilaani kile alichokiita kuwa ni uvamizi haramu uliofanywa na meli ya Marekani katika mipaka ya Venezuela.

Pradino hakutoa ushahidi wa kuunga mkono madai hayo lakini alisema wanajeshi wa majini wa Venezuela walilazimika kuondoka.

Katika maandamano hayo, Guaido aliwataka wafuasi wake kutokuwa na uwoga na kuyaendeleza maandamano ya kitaifa dhidi ya Rais Maduro, ambaye amekuwa akimpa wakati mgumu tangu jaribio la mapinduzi ya kijeshi.

Watu wapatao 2,000 walifurika katika uwanja wa eneo lenye wafuasi wengi wa upinzani la mashariki mwa Mji Mkuu Caracas kumsikiliza Guaido, lakini hiyo ilikuwa idadi ndogo ikilinganishwa na maelfu ya watu walioshiriki katika maandamano ya awali.

Guaido mwenye umri wa miaka 35, ameongoza maandamano ya mara kwa mara ya kutaka Rais Maduro ajiuzulu na kulitaka jeshi kutomtii Rais Maduro, ambaye anaendelea kupata uungaji mkono kutoka kwa Urusi na China.

Marekani na Umoja wa Ulaya wamelaani vitendo vya serikali ya Rais Maduro dhidi ya wabunge wa upinzani. *DW*

# Serikali yakuna wawekezaji nyama, maziwa kwa udhibiti

**Na Mwandishi Maalum, ARUSHA**

WAWEKEZAJI wa viwanda vya kuchakata nyama na maziwa, wameishukuru Serikali kwa hatua inazochukua za kudhibiti uingizaji holela wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi kwani imesaidia kuwawezesha kuanzisha viwanda vipya kutokana na kuweapo uhakika wa soko la bidhaa wanazozalisha.

Hivyo wafugaji nao kunufaika na fursa ya uwapo wa viwanda kwa kuwa sasa watauza mifugo hai na maziwa kwenye viwanda hivyo na kuachana na tabia ya kutorosha mifugo hai kwenda nchi jirani kuhangaika kutafuta soko.

Wakizungumza mbele ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, aliyetembelea kukagua ujenzi wa Kiwanda kipya cha nyama cha Eliya Foods Over Seas Limited kilichopo Longido na Kiwanda cha maziwa cha Kilimanjaro Fresh kilichopo jijini Arusha wamesema wamefikia hatua ya kuanzisha viwanda hivyo vipya kutokana na msukumo mkubwa walioupata wa serikali ya awamu ya tano kudhibiti uingizaji holela wa bidhaa hizo kutoka nchi za nje.

Mkurugenzi wa Eliya Foods Over Seas Limited, Shabbir Virjee, alisema kiwanda hicho cha nyama kina uwezo wa kuchinja ng'ombe 500 na Mbuzi 2,000 kwa siku, huku kikitarajiwa kutoa ajira za Watanzania 200 na kwamba watanunua mifugo kutoka Wilaya ya Longido na maeneo mengine nchini na kuishukuru Serikali kwa hatua inazochukua za kulinda wawekezaji wanaowekeza nchini.

Naye Meneja Mkuu Kampuni ya Galaxy Food & Beverage Ltd wazalishaji wa maziwa ya Kilimanjaro Fresh, Irfhan Virjee, aliishukuru Serikali ya kwa uamuzi wake wa kuweka tozo mpya kwenye uagizaji bidhaa za maziwa kutoka nje ya nchi hali iliyowezesha kuamua kuanzisha kiwanda hicho kutokana na kuwapo ushindani ulio sawa wa biashara tofauti na ilivyokuwa siku za nyuma ambapo isingekuwa rahisi wao kujenga kiwanda hicho.

Alisema uamuzi huo wa Serikali umewawezesha kuzalisha maziwa kwa gharama nafuu na kuwafikia watumiaji wa mwisho kwa bei nafuu, huku wafugaji nao wakinufaika kwa kuuza maziwa yao kwa bei nzuri ambapo kwa sasa wameanza kuzalisha lita 5, 000 kwa siku lakini kiwanda hicho kinauwezo wa kuchakata lita 75,000 kwa siku.

Waziri Mpina aliwahakikishia wawekezaji wa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo nchini kuwa hakuna mtu yeyote atakayechezea soko la bidhaa hizo kwani Serikali iko macho wakati wote kudhibiti uingizaji holela wa mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi.

Hivyo alisititiza kuwa hatua zinazochukuliwa na Serikali kudhibiti utoroshaji wa mifugo nje ya nchi na kudhibiti uingizaji holela wa bidhaa za nyama na maziwa hazikulenga kumuonea mtu bali kutengeneza mazingira mazuri kwa wawekezaji wa viwanda hivyo kuwekeza nchini.

Mpina alisema kuanza kwa viwanda hivyo vipya ni uthibitisho kuwa Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji kuja kuwekeza nchini baada ya wawekezaji wengi siku za nyuma kulazimika kufunga viwanda vyao na kukimbia kutokana na utitiri wa bidhaa zilizoingia nchini kwa njia za panya na kutokuwapo ushindani ulio sawa kwenye biashara.

Msajili wa Bodi ya Nyama, Imani Sichwalwe, alimhakikishia Waziri Mpina kuwa wataendelea kuvutia wawekezaji zaidi kwenye sekta ya nyama na kuwasaidia pia kupata masoko katika mataifa mengine duniani ikiwamo Ulaya na China.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alimhakikishia Mpina kuwa wilaya hiyo itaendelea kutekeleza kwa vitendo maelekezo yake katika kulinda rasilimali za mifugo na kupambana na vitendo vyote vya uhujumu wa rasilimali hizo ikiwamo utoroshaji wa mifugo kwenda nchi nyingine bila kufuata sheria.




Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango, akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Rukia Muwango, msaada wa vitanda vitano, magodoro na shuka 25 zilizotolewa na Benki hiyo kwa ajili ya kusaidia huduma katika Zahanati ya Majimaji inayomilikiwa na kikosi cha 41 kj Nachingwea ikiwa ni mpango wa benki hiyo kusaidia jamii katika hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika katika kambi hiyo wilayani Nachingwea. **PICHA: NMB**

# Wauguzi wakumbushwa maadili ya kazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAUGUZI wametakiwa kuendelea kutekeleza majukumu ya kazi kwa kuzingatia kanuni na taratibu za kitaaluma kwa lengo la kutoa huduma bora za afya kwa wagonjwa.

Wito huo ulitolewa jana na Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, Agnes Mtawa, katika maadhimisho ya siku ya Uuguzi na Ukunga Duniani ambayo yalifanyika Hopistali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kuudhuriwa na wauguzi na wakunga wa MNH na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI).

Maadhimisho hayo hufanyika Mei 12, kila mwaka na kauli mbiu ya mwaka huu ni "Wauguzi Sauti inayoongoza Afya kwa Wote." Mwaka huu kitaifa maadhimisho yanafanyika mkoani Katavi.

Mtawa aliwakumbusha wauguzi kuzingatia mafunzo yanayotolewa mahala pa kazi kwani ndio yanayochochea kutoa huduma bora ya afya kwa wagonjwa.

Aliwataka wauguzi kutambua kwamba huduma wanayotoa kwa wagonjwa ni huduma ya kibinadamu kwani elimu inachangia kufikia malengo ya kutoa huduma bora.

"Hivi sasa mambo yetu yanakwenda vizuri. Malalamiko mengi yamepungua kwani ukifuatilia utabaini kwamba malalamiko mengi ni ya wagonjwa au mgonjwa kutaka kupewa kipaumbele kupata huduma ya afya badala ya kufuata utaratibu," alisema Mtawa.

Pia, Msajili aliwapongeza wauguzi kwa kutekeleza majukumu ya kutoa huduma za afya kwa kuzingatia taratibu za kitaaluma kwa asilimia 100.

Akisoma risala katika maadhimishisho, Katibu wa Chama cha Uuguzi na Ukunga Tanzania, tawi la Muhimbili, Seif Hamisi, aliomba vitendo vya udhalilishaji kwa wauguzi vifanyiwe kazi kwa kuwa vinawapunguzia ari ya kufanya kazi.

Naye, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Muhimbili, Makwaia Makani, aliwataka wauguzi kutoa taarifa kwa uongozi wa MNH endapo watadhalilishwa wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kila siku ili watakaobainika wachukuliwe hatua za kisheria.

## Kakobe aenda kanisani kwa Gwajima kumsafisha

**INATOKA UK. 3**

alisema Askofu Kakobe.

Alisisitiza kuwa injili ni kwa ajili ya watu wote na alimsifu Askofu Gwajima kuwa na roho ya kusamehe watu waliomkosea.

Alisema Askofu Gwajima amesamehe bila masharti kama vile Bwana Yesu alivyosamehe bila ya masharti yoyote waliokuwa wamemkosea na kwamba kufanya hivyo ni ukomavu kwa kiimani zaidi ya ukomavu wa kisiasa.

Askofu Kakobe alijitolea mfano kuwa, yeye alirushiwa mishale ya kila namna lakini ameendelea kuwa imara na alimtaka Askofu Gwajima kutokuwa na muda wa kuendelea kujisafisha.

Aliwasihi waumini wa kanisa hilo kuwa, watu wakiendelea kuwazodoa kuwa Mchungaji wao ni mzinzi wajibu kufuatana na maandiko ya biblia takatifu kitabu cha 1Thimotheo 5:19 kinachosema 'usikubali mashtaka juu ya mzee mpaka kuwapo na vinywa vya mashahidi wawili hadi watatu'.

Alihoji kama upo ushahidi wa vinywa vya watu wawili na watatu vitoe na kama hamna hawawezi kukubali mashtaka juu ya mtumishi huyo.

Askofu Kakobe aliwataka waumini huo kutokuwa sehemu ya kuendelea kusema kuhusu jambo hilo ambalo wameshalifunga kiimani. Alisema Askofu Gwajima anaujasiri wa hali ya juu jambo ambalo Mungu anajivunia yeye, hivyo adui anatumia uovu kumuangusha mtumishi huyo.

"Askofu Gwajima ni jasiri kama simba, najivunia yeye, na hata siku nikitwaliwa (nikifa) najua yamebaki majemedari na 'I am so proud of you', naona fahari juu ya Gwajima na naona fahari juu yenu wote," alisema Askofu Kakobe huku akishangiliwa.

Mbali na Askofu Kakobe, maoskofu wa makanisa mengine walifika kwa ajili ya kumsafisha na Askofu Gwajima huku wakimtaka asikatishwe tamaa na jambo lolote. Maaskofu hao walisema wanaendelea kuwa nyuma yake na kumuunga mkono katika kazi ya Mungu inayofanywa na Askofu Gwajima na kamwe hawatarudi nyuma.

**Kauli ya Polisi**

Baada ya kuwapo kwa kashfa hiyo, Kamanda wa Polisi, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, aliibuka na kueleza kuwa kilichotokea kwenye video ile ni kumchafua mtumishi huyo wa Mungu huku akiahidi kuendelea na uchunguzi ili kubaini waliohusika.

Alisema Jeshi la Polisi Makao Makuu, Kitengo cha Upelelezi wa Makosa ya Jinai, linalifanyia kazi suala hilo na kuwataka waumini wa kanisa lake kuwa watulivu wakati wakiendelea na kazi hiyo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**EZRON BARONGO HINGABUNDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 812 AHF M/CANTER.** Chassis namba **FE425E520375.** Engine namba **4D32595533.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **BI/RB/265/2019.**

115224302

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT BUKOBA**
**LAND CASE APPLICATION NO. 104/2016**
**WINFRIDA FELISIAN ..........................APPLICANT**
**VRSUS**
1. **SEPERATUS KASITA**
2. **GEORGE KAMANZI......................RESPONDENTS**

**To George Kamanzi**
**Kashai Ward**
**BUKOBA MUNICIPAL**

**RE: NOTICE OF DATE MENTION**

Whereas the above mention Applicant lodged a case registered as Misc. Land Application No. 104/2016 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said Case has been scheduled for Mention on 28th day of May, 2019 at 9:00 am before Hon. Judge F. H. Mtulya. You are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case may hand and seal of the Court this 7th day of May 2019.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

115224202


NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz

au piga Simu: 0767 223 311



JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?


Nipashe

NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



## ZIDANE: WEWE BALE ONDOKA TU

**MADRID, HISPANIA**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane ameamua kumaliza utata baada ya kumwambia mshambuliaji wake, Gareth Bale kwamba anaweza kuondoka.

Gazeti la Marca limeripoti kwamba, Zidane amekuwa akifanya mawasiliano binafsi na wachezaji wake kwenye kikosi kuwaeleza mmoja mmoja kama nani anamtaka abaki kwenye kikosi hicho kwa msimu ujao.

Bale, Marcos Llorente na Dani Ceballos ni wachezaji watatu wa kwanza kukutana na maneno ya aina hiyo kutoka kwa kocha huyo raia wa Ufaransa.

Na sasa wachezaji hao wanajitambua wamekuwa wa ziada tu kwenye kikosi kama wataendelea kubaki hapo huku Kocha Zidane akitarajia kuondoka wakati dirisha la usajili ujao wa majira ya kiangazi litakapofunguliwa hivi karibuni.

Bale na Zidane wameripotiwa kutokuwa kwenye uhusiano mzuri tangu aliporudi kwenye klabu hiyo huku kukiwapo na taarifa nyingi kwamba mwanasoka huyo aliyesajiliwa kwa ada iliyovunja rekodi ya dunia mwaka 2013 hatakiwi kuwapo Bernabeu kwa msimu ujao.



# BARCA KUWAPIGA BEI NYOTA WATATU

**BARCELONA, Hispania**

WACHEZAJI Philippe Coutinho, Sergio Busquets na Jordi Alba wameripotiwa kwamba huenda wakauzwa kutoka kwenye kikosi cha Barcelona baada ya kucheza vibaya dhidi ya Liverpool na kuigharimu timu hiyo kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kocha Ernesto Valverde naye yupo kwenye mashaka makubwa kuhusu usalama wa ajira yake huko Nou Camp baada ya kikosi hicho kupoteza uongozi wake wa mabao 3-0 na kuchapwa 4-0 huko Anfield katika nusu fainali ya pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa mujibu wa Gazeti la AS, kuna wachezaji watatu ambao wapo kwenye hatari ya kuondolewa kwenye kikosi kutokana kipigo hicho cha aibu.

Coutinho ameshindwa kuonyesha makali kwenye mechi hiyo iliyomshuhudia akirudi Anfield na hakumaliza mechi hiyo. Amekuwa akihusishwa na Chelsea, lakini mashabiki wa timu hiyo wameiambia klabu yao isimsajili baada ya kiwango cha ovyo. Coutinho ameshindwa kucheza kwenye ubora wake tangu alipotua Nou Camp Januari mwaka jana kwa ada ya Pauni 145 milioni.

Kuhusu Busquets, ambaye yupo kwenye timu hiyo kwa miaka 11, huenda naye akakumbana na panga sawa na kinachodaiwa kwamba kitamkuta Alba. Baada ya mechi, Busquets aliwaomba radhi mashabiki wa Barcelona kwa kile kilichotokea AS Roma msimu uliopita na huko Liverpool msimu huu kwenye michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Chelsea yapanga kumbakiza Hazard

**LONDON, England**

KLABU ya CHELSEA wanafanya kila njia kumfurahisha Eden Hazard ili abaki kwenye kikosi chao kwa ajili ya msimu ujao.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amekuwa akihusishwa na mpango wa kutimkia Real Madrid katika dili linaloweza kutimia ada ya pauni milioni 100.

Lakini, Hazard baada ya kupewa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa timu hiyo pamoja na ile ya bao bora la msimu, aliulizwa kama atasaini mkataba mpya wa kuendelea kubaki Stamford Bridge.

Na yeye haraka alijibu kwamba yupo tayari kubaki na miamba hao ambao wametinga fainali ya Ligi ya Europa na sasa watavaana dhidi ya Arsenal Mei 29, mwaka huu.

Mashabiki wa Chelsea wameripotiwa kufurahishwa na jambo hilo, lakini walitumia kurasa zao za siku kuhoji kwa nini hakupewa peni haraka asaini ili waondokane na presha ya kumpoteza staa wao.

Hata hivyo, shabiki mwingine alikuwa na mtazamo tofauti akisema maneno hayo ya Hazard ni ya kuwanyanyasa tu.

Mkataba wa Hazard utafika tamati mwishoni mwa msimu wa 2020, lakini kutokana na Chelsea kutumikia adhabu ya kuzuiwa kusajili kwa kipindi cha mwaka mmoja, jambo hilo linawafanya kuweka nguvu katika kumwaachia staa huyo aondoke kwa sababu hawatakuwa na nafasi ya kusajili nyota mpya wa kuziba pengo lake.

Baadhi ya mashabiki wanaamini kwamba Hazard hatasaini dili jipya kwenye timu yao, isipokuwa ataendelea kubaki hapo Stamford Bridge ili kuokoa pauni milioni 100 za Real Madrid, ambapo atakapokwenda kujiunga nao bure mwishoni mwa msimu ujao atakwenda kulipwa mshahara mara mbili ya kiwango anachovuna kwa sasa kwenye kikosi cha 'The Blues'.

Kama Hazard akibaki Chelsea atakuwa na ruhusa ya kusaini mkataba wa awali na Real Madrid itakapofika Januari mwakani.



# HERRERA AONDOKA RASMI MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

KIUNGO Ander Herrera, alitarajiwa kuachana rasmi na Klabu ya Manchester United baada ya mechi ya jana kutokana na mkataba wake kufikia tamati.

Jana ilikuwa ndiyo mwisho wa msimu wa Ligi Kuu ya England kwa msimu wa 2018/19 na pia ndiyo mwisho wa mkataba wa kiungo huyo raia wa Hispania na Mashetani Wekundu.

Taarifa juu ya kuondoka kwake zimethibitishwa rasmi baada ya kipindi kirefu cha tetesi juu ya mustakabali wa mchezaji huyo klabuni hapo.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 29, alijiunga na United mwaka 2014 kipindi klabu hiyo ikinolewa na kocha Mholanzi Louis van Gaal.

Herrera alijiunga na United akitokea Athletic Bilbao ya Hispania, na inaelezwa kuwa ataelekea kujiunga na miamba ya Ufaransa klabu ya Paris St-Germain kama mchezaji huru.

United walijaribu kumbakiza Herrera, lakini hawakuafikiana na mahitaji aliyokuwa akiyataka mchezaji huyo.

Imearifiwa kuwa mchezaji huyo alighadhibishwa na klabu hiyo kuchukua muda mrefu mpaka kukaa naye kwenye meza ya mazungumzo. Pia imearifiwa kuwa alitaka aongezewe mshahara na kulingana na wachezaji ambao wanapokea donge kubwa klabuni hapo.

Uongozi wa klabu ya United uliona kuwa matakwa hayo ya Herrera ni makubwa, na kushindwa kuafikiana naye.

Katika miaka yake mitano Old Trafford, amefunga mabao 20 katika michezo 189 na kutwaa Kombe la FA, Ligi ya Euoropa na Kombe la Ligi.

Herrera, ambaye alishinda tuzo ya Mchezaji Bora wa United mwaka 2017 baada kupigiwa kura na mashabiki, amesema, "kuna wekundu ndani ya moyo wangu."

"Kuchezea klabu kubwa zaidi England imekuwa ni heshima kubwa sana kwangu. Kila wakati nilipoiwakilisha klabu hii, katika kila mechi, katika ushindi na kufungwa, hata pale nilipokuwa nipo benchi, nilikuwa najua fika uzito wa klabu hii."

Mechi ya jana dhidi ya Cardiff pia ilikuwa ya mwisho kwa nahodha Antonio Valencia, 33, ambaye anaachana na United baada ya kuchezea timu hiyo kwa miaka 10.

Beki huyo wa kulia na winga alijiunga na United mwaka 2009 na ameshinda mataji mawili ya Ligi Kuu, Kombe la FA, makombe mawili ya Ligi na Kombe la Ligi ya Europa.

Mchezaji huyo kutoka Ecuador, ambaye ameichezea United mechi tisa tu msimu huu, amesema anataka aendelee kusakata kabumbu kwa walau miaka miwili au mitatu zaidi.

"Uamuzi huu unamaanisha kila kitu kwangu. Ni mchanganyiko wa huzuni na furaha," Valencia ameliambia shirika la habari la kimataifa la Pres Association.

"Huzuni kwa sababu nimeshinda kila taji kama mchezaji kwenye klabu hii, na nitazikumbuka sana zama hizo.

"Ni huzuni pia kwa sababu tumepokea vipigo vikali kama timu, lakini shukrani kwa kuungwa mkono na mashabiki tumejinusuru na ninaamini hivi karibuni watapata mafanikio wanayostahili."

# Mkhitaryan ruksa kuichezea Arsenal nchini Azerbaijan

**LONDON, England**

NYOTA wa Arsenal, Henrikh Mkhitaryan ameambiwa na maofisa wa nchini Azerbaijan kwamba ataruhusiwa kuingia kwenye nchi hiyo kwenda kuitumikia timu yake katika fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Chelsea, Mei 29, mwaka huu.

Kulikuwa na wasiwasi wa kiungo huyo kushindwa kwenda kucheza katika fainali hiyo itakayofanyika kwenye mji wa Baku baada ya kuwapo kwa tofauti za kisiasa baina ya nchi yake ya Armenia na Azerbaijan, ambazo ziliwahi kupigana vita miaka mitatu iliyopita.

Hofu ya awali ilikuwa kwamba huenda Mkhitaryan asingeruhusiwa kupata kibali cha kuingia nchini humo baada ya uhasama huo ambao haukupatiwa ufumbuzi wowote wa kidiplomasia.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Azerbaijan, Leyla Abdullayeva, alisema mambo ya kisiasa hayawezi kupewa nafasi na kuwa kikwazo cha kumzuia mchezaji huyo asiende kuisaidia timu yake kubeba ubingwa.

Alisema: "Matukio makubwa ya michezo yamefanyika Azerbaijan na wanamichezo wa Armenia wamekuja kushiriki. Michezo na siasa ni vitu viwili tofauti."

Hata hivyo, Arsenal bado wanataka kuhakikishiwa na Uefa kuhusu usalama wa mchezaji wao atakapokwenda Baku. Arsenal inahitaji kushinda Ligi ya Europa ili kukata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.




# Lukaku sasa kutulia Manchester United

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester Unted, Romelu Lukaku, ataendelea kubaki katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu baada ya kununua jumba lenye thamani ya pauni milioni tatu karibu kabisa na uwanja wa mazoezi wa timu hiyo.

Kulikuwa na taarifa kwamba Lukaku anaweza kuwa mmoja wa wachezaji watakaofungasha virago vyao na kuachana na Man United mwishoni mwa msimu huu, lakini kitendo chake hicho cha kununua makazi mapya karibu na uwanja wa mazoezi wa timu hiyo kimemaliza tetesi za Mbelgiji huyo kutaka kutimkia Italia.

Jengo hilo lilipo huko Altrincham, Gtr Manchester ni la ghorofa nne ambapo ndani yake kuna chumba cha sinema, gym, baa, chumba cha kucheza mpira wa meza, chumba cha mvuke pamoja na studio ya kurekodia muziki. Lukaku anaajiri pia mpishi wake maalumu kutoka Paris, Ufaransa.

Kwa mwezi sasa, Lukaku amekuwa akidaiwa kwamba huenda akaachana na Man United, lakini maisha yake yanaonekana kutulia jijini Manchester ambapo Januari mwaka huu, mpenzi wake mrembo Sarah Mens alijifungua mtoto wao wa kwanza wa kiume, Romeo.

"Ilionekana kama angehama timu hiyo mwishoni mwa msimu, lakini sasa anaonekana kutulia na kubaki. Kwa sasa amekuwa na familia hivyo anahitaji kuwa na sehemu ambayo atapaita nyumbani. Amepata nyumba nzuri sana," kilibainisha chanzo kimoja kuhusu suala hilo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN HAMTIKISI SIMEONE KUTUA BARCA

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, hana hofu ya kumpoteza mshambuliaji wake, Antoine Griezmann kwa Barcelona mwishoni mwa msimu huu.

Majaliwa ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano yamekuwa shakani kutokana na uvumi wa kuzagaa kwamba anaondoka klabuni hapo.

Griezmann alikataa uhamisho wa kwenda pale Barca mwanzoni mwa msimu 2018-19, lakini uvumi wa hivi karibuni umebainisha kwamba, mchezaji huyo ataondoka kwa miamba hao.

Lakini Simeone amepuuzia uvumi huo kuhusu mchezaji huyo raia wa Ufaransa, ambaye amefunga mabao 15 kwenye La Liga msimu huu.

"Tangu uvumi ulipoanza kuhusu Griezmann kwenda Barcelona na vyombo vya habari kuzidi kuukoleza, mara zote nimekuwa nikisema kwamba nafikiri yupo sawa.

"Ametulia na anafuraha na wachezaji wenzake," alisema Simeone wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari juzi.

"Yeye ni nahodha kwa timu yetu na mara zote tumekuwa tukimpa nafasi muhimu ambayo anatastahili kuipata, lakini bila shaka hatupo ndani ya kichwa chake kujua mipango yake.

"Kama ana kitu cha kusema atasema siku moja. Tunafikiri atabakia na sisi. Sina hofu ya kumpoteza. Yeye ni nahodha wetu na chochote kitakachotokea kuanzia sasa hatukitegemei sisi."

Atletico inahitaji pointi moja katika mechi zake mbili zilizobakia, nyumbani dhidi ya Sevilla na ugenini dhidi ya Levante, ili kuishikilia nafasi ya pili kwenye msimamo wa La Liga dhidi ya Real Madrid.

Na huku kikosi chake kikiwa kimeshinda mfululizo mechi zilizopita, Simeone ana matumaini ya kukiimarisha msimu ujao na kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya kushinda mataji.

"Kama ninavyojijua, naweza kuwaambia kwamba tutakuwa na hamasa kubwa zaidi msimu ujao," alisema.

"Utakuwa msimu mgumu kama mingine iliyotangulia na kwa sababu ya nafasi tutakayokuwa nayo mwishoni mwa msimu huu.

"Naweza kuwaambia kwamba wachezaji watakuja na ari kubwa zaidi, wakitaka kujiimarisha zaidi wenyewe na hicho ndio tunachokitaka.

Griezmann, (Jan) Oblak, (Jose) Gimenez, (Diego) Godin, Gabi na wachezaji wote waliokuja hapa wamepata mafanikio hadi kuwa katika kiwango walichonacho sasa.

"Mara zote nimekuwa nasema, hatusajili wacheaji kwa euro milioni 150, euro milioni 120 au euro milioni 100 - tupo hapa kuwajenga wachezaji.

"(Thomas) Lemar amekuwa mchezaji ghali zaidi katika historia ya Atletico Madrid na ni kweli kwamba msimu huu ulikuwa mgumu kwake, lakini sina shaka kwamba msimu ujao utakuwa wa kuvutia kwake, na hivyo ndivyo tunavyofanya mambo yetu."

## KWA UFUPI

**GUARDIOLA AITOA HOFU CITY**

Pep Guardiola ameihakikishia Manchester City hana mpango wa kuachia ngazi kuinoa klabu hiyo licha ya kuwapo taarifa zinazomhusisha na kutua Juventus majira haya ya joto. ***(Express)***

**GUEYE AIPAGAWISHA UNITED**

Manchester United inavutiwa na kiungo wa Everton, Idrissa Gueye, 29, na Everton ikihitaji takriban pauni milioni 40 ili kumwachia nyota huyo wa kimataifa wa Senegal. ***(Mail)***

**HUDSON-ODOI BADO LULU BAYERN**

Bayern Munich bado inavutiwa na winga wa Chelsea na England, Callum Hudson-Odoi, 18. ***(Bild - in German)***

**'OZIL HAONDOKI ARSENAL'**

Mesut Ozil, 30, hataondoka Arsenal majira haya ya joto na Mjerumani huyo ataendelea kubaki 'Gunners' hadi mwishoni mwa mkataba wake. ***(Mirror)***

**GIROUD KUREJESHWA UFARANSA**

KLABU ya Ligue 1, Nice inavutiwa kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Mfaransa Olivier Giroud, 32, majira haya ya joto, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Ufundi wa klabu hiyo, Gilles Grimandi. ***(Canal Football Club via Bleacher Report)***

**BALE, ZIDANE KIMENUKA REAL**

KUMEKUWA na mpasuko mkubwa kati ya mshambuliaji wa Real Madrid, Gareth Bale na kocha wa klabu hiyo, Zinedine Zidane, hiyo ikiwa na maana mustakabali wa baadaye wa nyota huyo wa kimataifa wa Wales haupo tena klabuni hapo. ***(AS - in Spanish)***

**RAKITIC ANUKIA KUTUA INTER**

Inter Milan inakaripia kuipata saini ya kiungo wa Barcelona, Mcroatia Ivan Rakitic, 31, kwa pauni milioni 43. ***(Goal)***

**DE LIGT AKARIBIA KUTUA BARCA**

Barcelona inakaribia kumsajili beki wa kati wa Ajax, Mholanzi Matthijs de Ligt, 19, na pia inavutiwa na kuipata saini ya mchezaji mwenza katika klabu hiyo, Donny van de Beek, 22. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**SPURS KUMFUATA FERNANDES**

Tottenham inapanga kumfuata nyota wa kimataifa wa Ureno na Benfica, Gedson Fernandes, 20, anayethaminishwa na pauni milioni 35. ***(Mirror)***

**TIELEMANS KURUDI MONACO**

KIUNGO wa Leicester, Mbelgiji Youri Tielemans, 22, anatarajia kurudi Monaco majira haya ya joto wakati mkataba wake wa mkopo utakapomalizika mwishoni mwa msimu. ***(VTM Nieuws - in Dutch)***

**RICHARLISON AZIVUTIA PSG, ATLETICO**

Paris St-Germain na Atletico Madrid zote zinavutiwa na mshambuliaji wa Everton, Mbrazil Richarlison, 22, anayethaminishwa na pauni milioni 70. ***(Mirror)***

**EVERTON YANOGEWA NA GOMES**

Everton imefungua meza ya mazungumzo na Barcelona kuhusu uwezekano wa kuufanya mkataba wa mkopo wa kiungo Mreno Andre Gomes, 25, kuwa wakudumu. ***(Liverpool Echo)***

**SOUTHAMPTON KUSAJILI MITROVIC**

Southampton inapanga kutoa pauni milioni 30 majira haya ya joto ili kuipata saini ya mshambuliaji wa Fulham, Aleksandar Mitrovic, 24. ***(Express)***



HABARI MICHEZO

# BOCCO AISHUKURU SPORTPESA AKIPANIA KUITUNGUA SEVILLA

**Na Mwandishi Wetu**

Nahodha wa Klabu ya Simba, John Bocco ameishukuru Kampuni ya Kubashiri Matokeo Michezoni ya SportPesa, kwa kufanikisha ujio wa Sevilla nchini Tanzania na amesema watatumia mechi hiyo ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya Hispania, La Liga kunadi vipaji vyao huku akiahidi ushindi dhidi ya timu hiyo yenye historia kubwa barani Ulaya.

Sevilla FC inatarajia kuwasili nchini Mei 21 na kucheza na Simba Mei 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa chini ya uratibu wa SportPesa Tanzania kwa kushirikiana na La Liga na usimamizi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Bocco alisema watatumia fursa hiyo kuonyesha uwezo wao pamoja na kuwa wanacheza mechi ya kihistoria ya kwanza dhidi ya timu inayotoka Bara la Ulaya.

Alisema wanajiona ni wenye bahati kubwa na kuipongeza SportPesa Tanzania kwa kufanikisha ziara ya timu hiyo.

"SportPesa Tanzania ni wadhamini wetu. Wanastahili pongezi kubwa sana kwani wamefanya zaidi ya majukumu yao kwa kuileta timu ya Sevilla ambayo imewahi kutwaa ubingwa wa Europa. SportPesa wameonyesha mfano na kudhihirisha kuwa pamoja na kuwa wadhamini, pia wanapenda kuona timu wanayoidhamini inacheza mechi za kimataifa ili kukuza kiwango chao," alisema Bocco. Alisema hana wasiwasi na viwango vya wachezaji wenzake kwani hivi karibuni wametoka kucheza hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kukutana na timu kama TP Mazembe, Al Ahly, AS Vita na kujipima uwezo wao.

"Nawaomba mashabiki wafike kwa wingi siku ya mechi na tunawaahidi, wachezaji hatutawaangusha. Tutapigana kiume ili kushinda mechi hiyo. Uwezo huo tunao na makocha wameanza kutupa mbinu mbalimbali kwa ajili ya mechi hiyo na Ligi Kuu ya Tanzania Bara," alisema.

Golikipa wa timu ya Sevilla, Tomas Vaclik, alisema kuwa wamejipanga kufanya vema katika mechi dhidi ya Simba na watashusha kikosi cha kwanza.

Mechi hiyo iliyoandaliwa na SportPesa, ambayo itapigwa Uwanja wa Taifa kuanzia majira ya saa 1:00 usiku, tayari viingilio vimetangazwa kuwa ni Sh. 5,000 mzunguko, Sh 15,000 VIP B na Sh. 100,000 kwa Platinum.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Suleiman Jaffo, akionyesha ufundi wa kupiga danadana wakati wa uzinduzi wa michuano ya Copa Coca-Cola UMISSETA kwa Mkoa wa Dodoma katika hafla iliyofanyika jana mkoani humo. Sambamba na mashindano hayo, Waziri Jaffo pia alizindua Kampeni ya 'Rejesha na Ushinde' kitaifa inayolenga kutunza mazingira kwa kukusanya chupa za plastiki katika shule zinazoshiriki kwenye mashindao ya Copa Coca-Cola UMISSETA. **MPIGAPICHA WETU**

# Copa Coca-Cola UMISSETA yaja na 'Rejesha na Ushinde'

**Na Mwandishi Wetu**

Kampuni ya vinywaji baridi ya Coca-Cola, imezindua rasmi Kampeni ya 'Rejesha na Ushinde' ambayo imebuniwa kwa ajili ya kufanikisha ukusanyaji wa chupa za plastiki katika shule zinazoshiriki michezo ya Copa Coca-Cola UMISSETA mwaka huu.

Dhamira ya kampeni hiyo ni kujenga utamaduni wa kutunza mazingira, si tu kwa shule shiriki, lakini pia kwa jamii zinazozunguka maeneo hayo na Taifa kwa ujumla.

Akizindua kampeni hiyo jijini Dodoma, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Naibu Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Josephat Kandege, aliipongeza Kampuni ya Coca-Cola kwa kuja na kampeni hiyo akisema itawawezesha wanafunzi kuwajibika kwa jamii katika kutoa elimu juu ya namna ya kuyatunza mazingira.

"Nimeambiwa kupitia mpango huu, Coca Cola inataka kuwawezesha wanafunzi katika shule za sekondari kuwa sehemu ya kulinda mazingira shuleni kwa kukusanya chupa za plastiki. Nilipewa taarifa pia watatoa zawadi ya kukarabati kiwanja cha mpira wa miguu kwa shule moja itakayokusanya idadi kubwa ya chupa za plastiki pamoja na zawadi nyingine kabambe kwa shule zitazofanya vizuri katika zoezi hili," alisema Kandege.

Naibu Waziri huyo aliahidi kuunga mkono jitihada hizo huku akitoa wito kwa walimu wa shule za sekondari kusaidia mpango huo ili kuhakikisha usafi unaimarika katika maeneo yao ya kazi.

"Kampeni ya Rejesha na Ushinde, ni zaidi ya ushindi wa tuzo shuleni,"alisema Haji Mzee, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Mahusiano kwa Umma Coca-Cola Kwanza.

"Kupitia kampeni hii, tunawapa wanafunzi na walimu nchini kote fursa ya kujifunza zaidi kuhusu faida za mazingira kupitia kampeni hii na kuwapa motisha wengine kufanya jambo linalofanana na hili katika nyumba na jamii zao,"alifafanua.

Aliongeza: "Tunatarajia kuona shule nyingi zikishiriki katika jitihada hizi na tunawapa nafasi wadau wengine ili kufanya nao kazi hususan wanaovutiwa na mpango huu muhimu, lengo ni kuhakikisha tunayaweka mazingira ya shule zetu kuwa safi,"

Haji aliongeza kuwa Kampuni ya Coca-Cola inatarajia kutoa zawadi mbalimbali ikiwamo zawadi kuu ambayo ni kugharamia urekebishaji wa kiwanja cha mpira wa miguu kwa shule moja itakayoibuka mshindi wa jumla katika kukusanya chupa za plastiki katika kipindi chote cha mashindano ya Copa Coca-Cola. Sambamba na zawadi hiyo, zawadi nyingine ni pamoja na mashine ya 'Photocopy', Projekta mbili, Laptop 108, Kompyuta za mezani 11, 'Tablet' 108, Saa 12, Jezi 1,176 na mipira 360 kwa shule zitakazokusanya idadi kubwa ya chupa za plastiki kwa kila mkoa.

# JKU mapumzikoni ikipisha Ramadhan

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya JKU ambayo ni moja ya timu za Ligi Zanzibar, imefunga rasmi kufanya mazoezi katika kipindi hichi cha Ramadhan ili kupisha mwezi huo sambamba na kuwapumzisha wachezaji wao.

Akizungumzia maendeleo ya timu hiyo katika mwezi huu wa Ramadhan, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hassan Ramadhan Pele, alimwambia mwandishi wetu juzi kuwa, wameamuwa katika kipindi hiki wawapumzishe wachezaji kutokana na kwamba walichoka sana katika kipindi cha ligi iliyomalizika mwezi uliopita.

Alisema katika kipindi cha ligi wachezaji walitumika sana kutokana na ratiba kuwa ngumu, hivyo wameona katika kipindi hichi cha mfungo wa Ramadhan wawapumzishe wachezaji wao hadi mwezi huu utakapomalizika.

**"Tumeamua tusitishe mazoezi ili kupata muda mzuri wa kupumzika na kufunga Ramadhan kwa utulivu," alisema.**

Alisema kipindi hichi wakati wapo mapumzikoni, pia wanajiandaa na taratibu za kutafuta wachezaji watakaowasajili kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu wa 2019/20 ili matarajio yao msimu ujao ya kuwa timu bora zaidi itakayoweza kuhimili vishindo vya ligi na kutwaa ubingwa yaweze kutimia.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.SIMBA | 32 | 26 | 3 | 3 | 69 | 14 | 81 |
| 2.YANGA | 35 | 25 | 5 | 5 | 54 | 25 | 80 |
| 3.AZAM | 35 | 19 | 11 | 5 | 50 | 21 | 68 |
| 4.MTIBWA SUGAR | 34 | 14 | 7 | 13 | 36 | 28 | 49 |
| 5.LIPULI | 35 | 12 | 12 | 11 | 30 | 33 | 48 |
| 6.KINONDONI MC | 35 | 10 | 16 | 9 | 35 | 25 | 46 |
| 7.SINGIDA UNITED | 35 | 11 | 11 | 13 | 28 | 35 | 44 |
| 8.NDANDA | 34 | 11 | 11 | 12 | 22 | 31 | 44 |
| 9.TANZANIA PRISONS | 35 | 10 | 13 | 12 | 27 | 28 | 43 |
| 10.KAGERA SUGAR | 35 | 10 | 13 | 12 | 31 | 37 | 43 |
| 11.MBAO | 35 | 11 | 10 | 14 | 23 | 35 | 43 |
| 12.RUVU SHOOTING | 35 | 10 | 12 | 13 | 33 | 40 | 42 |
| 13.ALLIANCE | 35 | 10 | 11 | 14 | 28 | 38 | 41 |
| 14.STAND UNITED | 35 | 11 | 8 | 16 | 33 | 44 | 41 |
| 15.COASTAL UNION | 34 | 9 | 14 | 11 | 30 | 41 | 41 |
| 16.MBEYA CITY | 33 | 11 | 7 | 15 | 32 | 36 | 40 |
| 17.BIASHARA UNITED | 34 | 10 | 10 | 14 | 26 | 31 | 40 |
| 18.JKT TANZANIA | 35 | 9 | 13 | 13 | 22 | 32 | 40 |
| 19.MWADUI | 35 | 10 | 7 | 18 | 38 | 48 | 37 |
| 20.AFRICAN LYON | 34 | 4 | 10 | 20 | 21 | 46 | 22 |

Michezo
Jumatatu Mei 13, 2019
Nipashe



Griezmann hamtikisi Simeone kutua Barca

HABARI UK 30

MABINGWA...



Sergio Aguero akiifungia Manchester City bao la kusawazisha wakati wakishinda 4-1 ugenini dhidi Brighton, kwenye mechi ya funga msimu wa Ligi Kuu England. Kwa matokeo hayo City imetwaa ubingwa ikiizidi Liverpool kwa pointi moja ambayo nayo jana iliichapa Wolves 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA KUIVAA AZAM NA MBINU MBADALA

●●●Aussems akwepa leo isikutane na balaa kama la Kagera Sugar Uhuru, asema...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI Simba ikitaka kuendelea kujiimarisha katika mbio za kuwania ubingwa, Azam FC wao watakuwa wanahitaji kuweka heshima dhidi ya vinara hao watakapokutana katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa, Azam FC ikiwa chini ya Mholanzi Hans van der Pluijm pamoja na Mzalendo Juma Mwambusi, ilichapwa mabao 3-1.

Hata hivyo, Simba leo itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 na Kagera Sugar katika mechi iliyopita ya ligi hiyo, huku Azam FC ambayo haina tena nafasi ya kutwaa ubingwa huo msimu huu wakiwa na kumbukumbu ya kutoka suluhu na KMC FC zote za jijini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, alisema timu yake itaendelea kupambana kuhakikisha inapata ushindi licha ya kubanwa na ratiba ngumu msimu huu.

**Aussems alisema wanahitaji kutumia mbinu mbadala ili kuhakikisha wanacheza katika kiwango cha juu na hatimaye kuibuka na ushindi katika mechi ya leo na kubakiza pointi chache za kutetea ubingwa wa ligi hiyo wanaoushikilia.**

"Haitakuwa mechi rahisi kwa pande zote mbili, sisi tuna malengo ya ubingwa na wenzetu nao wana malengo yao, wachezaji wanahitaji kuongeza umakini katika mechi hii, najua Azam hawana presha ya kutwaa ubingwa, lakini wanahitaji kushinda ili kujiweka katika rekodi nzuri," alisema Aussems.

Naye mshambuliaji aliyerejesha makali yake, Emmanuel Okwi, alisema wamejipanga kuendelea kushirikiana ili waweze kushinda mechi ya leo na nyingine tano zilizobakia katika msimu huu.

"Tunahitaji kufikia malengo yetu, huu ni mwisho wa msimu, tungependa kuona tunamaliza vizuri na hii itatusaidia kujipanga kwa ajili ya msimu ujao, Simba nguvu moja," alisema mshambuliaji huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdul Mingange, alisema anatarajia kuona mechi yenye ushindani kwa sababu timu zote zina wachezaji wazuri na wenye uzoefu.

"Tunafahamiana, hii inaongeza ushindani na ugumu wa mechi, tumejipanga kurekebisha makosa ya nyuma, tulifungwa mechi ya kwanza na safari hii tungependa kuona tunabadilisha matokeo," alisema kocha huyo.

Simba inaongoza ligi ikiwa na pointi 81 ikifuatiwa na Yanga yenye pointi 80 na Azam FC yenye pointi 67 iko katika nafasi ya tatu.

## Zahera apania heshima Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

HESHIMA! Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema anahitaji kuona timu yake inamaliza kwa kupata ushindi na kuweka heshima katika mechi zote tatu zilizosalia za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Mechi tatu ambazo zimebakia za Yanga ni dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa kesho na kisha wataikaribisha Mbeya City Mei 22 na watafunga pazia la ligi hiyo msimu huu kwa kuivaa Azam FC hapo Mei 28, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera, ambaye pia ni Kocha Msaidizi wa Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), alisema licha ya kuwapo na changamoto za waamuzi, bado timu yake itapambana kuhakikisha wanapata ushindi.

Zahera alisema mechi za mwisho wa msimu huwa na ushindani, na ni vema wasimamizi wakawa makini ili timu inayostahili kushinda iweze kupata haki yake.

Alisema pia hali ya majeruhi ilikuwa ni changamoto nyingine ambayo imemsumbua katika kikosi chake msimu huu, lakini akaweka wazi kwamba hali hiyo ni ngumu kuiepuka kikosini.

"Matatizo yalikuwa mengi, kama leo mchezaji huyu unamkosa kwa sababu ni mgonjwa, mchezaji mwingine anakosekana kwa sababu ya kadi, ndio mpira wa miguu ulivyo, tutafanya kile kilichoko ndani ya uwezo wetu ili kumaliza tukiwa tumeshinda mechi zote tatu," alisema kocha huyo.

Naye Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, alisema jana kuwa kikosi chake kimejiandaa kutoa "dozi" kwa Yanga baada ya kuwapa kichapo wababe wao, Lipuli FC.

"Sisi ndio Wazee wa kazi, tumeshawapiga wababe wao, Lipuli FC, sasa tunawasubiri Yanga, tunajua mahali wanapokamatika, tumejiandaa vema kwa mchezo huo, wanatufahamu na wanatujua" alisema kiongozi huyo ambaye kwa taaluma ni mwalimu wa somo la Hisabati katika Shule ya Msingi Makumbusho, jijini Dar es Salaam.

Yanga ilirejea jijini tangu juzi jioni ikitokea Musoma ambapo ilipoteza mchezo wake wa ligi kwa kufungwa bao 1-0 na wenyeji, Biashara United inayofundishwa na beki wa zamani wa Simba, Amri Said.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >